
# HATUA ZA KWANZA

## Hamasisheni kanisa lenu kwenye shamba la mavuno ya Mungu




 ©2005 e3 Partners Ministry 

# HATUA ZA KWANZA

## Hamasisheni  kanisa lenu
## Kwenye shamba la mavuno ya Mungu

***KISWAHILI Translation***

**e3 Partners Ministry**

**2001 W. Plano Pkwy., Suite 2600**

**Plano, Texas 75075**

**214-440-1101**

**first.steps@ e3partners.org**

**www.e3partners.org**

**©2005 e3 Partners Ministry**

Umeruhusiwa na kuhimizwa kutoa nakala na kusambaza vifaa hivi katika maandishi yoyote iwapo.
utatia ilani ya haki ya kubuni ifuatayo
©2005 e3 Partners Ministry Used by permission"
Utaonyesha kama kuna mabadiliko yoyote yamefanywa
Usilipishe ada inayozidi ya uchapishaji
Usichapishe nakala zinazozidi elfu moja (1,000)

Ikiwa ungependa kutuma vifaa hivi kwa mtandao na ikiwa matumizi unaokusudia ni tofauti na yale yaliotajwa awali, tafadhali wasiliana na:
mike.jorgensen@e3partnerspartners.org

Maandiko (matakatifu) yaliyonakiliwa yametolewa katika
BIBLIA TAKATIFU……………………………………………

# JEDEWALI LA YALIYOMO


ukurasa wa

**UTANGULIZI**…………………………………………………………… 5

**MAONO YA KUANZISHA MAKANISA MAPYA**……………….. 9

**KITENDO: HATUA ZA KWANZAA KUANSISHA MAKANISA MAPYA**… 27

Kuomba…………………………………………………………… 27

Fanyeni Uinjilisti………………………………………………. 43

Fanyeni Wanafunzi…………………………………………….. 63

Kusanyikeni pamoja…………………………………………… 77

Endelezeni viongozi…………………………………………… 93

Zidisheni……………………………………………………….. 111

**JITOLEENI KUANZISHA KANISA**………………………………. 123

**MKAKATI WA UKURASA WA UTENDAJI KAZI**…………….. 133


Kuanzisha kanisa = maono + kitendo


Kuanzisha kanisa = maono **ya Mungu** + kitendo **kilichoelekezwa na Roho Mtakatifu**



©2005 e3 Partners Ministry

**KIDOKEZO CHA KUFUNDISHA**

- Toa mbegu ukianza kufundisha somo hili.
- Waulize wanafunzi kuelezea muda wa mmea kuanzia majira ya kupanda mpaka kuvuna.
- Soma kwa sauti Marko 4:3-8.
- Mjadiliane mawazo katika fumbo la mavuno.




# UTANGULIZI

**MAWAZO MAKUU**

- Maono ni picha wazi ya akili ya kile kilicho mbele yako kitakuwa je.
- Twatumaini kitabu hiki cha maelezo kitakusaidia kuona maono ya Mungu kwa kanisa lenu.
- Mtumiavyo kitabu hiki, jibu changa moto za "Hatua za Kwanza" katika kila sura. Zitawasaidia kuendeleza mkakati wa kazi kuona kwamba maono huwa hali ya ukweli.
- Kitabu hiki kitawasaidieni KUWAANDAA watu kanisani mwenu KUFANYA UINJILISTI kwa majirani wapya, ili KUANZISHA makanisa mapya.

## 1. FUMBO LA MAVUNO

Kila mkulima ataka mavuno. Macho yake yaona shamba tupu ambalo limefunikwa kwa majani na magugu na kufunikwa na mawe.

Lakini akili yake yaona shamba lake au upande wa kilima kilichofunikwa na mimea yenye afya. Na ahadi katika akili yake, si shida mbele ya macho yake, zampeleka katika shamba lake kufanya kazi.

Kwanza, avunja mchanga mgumu,ili mbegu ziweze kukua kwa urahisi. Halafu apanda mbegu. Zikuavyo ang'oa magugu ambayo yajaribu kusonga mimea mipya. Ahakikisha kuwa ina maji ya kutosha na kuilinda kutokana na ndege na wadudu.

Afanya sehemu yake, akijua ya kwamba Mungu pekee ana nguvu ya kufanya mbegu zimee.


Wakati ukitimia, mkulima huenda shambani kukusanya matunda ya mavuno yake na kuyapeleka katika ghala lake. Pale, huchukua mbegu mpya kwa msimu ujao wa upanzi – mbegu nyingi zaidi kuliko alizoanzia. Kwa hiyo mavuno yake huongezeka kila mwaka. Hicho ndicho kile Yesu alichozungumzia katika Marko 4: 3-9.

> Sikilizeni, tazama mpanzi alitoka kwenda kupanda, ikawa alipokuwa akipanda, mbegu nyingine ilianguka kando ya njia wakaja ndege wakaila. Nyingine ikaanguka penye mwamba, pasipokuwa na udongo mwingi, mara ikaota kwa kuwa na udongo haba, hata jua lilipozuka, na kwa kuwa haina mizizi ikanyauka. Nyingine ikaanguka penye miiba na ile miiba ikamea ikaisonga isizae matunda. Nyingine ikaanguka penye udongo ulio mzuri zikazaa matunda, zikamea na kukua na kuzaa, moja thelathini, moja sitini na moja mia. Akasema, aliye na masikio ya kusikia, na asikie. (Marko 4:3-9)

### Hatua za Kwanza


©2005 e3 Partners Ministry

**Hapa ni vile muda wa kupanda na kuvuna kwaonekana**




Kuanzisha makanisa kunafanana na majira ya kupanda na kuvuna. Jaribu kuwazia kwamba jamii yako ni shamba. Yaonekanaje kwako? Ni tupu, imesongwa na magugu ya hekima ya kidunia (maarifa) na kutatanishwa na vizuizi vya mawe mengi dhidi ya Injili? Yaonekana kwamba haitawahi kuzaa matunda?

Au Mungu ameweka picha tofauti akilini mwako? Je waweza kuwaona majirani wako wakijaawa na furaha na kumwabudu Mungu? Waweza kuwaona huru kutokana na ngome za dunia? Waweza kuwaona wakishinda kila kizuizi?

Kile twaona katika akili zetu kinaitwa maono. Maono ni picha wazi ya vile hali itakavyokuwa wakati ujao .Ni lazima ije kwetu kutoka moyoni mwa Mungu kupitia Neno lake na Roho Wake. Maono huleta tamaa inayokua, kutaka kuona kwa macho yetu picha sawa na ile tulionayo akilini mwetu. Hiyo yatufanya **TUOMBE**, ambayo, kama jembe la kukokotwa, yavunja ardhi ngumu katika ulimwengu wa kiroho.

Injili ni mbegu yetu, ambayo twapanda tukifanya **UINJILISTI**. Biblia yaahidi kuwa tupandavyo mbegu zaidi ndivyo mavuno yatakavyo kuwa mengi.'

**Mavuno yatakapokuwa tayari, twahitaji KUKUSANYA** PAMOJA waumini wapya katika vikundi viitwavyo MAKANISA. Makanisa ni watu, si majengo- watu wamjuao na kumpenda Mungu na wanao **WAFANYA WANAFUNZI** na kuwasaidia kuwa zaidi kama Yesu.

Wale ambao wamekomaa zaidi hukuza **VIONGOZI** makanisani na kuendeleza mzunguko.

Na tokeo lake, makanisa **YANAZIDI KUONGEZEKA.** Moja huwa mbili, kumi huwa ishirini mia tano huwa elfu moja!

Kama vile ilivyo katika kitabu cha Matendo ya Mitume.

## Hatua za Kwanza


©2005 e3 Partners Ministry

## 2. KUSUDI LA HIKI KITABU CHA MAELEZO

Dunia iko tayari kwa mavuno siyo kama hapo awali. Na Ufalme wa Mungu unaendelea mbele.

Kitabu hiki cha maelezo ni cha viongozi wa kanisa ambao, kama Mtume Paulo, wamekusudia kuwa sehemu ya kile Mungu anafanya leo. Kitawaandaa kuchukua **HATUA ZA KWANZA** kuanzisha makanisa mapya na kuona Ufalme wa Mungu ukiimarishwa katika jamii zao. Lakini muhimu zaidi, itawawezesha kuwafunza watu katika kusanyiko lao- kama vile Paulo alivyomfundisha Timotheo – kusaidia kuanzisha makanisa mapya kando yao.

Mwajifunza, Mwatenda, Wanawatazama., Halafu wanatenda, Mwawashauri wafanyapo huduma.

Siyo kitabu chenu tu kuwasomea kusanyiko lenu au kuhubiri Jumapili tu. Katika Biblia mwandishi wa kitabu cha Yakobo atuhimiza "kuwa watendaji wa neno, na siyo wasikilizaji tu." Ikiwa twasikia tu na hatutendi, atuonya, twajidanganya katika kuamini kwamba tunamtii Kristo. Weka kwenye matendo kile wajifunza katika kitabu hiki cha maelezo.

## 3. JINSI YA KUTUMIA KITABU CHA MAELEZO

Tumia kitabu hiki mmoja kwa mwingine- Paulo kwa Timotheo – kama kocha au mshauri. Kitumie katika kikundi kidogo cha viongozi ambao wanaanzisha kanisa jipya, au kitumie kufunza kusanyiko lako lote.

Hiki kitabu cha maelezo, kwanza chatoa amri za Kristo, halafu chaonyesha jinsi Paulo alivyotii hizo amri.

**Tumia mkakati wa kazi kwenye karatasi katika ukurasa wa 133 unapofanya zoezi kupitia kitabu hiki cha maelezo**

Kila sehemu ina "hatua za kwanza" changamoto. Changamoto hizo zauliza maswali kuwasaidieni kufikiri na kuomba juu ya jinsi mwaweza kutii amri za Kristo na kufuata kielelezo cha Paulo leo.

Mfanyavyo kazi kupita kitabu hiki cha maelezo, na Bwana awapeni jibu kwa kila changamoto liandike chini katika ukurasa kwenye mkakati wa kazi, ulioko mwishoni mwa kitabu hiki cha maelezo. Unapomaliza, utakuwa umeendeleza mkakati wa kuanzisha kanisa uliobuniwa hasa kwa ajili yako na kundi la kusanyiko lenu. Kumbuka kuwa la muhimu si kile unachojifunza. Ila la muhimu ni unachofanya na kile unachojifunza.

## 4. JE, HUDUMA YA 'e3 PARTNERS', NI NINI?

Huduma ya e3 Partners inalenga vitu vitatu:

**KUANDAA** wafuasi kwa


**KUFANYA UINJILISTI** katika maeneo yao ya ujirani, na

**KUANZISHA** makanisa mapya.

Kitabu hiki cha maelezo cha **hatua za kwanza** ni mojawapo ya vifaa vilivyopo, kutoka kwa Huduma ya e3 Partners kwa kukusaidia kama mchungaji au kiongozi kwa kuhamasisha **kanisa** lako kwa **KUANDAA, KUFANYA UINJILISTI NA KUANZISHA MAKANISA MAPYA.** Kwa vifaa vinginevyo, fikia mtandao wetu wa **www.e3partners.org.**

©2005 e3 Partners Ministry

# MAONO YA KUANZISHA MAKANISA MAPYA




 ©2005 e3 Partners Ministry 

**" Ukitaka kupanda kitu kitakachodumu kwa msimu**
**panda ua."**

**" Ukitaka kitu kinachodumu kwa maisha yote,**
**panda mti."**

**"Ukitaka kitu kitakachodumu milele,**
**panda kanisa."**

Kunukuu - David- Hesselgrave



**Alama ya moyo ambayo imetumiwa katika kitabu hiki cha maelezo, ina maana tatu:**

1. Mungu anatupenda. (Yohana 3:16)
   Alituumba kwa makusudi. (Waefeso 2:10)

2. Yatufaa kumpenda Mungu kwa moyo wetu wote.
   (Mathayo 22:37 na Mariko 12:30). Twaonyesha upendo wetu kwake kwa kumtii. (Yohanan 15:10)

3. Mungu anao moyo wa Upendo kwa ajili ya mataifa. Inatulazimu kuufuata moyo wake kwa kufikia mataifa. (Matendo 1:8)


©2005 e3 Partners Ministry

# MAONO YA KUANZISHA MAKANISA MAPYA

**MAWAZO MAKUU**

- Wakati Yesu alipopaa kutoka duniani, aliamuru wanafunzi wake kufanya wanafunzi. Atarudi tena hivi karibuni. Je, atakupata ukimtii?
- Paulo ni kielelezo cha mwanafunzi aliye na maono. Maono hayo yalimwongoza kumtii Kristo kwa kuanzisha makanisa mapya.
- Changamoto yako ya “Hatua za Kwanza” ni kutii amri za Yesu na kufuata kielelezo cha huduma ya Paulo.
- Muulize mkuu wa kanisa, Bwana Yesu, akuongoze kwa sehemu inayohitaji kanisa jipya. Ombeni na mpange kuhusu kuanzisha kanisa jipya pale.

## 1. FUMBO LA MAVUNO: MAONO

Wakulima wote wana maono. Maono ni tofauti kati ya jinsi mambo yalivyo na vile yanavyofaa kuwa au yangekuwa- maono hutazama mashamba matupu na kuyaona yamejazwa mimea. Wakulima wanajua wahitajika kufanya kazi kwa bidii ili waweze kubadilisha mashamba matupu kuwa mashamba ya mavuno, na wao hufurahia kujitolea mhanga kwa hayo.

Yesu aliwafunza wanafunzi wake kuona uwezekano kwa kila kitu kinacho wazunguka. Je, wewe waweza?

Hatua ya kwanza ni kutazama. Zuru maeneo ya ujirani wako pamoja na jamii, tazama pande zote na wazungumzie watu. Ikionekana kuwa hakuna chochote kinachotendeka, tazama karibu zaidi. Tazama kwa macho yako ya kiroho, na uote ndoto kuhusu mavuno ya mioyo inayowezekana. Muulize Mungu akupe maono Yake ya kupanua Ufalme Wake kwa kukutumia wewe na kanisa lako, kuanzisha kanisa jipya.

## 2. KUMBUKA: YOTE YAMHUSU YESU!

Kabla ya kuendelea zaidi, funga macho yako na uruhusu nia zako zihamishwe kwenda mbinguni yapata miaka zaidi ya elfu mbili iliopita. Je waweza kumfikiria Yesu akiwa enzini karibu na Babaye? Je, waweza kuuona utukufu? Je, waweza kusikia ibada ya malaika? (Yohana 17:5,24)

Halafu Babaye amwambia kuwa wakati umewadia wa kuenda. Bila kusita, bila kukataa, Yesu akaamka kutoka kwa enzi Yake…. Na papo hapo Mimba ikaumbika katika mfuko wa uzazi wa kijana msichana wa Mashariki ya Kati aitwaye Mariamu. Muumbaji wa ulimwengu akawa kitu kidogo sana cha kutazamwa kwa kupitia darubini, na asiye na nguvu. Miezi tisa baadaye, Mwana wa Mungu aliyeweka misingi ya dunia, akazaliwa akiwa hoi na akilia, akiwa amezungukwa na mifugo na mbolea, badala ya viumbe wa mbinguni (Luka 2:4-7).

 ©2005 e3 Partners Ministry 

Chini ya usimamizi wa mseremala na bibi arusi wake mchanga, Shina la Yese na Mzao wa Daudi, Nyota angavu ya Asubuhi, akakua katika hekima na kimo na kibali mbele ya Mungu na mwanadamu (Luka 2:52)

Akiwa karibu na umri wa miaka thelathini Yesu aliingia katika huduma yake ya hadhara. Alianza kwa kuwaalika wanaume kumi na wawili kumfuata. Na kwa muda wa miaka mitatu iliofuata akawabadilisha kuwa wanafunzi – yaani kuwa watu wa maono, imani, na uhodari, ambao siku moja watatumia kusaidia kubadilisha ulimwengu! (Luka 6:12-13, Matendo 17:6)

Wakati Yesu aliendelea kuwafunza hao kumi na wawili, aliyafunua maono yake kuhusu tume, akatoa mwito dhahiri wa kutenda! Basi tuanze na ziara fupi kupitia Injili ya Mathayo tukitazama vifungu fulani, vinavyofahamika sana.

## 3. TANGAZO KUU

**Soma Mathayo 16:18**
18 Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.

### 3.1 Je, Yesu aliahidi nini?

**Mimi** - Yesu - si wainjilisti, wachungaji, waalimu, mashemanzi au wazee viongozi – aliahidi atalijenga shirika.

Yesu hakuwahi kutuambia kuwa tujenge Kanisa Lake. Maono Yake yalikuwa makubwa sana kwetu. Alituambia kujenga wanafunzi mmoja kwa wakati mmoja. Tunapotii amri hiyo, yeye hutumia wanafunzi hao kulijenga Kanisa Lake. Na Baba Mungu anatukuzwa!

**Nita** – si pengine au natumaini ku…… Bali atatenda. Alitoa ahadi yake halisi.

**Jenga** – Hili neno ni jepesi. Lina tazama mbele. Linapaza sauti, “Kuza!, Endelea! Shika njia! Songa mbele!” Yesu angeweza kuunda kanisa upesi, vile alivyofanya alipoumba ulimwengu. Bali alisema atalijenga, ambayo ni njia inayochukua muda au inayoendelea. Baadaye katika sura hii tutatazama njia ambayo Roho Mtakatifu alimpa Mtume Paulo kwa kuanzisha makanisa mapya.

Hii njia ya kujenga ina kina - watu wakikua kuelekea ukomavu wa kiroho. Na pia ina upana – watu wengi kumwamini Kristo na kuja katika kanisa.

**Kanisa -** Lengo la Yesu lilikuwa kulijenga Kanisa Lake. Kanisa si jengo. Bali ni watu walioitwa na kuteuliwa na Mungu. Hakusema kuwa atalijenga dhehebu Lake, chuo, duka la vitabu, kituo cha redio au mashirika ya umisheni. Hayo yote ni mazuri, lakini yapasa kulitumikia kanisa la Yesu. Kanisa ni njia ya Mungu ya kuikamilisha ile Tume kuu.

**Langu** – Yesu hulimiliki kanisa.  Alilinunua kwa damu yake mwenyewe! Si kanisa la mchungaji  au kanisa la wazee wa kanisa au mashemanzi.  Kanisa ni la Yesu.

## 4. TAMATI KUU

**Soma Mathayo 24:14**
14 Tena habari njema ya Ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.

### 4.1 Yesu alisema mwisho utakuja lini?

Akiwa juu ya Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake walimwuliza wakati ambapo mwisho wa dunia utakapokuja.  Kwa sababu alikuwa na maono makubwa, jibu lake lilikuwa kubwa kuliko swali lao.

Yesu hakuwapa tarehe na wakati. Bali aliwapa kipimo.  Kwa ufupi, Aliwaambia wanafunzi Wake, "mradi tu injili ya Ufalme imeshahubiriwa katika ulimwengu wote, mwisho utakuja.  Kwa wakati huu, kazi yenu ni kunitii Mimi ili yaweze kutendeka."

Vile tulivyosema awali, njia ya Mungu ya kuitimiza Tume Kuu ni Kanisa – yaani Mwili wa Kristo, uliotawanyika kote kote ulimwenguni.  Kwa hivyo, njia ya Mungu ya kuhubiri injili kwa ulimwengu wote ni kuanzisha makanisa mapya mahali ambapo hakuna lolote. Wakati wewe na kanisa lako mnaanzisha makanisa mapya, ni hatua moja karibu zaidi, kwa kurudi kwa Yesu!

Hasa injii hii ni nini ambayo Yesu alizungumzia? Injili ya Ufalme ni kuwa Yesu aliteseka na kufa kulipia gharama ya dhambi zetu NA kuwa yu hai leo na hutawala Ufalme wa Mungu.

Baada ya kutoa ahadi hii, Yesu alijiruhusu asulubishwe! Yake haikuwa kushindwa vibaya… bali ilikuwa ushindi mkubwa zaidi katika historia!

Alikufa, lakini si mfu tena. Alifufuliwa kutoka kwa wafu kupitia nguvu zisizofungika za Roho Mtakatifu.  Baada ya kufufuka, alitupa sisi sote amri nyingine muhimu kupitia kwa wanafunzi wake wa kwanza.


©2005 e3 Partners Ministry

## 5. TUME KUU

**Soma Mathayo 28:18-20**
18 Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni
na duniani. 19 Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,
mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; 20 na kuwafundisha
kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote,
hata ukamilifu wa dahari."

### 5.1 Je, Yesu aliwaambia wanafunzi wake wafanye nini?

**Enendeni! Mkawafanye wanafunzi! Wabatizeni! Wafunzeni!**

Hizi ni amri zilizodhahiri na za waziwazi bali siyo mashauri au mapendekezo. Tena siyo mawazo makuu au maoni makuu. Hiki si kitu kingine ila Tume Kuu ya Mungu Mkuu.

Yesu aanza kwa kuifanya dhahiri kwamba Mungu Baba akimkabidhi mamlaka yote. Kote mbinguni na duniani juu ya vyote tuonavyo na visivyoweza kuonekana – isiyo na mpaka na visivyozuiliwa. Hii yadhihirisha kuwa tuangalie kwa makini ni nini kingine anachosema.

### 5.2 Je amri kuu ni gani katika aya ya 19 na 20?

Fungu hili liliandikwa kwanza katika Kiyunani. Katika lugha hiyo, maneno yana mikazo tofauti. Maneno mengine yana mikazo ya kawaida – kama aongeaye kwa mazungumzo ya kawaida. Maneno mengine yana mikazo zaidi - Ni kama mtu aongeaye kwa sauti! zaidi ili apate usikivu wa mtu.

Halafu maneno machache yana mkazo mkubwa. Ni kama mtu anayepaza sauti juu. "Fanyeni wanafunzi" ina mkazo wa "paza sauti kwa juu".

Halafu fanyeni wanafunzi ilikuwa Amri Kuu ya Yesu katika vifungu hivi. Yafaa tufanye vile alivyofanya – kwa kwenda, kwa kubatiza, na kwa kuwafundisha watu kutii vitu vyote alivyotufunza.

### 5.3 Ni ahadi gani Yesu alifanya katika Tume Kuu?

Aliahidi ya kwamba hatuhitaji kwenda pekee kufanya wanafunzi, kubatiza, kufundisha. Yesu hakutoa amri Zake, kutupongeza kwa kutupigapiga mgongoni na kututakia heri.

Alisema, "njooni! tuandamane pamoja. Hatua kwa hatua, upande kwa upande, mikono kwa mikono. Popote na siku zote."

Lakini msielewe vibaya, haugani na tume yetu. Tunaungana na yake!


©2005 e3 Partners Ministry

**Kwa kweli twatii Tume Kuu?**

Kanisa huongea mno kuhusu Tume Kuu. Lakini tunaitii kwa kweli? Tuchukue mtazamo wa karibu.

| | Mkakati wa Mwokozi (Mwili wenye Afya) | Badilisho la shetani (mwili unaougua) |
|---|---|---|
| NANI | **WANAJESHI**<br>Ajiri wote wapatikanao<br>1. Waumini wote wanakabiliana nayo kila wakati<br>2. Matendo 2:42:47 – miaka 200 ya kwanza, Ukirsto ulienea kama moto wa mwituni-kupitia wafuasi wa kawaida, si wanathiologia walio hitimu. | **WATAZAMAJI**<br>Wenye elimu ya kuongoza dini tu ndio wanaofuzu<br>1. Mgawanyiko kati ya wenye elimu ya kuongoza dini, na wasio na elimu hiyo.<br>2. "Wataalamu hufanya kazi ya Kiroho.<br>3. Wasio na elimu ya dini kusaidia wataalamu.<br>4. Washiriki wa kanisa ni watazamaji. |
| WAPI | **MATAIFA YOTE**<br>Panua maono<br>1. Mungu anataka sisi tuwazie makubwa iwezekanavyo!<br>2. Maono yako ni makubwa kiasi gani?<br>– Mataifa yote?<br>– Au nchi yako tu?<br>– Au jiji lako tu?<br>– Au ujirani tu? | **MIMI NA KANISA LANGU**<br>Kunyata maono (kuyafanya madogo)<br>1. Shetani atutaka tuwaze kwa udogo iwezekanavyo!<br>2. Maono yako ni madogo kiasi gani?<br>- Mimi, binafsi<br>- Jamii yangu na marafiki<br>- Mimi na kanisa langu |
| KITU GANI | **FANYENI WANAFUNZI**<br>1. Anza na uinjilisti<br>2. Endelea na uanafunzi<br>3. Kila mtu amfunze mwingine<br>4. Tume Kuu ni ya kila mtu | **CHOCHOTE LAKINI MSIFANYE WANAFUNZI**<br>1. Wanaweza kusema la na waniaibishe.<br>2. Kuna mashaka chungu nzima mimi sijahitimu.<br>3. Nimetosheka kama mwenye kuonja mahubiri.<br>4. Mimi ni mkristo wa mkahawa. Nachagua ninachohitaji na kuacha vingine. |
| VIPI | **ENENDENI NA MUWAAMBIE**<br>Fanyeni watu kuwa wanafunzi tunavyoendelea. | **NJOO USIKIE**<br>1. Shetani hugeuza "Enenda ukawaambie" kuwa " Njoo usikie"<br>2. Anatufanya kutilia mkazo mipangilio ya ndani ya kanisa badala ya watu walio nje ya kanisa.<br>3. Jinsi unavyoweza kukomesha ugonjwa unaoshika watu wengi kwa kuwatenga walioambukizwa, shetani hukomesha kuenea kwa Ukristo kwa kuzuilia waumini mahali fulani. |

Ombi letu kwenu na Kanisa lenu ni kwamba mngefanya wanafunzi ambao wana kishindo kwa mataifa yote, na kuwa kanisa lenu liwe **KITUO CHA KUFUNZA HABARI ZA TUME AU UMISHENI DUNIANI.**

## Hatua za Kwanza

## 6. AHADI KUU

**Soma Luka 24:46-53**
46 Akawaambia, "ndivyo ilivyoandikwa; kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; 47 na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu. 48 Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya. 49 Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu, lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu." 50 Akawaongoza mpaka Bethania, akainua mikono yake akawabariki. 51 Ikawa katika kuwabariki, alijitenga na; akachukuliwa juu mbinguni. 52 Wakamwabudu; kisha wakarudi Yerusalemu wenye furaha kuu. 53 Nao walikuwa daima ndani ya hekalu, wakimsifu Mungu.

**6.1 Wanafunzi waliona nini wakati ule wa mwisho Yesu akiwepo kimwili duniani?**

Yesu alipoinua juu mikono Yake na kuwabariki wanafunzi, waliona vidonda vya kutisha katika mikono Yake. Alivyobebwa juu mbinguni, waliangalia juu na kuona mashimo ya kuogofya katika miguu Yake, vidonda vya upendo na neema.

Twapaswa kila mara kukumbuka upendo Wake na zaidi ya hayo jinsi alijitolea kwetu. Lakini wanafunzi walikuwa wakumbuke kitu kingine pia ambacho kiliwajaza na furaha kuu, ya kufurika kwa sifa.

"Kumbuka kungojea mjini mpaka niwatumie nguvu, mwahitaji kutii amri nilizowapeni." Hicho ndicho walichohitaji kukumbuka.

Luka alianza hotuba yake ya kanisa la mwanzo katika kitabu cha MATENDO, katika njia ile ile aliyomalizia kitabu cha Luka nayo. Yesu alijua kanisa la mwanzo halikuwa na nguvu ya kutii Tume Kuu. Alijua walihitaji nguvu isiyo ya ulimwengu na mwongozo pamoja na maono na utiifu, kwa hiyo aliahidi kwamba Roho Mtakatifu angetumwa kukaa ndani yao na kuwapa nguvu hiyo.


©2005 e3 Partners Ministry

**Soma Matendo 1:8-11**
8 Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi
mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote,
Samaria, na hata mwisho wa nchi." 9 Akiisha kusema hayo, walipokuwa
wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao.
10 Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake,
tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe,
11 wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama
mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni,
atakuja jinsi hiyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni.

**6.2 Nguvu hii ilikuwa iwawezeshe kufanya nini? Wapi?**

Aya muhimu ya kitabu cha Matendo 1:18 Yesu alijua kuwa wanafunzi wa mwanzo walihitaji nguvu isiyo ya ulimwengu na mwongozo. Nguvu hii ilikuwa iwawezeshe kuwa mashahidi wake kwa ulimwengu wote.

Lazima tufanye hivyo hivyo. Lazima tumngojee Roho Mtakatifu, tupate nguvu inayotoka Kwake. Lazima tutafute kusikia kutoka Kwake. Kupata mwelekeo kutoka Kwake na kuungana naye katika kazi anayoifanya. Tukifanya kazi peke yetu, twaona tu matokeo ambayo twaweza kutimiza, kile ambacho hakitoshi kukamilisha Tume Kuu.

Baada ya Yesu kutoa ahadi hii na maagizo ya kile kitafanywa na nguvu hii, alirudi mbinguni.

Lakini tena Luka aliweza kuongezea kitu ambacho lazima kili wasisimua wanafiunzi "Yesu anarudi tena" ilitangazwa na kudi la malaika..

Hiyo yamaanisha kwamba ingawa wewe nami hatukuwapo pale kumtazama akiondoka, labda huenda tuwe hapa tumwone akirudi!

**Hatua za kwanza** **Mtakuwa mkifanya nini Yesu akirudi?**

Hatutaki tuwe tukitazama kitu – ambacho hatusitahili kutazama. Hatutaki tuwe tukisema au kufanya au kusoma kitu, ambacho hakistahili wakati atarudi. Hata hatutaki kuwa tu na shughuli akirudi. Twatumaini sote kuwa tukitii amri Zake, kwa hiyo tuweze kumsikia akisema maneno haya matamu: "pongezi mtumishi mwema na mwaminifu".

Sasa tuone jinsi wakristo walizitii amri za Yesu katika karne ya kwanza.


©2005 e3 Partners Ministry

## 7. VIELEKEZO VYA KARNE YA KWANZA

Mungu alijiletea utukufu mkuu mwingi katika karne ya kwanza. Kitabu cha Matendo kimejaa hadithi za kuonyesha jinsi Mungu alivyotenda kazi kupitia watu wake kwa ajili ya kuendeleza Ufalme Wake.

Mbona hatuoni utukufu Wake sasa katika karne ya ishirini na moja (21), jinsi watu wa karne ya kwanza walivyofanya katika kitabu cha Matendo? Je inawezekana kuwa hatutii amri Zake? Changamoto ya kanisa katika karne ya ishirini na moja ni kuweza kuwa zaidi kama kanisa la karne ya kwanza! Pengine hatuhitaji kitu kingine kipya…… bali tunahitaji kurejelea mambo ya kimsingi.

Katika kitabu cha Matendo, mwandishi Luka, alitupa ukumbusho jinsi Roho Mtakatifu alivyotenda kazi katika kanisa la mwanzo. Tunaweza kujifunza mengi kutoka kwa kanisa la mwanzo. Ni Roho Mtakatifu yule yule aishiye ndani yetu, na ambaye hututia nguvu ili tuwe mashahidi, zapata karne ishirini baadaye!

Tumeweza kutazama maandiko manne muhimu, yanayowakilisha maono ya Yesu Kristo, yaani, Tangazo Kuu, Tamati Kuu, Tume Kuu, na Ahadi Kuu.

Sasa tumefikia mahali muhimu katika hadithi! Hapa kuna swali zuri! "Baada ya kuyasikia maneno haya kutoka kwa Yesu, Je, ni vipi kanisa la mwanzo liliweza kutii maneno haya?" Au njia nyingine ya kuliuliza ni, "walifanya nini wakiwa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu ili kuweka kwa matendo, maono ya Yesu katika karne ya kwanza?"

Basi na tutazame aya nyingine katika kitabu cha Matendo zinazotuonyesha jinsi Mungu alivyojiletea Utukufu Mkuu katika karne ya kwanza.

**Soma Matendo 1:15**
15 Siku zile akasimama Petro kati ya hao ndugu (jumla ya majina ilipata mia na ishirini)

### 7.1 Je, Yesu alianza na wanafunzi wangapi?

Walikuwa watu mia na ishirini tu! Alikuwa na maono ya ajabu kiasi gani! Bali Yesu aliweza kuona zaidi ya kikundi kidogo cha wafuasi hadi ile siku ambapo "hii injili ya ufalme itahubiriwa duniani kote."

**Soma Matendo 2:47**
47… wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote (Na) Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.


©2005 e3 Partners Ministry

### 7.2 Ni nani alilifanya kanisa kukua? Ni nani aliongezeka kila siku?

Alikuwa Bwana ndiye "alilizidisha kanisa kila siku, wale waliokuwa wakiokolewa." Alifanya kazi kupitia watu wake, na Mungu, sio wanadamu, alipokea utukufu wote!

**Mungu kwanza aliongeza waumini wapya.**

Wewe ungesikiaje (vipi) kama angeongeza mwumini mmoja mpya zaidi kwa kusanyiko lenu kila siku kwa mwaka mmoja ujao? Haikosi watu saba kila wiki? Thelathini kila mwezi? Zaidi ya waumini wapya 360 (Mia tatu sitini) kila mwaka? Sisi sote tungekuwa tukishangilia kwa kusema, "Halleluya!" lakini hii ilikuwa tu hatua ya kwanza ya Mungu kijiletea Utukufu mwenyewe katika karne ya kwanza.

> **Soma Matendo 5:14**
> 14 Walioamini wakazidi kuongezeka kwa Bwana, wengi, wanaume na wanawake.

### 7.3 Je, ni jinsi gani Mungu alidhihirisha utukufu wake zaidi?

Sasa Luka anazungumzia kuhusu WAUMINI kuzidizishwa kwa WINGI - wakizidishwa na wakikuza Utukufu wa Mungu!

Sio tu mmoja au wawili kwa siku, bali wengi zaidi. Wangapi? Labda kwa madazeni, mamia au maelfu.

> **Soma Matendo 6:1**
> 1 Hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakiongezeka hesabu yao, palikuwa na manung'uniko ya wayahudi wa kiyunani juu ya Waebrania kwa sababu wajane wao walisahauliwa katika huduma ya kila siku.

### 7.4 Sasa ni nani alikuwa akiongezeka?

Hata Mungu alijiletea utukufu mwingi kwa kuongeza idadi ya WANAFUNZI.

Kwa bahati mbaya, leo kunao waumini ambao hawaendelei kukua kama wanafunzi. Wameweka imani yao katika Kristo, bali hawaendelei kujifunza, kukua, na kutii.

Wanafunzi ni wale wajifunzao kwa muda mrefu na ni wafuasi wa Kristo daima. Wanaishi na kuhudumu vile Mungu alivyokusudia. Kujitolea kwao kwa Kristo kwaendelea kuongezeka. Wao huandaa wanafunzi wengine, vile Yesu aliamuru.


©2005 e3 Partners Ministry

**Soma Matendo 6:7**
7 Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalemu; Jamii kubwa ya Makuhani wakaitii ile Imani.

### 7.5 Kuzidisha kulileta je Utukufu zaidi kwa Mungu?

Luka hakuwa akinena tena kuhusu ongezeko. Ukuzaji wa Ufalme ulianza kuzidisha mwendo mwepesi kwa sababu, "idadi ya wanafunzi ilikuwa IKIZIDISHWA".

Ukuzaji wa Ufalme ulizidisha mwendo kama vile wanafunzi walikuwa wakizidishwa. Kuzidisha kuna kishindo kingi zaidi kuliko ongezeko.

### 7.6 Ungechagua hiari gani?

Jaribu kuiwazia kama mtu anayetaka kukupa zawadi, na wapewa chaguo mbili. Hiari ya kwanza ni wewe upate mbegu za mpunga elfu tatu kila siku moja kwa mwezi mmoja. Hiari ya pili ni wewe upokee mbegu moja ya mpunga siku ya kwanza, mbili kwa siku ya pili, nne kwa siku ya tatu kwa njia hiyo – kuzidi mara mbili idadi kila siku kwa mwezi mmoja.

Kama ungechagua mbegu elfu tatu za mpunga kwa siku, ungepokea elfu tisaini na tatu mwisho wa mwezi. Hiyo ingekuwa baraka kubwa! Bali ungekuwa umekosa hata baraka kuu zaidi. Ungaliamua kuanza na mbegu moja na kuizidi mara mbili kila siku kwa siku thelathini na moja, ungepokea zaidi ya mbegu za mpunga bilioni mbili!

Nguvu ya kuzidisha ni kuu sana kuliko ongezeko. Kukiri kwa imani ni jambo la ajabu. Lakini uinjilisti ni huduma ya ongezeko. Uinjilisti huwa huduma tu ya kuzidisha waumini wapya wanapofunzwa.Wanavyokuwa wanafunzi ambao wafanya uinjilisti halafu kuwafunza wengine, ufalme wa Mungu hupanuka zaidi sana ifaavyo. Kwa hiyo tunatii amri ya Kristo,"Kufanya wanafunzi".

Kumbuka kile Mungu alifanya katika Matendo 2:41? Watu elfu tatu (3000) waliokoka siku Petero alihubiri. Hii ni baraka kuu.

Lakini Mungu alionyesha hata zaidi ya nguvu Zake alipoanza kuzidisha wanafunzi.

**Mungu alijitukuzaje katika karne ya kwanza**

| | |
|---|---|
| **Matendo 1:15** | Yote haya yalianza na watu mia moja na ishirini tu! |
| **Matendo 2:47** | WAUMINI wapya WALIONGEZEKA kila siku |
| **Matendo 5:14** | Laiki ya kuongezwa WAUMINI wapya |
| **Matendo 6:1** | WANAFUNZI wanaongezeka |
| **Matendo 6:7** | WANAFUNZI WANAZIDISHWA |
| **Matendo 9:31** | MAKANISA YANAZIDISHWA |
| **Matendo 19:10** | WOTE katika Asia walisikia neno la Bwana Yesu. |

## Hatua za Kwanza

 ©2005 e3 Partners Ministry

**Soma Matendo 9:31**
31 Basi kanisa likapata raha katika Uyahudi wote na Galilaya na Samaria, likajengwa, likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana, na faraja ya Roho Mtakatifu.

**7.7 Sasa ni nini kinazidishwa?**

Wanafunzi walipozidishwa, kitu kingine kilianza kuzidishwa! Sio tu waumini na wanafunzi, bali sasa makanisa yote yalikuwa ya kizidishwa!

Haleluya!

Mungu alikuwa amekwisha anzisha mwendo au mfumo wa kwanza wa kuanzisha makanisa! Je, mfumo wa kuanzisha makanisa ni nini? Ni ongezeko kubwa kwa haraka, la makanisa ya kiasili; makanisa yakianzisha mengine, miongoni mwa kikundi cha watu au sehemu ya idadi ya watu. (Kutoka kwa David Garrison katika kitabu chake cha '*Church Planting Movements'*).

Je twawezaje kushiriki katika mwendo au mfumo wa kuanzisha makanisa ambao ni Mwendo wa Roho Mtakatifu? Twatii na kutenda kile Mungu alituumba tufanye. Wanafunzi huongoza wengine kwa Kristo na kuwafunza, kuwa wanafunzi. Watenda kazi hufunza watenda kazi wapya. Viongozi huzidisha viongozi wapya. Wachungaji hushauri na kuzidisha wachungaji wapya. Ndipo Yesu, katika neema Yake atawatumia hawa wanafunzi, watenda kazi, viongozi na wachungaji kulijenga kanisa Lake anapoupanua Ufalme Wake.

## Mungu Alikuumba kama maembe



Maembe yalitoka huko Mashariki mwa India, Burma na Visiwa vya "Andaman" vinavyopakana na Ghuba la Bengal

Karibu Karne ya tano B.C. ( Kabla ya Kristo), watawa wa dini ya Budha wanaoaminiwa kulitanguliza embe huko Malaysia na Asia Mashariki. Wafanyi biashara wa Kiajemi walilipeleka embe huko Mashariki ya Kati na Afrika. Kutoka huko, Wareno walilileta hadi Brazil na Uhindi wa Magharibi ( West Indies). Wakulima wa miembe walifika katika Florida hapo miaka ya 1830 na huko Kalifonia katika miaka ya 1880.

Wingi wa Afrika na Latin Amerika sasa zimejawa na miembe. Je, ni jinsi gani miembe ilikuzwa huko? Kuzidisha! Kila mwembe kwa urahisi ulifanya kile Mungu aliuunda kufanya. Ulizaa mbegu ambazo zilikua, zikawa miti mipya; ambayo ilizaa mbegu zaidi, ambazo zilikua, zikawa miti zaidi ambayo ………………

## Hatua za Kwanza


©2005 e3 Partners Ministry

**Soma Matendo 19:9, 10**
[9] Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakiitukana ile Njia mbele ya mkutano, basi, akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano. [10] Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana.

**7.8 Je Tume Kuu imewahi kukamilishwa katika eneo lolote?**

Ndiyo! Katika karne ya kwanza, kama Paulo vile alikuwa akilenga katika kufanya wanafunzi. Matokeo yalikuwa kwamba wote katika eneo hilo la dunia walisikia neno la Bwana Yesu. Wasomi wengine waamini kwamba Luka aliwarejelea wale wote katika Asia ndogo, kati ya Bahari Nyeusi na bahari ya Kati, pamoja na Asia ya Uturuki!

Mungu alikwisha kamilisha Tume Kuu katika eneo hilo wakati huo. Hilo ndilo ombi letu kwa jiji lenu, nchi yenu na watu wenu, kwamba Mungu awashe mwendo au mfumo wa kuanzisha makanisa! Ndiyo maana tunaita taratibu hii " Hamasisheni kanisa lenu katika mashamba ya mavuno ya Mungu!"

Inahuzunishaje ya kuwa kanisa kwa muda mrefu limeimarika kwa waumini wachache wapya mara kwa mara au jamaa ambayo imehamisha uwanachama wake kutoka kwa kusanyiko la mtu mwingine. Undogo wa utukufu wa aina gani Mungu amepokea, na jinsi gani tumewafurahisha adui wa Mungu.

Je mnataka kuuona utukufu wa Mungu katika karne ya ishirini na moja kama katika karne ya kwanza?

Basi ni wakati wa kuamka kuondoa usingizi kwenye macho yetu, na tutubu kwa ajili ya uvivu wetu na ukosefu wa bidii ya moyo na kumtii Mungu. Wakati tunaanza **kutenda** kile ametuamuru tufanye kwa **Njia yake**, katika nguvu za Roho Mtakatifu, Mungu atatimiza kufanya sehemu yake. Na tutaona makanisa yanayofunza, ya afya na imara yakizuka, kokote duniani kama tunda mtini.

Maneno muhimu ni "tenda" na "Njia yake"

Halafu tena, Mungu atawasha mwendo au mfumo wa kuanzisha makanisa. Anatafuta wanaume na wanawake wenye himizo ya kujitupa kwenya moto ili aweze kupepea mwako wa moto wa kuanzisha makanisa mapya, kuliko vile tunafikiria.

Je habari hii yaelezea wewe?

Ni maelezo mazuri ya mtu aliyeitwa Paulo.

 ©2005 e3 Partners Ministry 

## 8. KIELELEZO KINGINE CHA KARNE YA KWANZA

Yesu alikuwa mtu wa maono. Aliona mbali kupita chochote kilicho kuwa hapo mbele yake. Macho Yake ya asili yalipoona ukoma, Roho Yake iliona usafi na mwili laini. Macho Yake ya asili yalipoona maiti, macho Yake ya Kiroho yaliona msichana mdogo anacheza huku akitembea akizunguka ndani ya chumba. Kwa sababu Alikuwa na maono aliyopewa na Baba Yake, Yesu, "ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba, na kuidharau aibu yake, naye akaketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu". (Waebrania 12:2)

Paulo alikuwa mtu mwingine wa maono

**Soma Matendo 14:21-28**
**21** Hata walipokwisha kuihubiri Injili katika mji ule, na kupata wanafunzi wengi,
wakarejea mpaka Listra na Ikonio na Antiokia. **22** Wakifanya imara roho za wanafunzi
na kuwaonya wakae katika ile imani, na ya kwamba imetupasa kuingia katika ufalme
wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi. **23** Na walipokwisha kuwachagulia wazee katika
kila kanisa, na kuomba pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono ya Bwana
waliyemwamini. **24** Wakapita kati ya Pisidia wakaingia Pamfilia **25**Na baada ya
kuhubiri lile neno katika Perge wakatelemka mpaka Atalia. **26** Na kutoka huko
wakaabiri kwenda Antiokia. Huko ndiko walikoombewa neema ya Mungu kwa ile
kazi waliyokwisha kuitimiza. **27** Hata walipofika wakalikutanisha kanisa wakawaeleza
mambo yote aliyoyafanya Mungu pamoja nao, na ya kwamba amewafungulia mataifa
mlango wa imani. **28** Wakaketi huko wakati usiokuwa mchache, pamoja na wanafunzi.

Hebu tutazame kielelezo cha Paulo cha huduma.



**1. KUOMBA:**
Paulo aliomba na kuwafunza wanafunzi wake kuomba. Na walipokuwa, wakiomba, Mungu aliwaelekeza katika maeneo mapya *(Matendo 14:23)*



**2. UINJILISTI:**
Paulo alielekeza mahubiri yake kwa Yesu, akimwambia kila mtu habari njema za Injili za Ufalme wa Mbinguni.
*(Matendo 14:21)*



**3. FANYENI WANAFUNZI:**
Paulo aliwafunza waumini wapya, akiwasaidia kuishi kama wafuasi wa Kristo, hata walipoteswa. *(Matendo 14:21-22)*



**4. KUSANYA PAMOJA:**
Paulo aliwakusanya waumini wapya katika makanisa mapya. Hakuwaacha peke yao, lakini mara kwa mara aliwaleta pamoja katika jamii, ili wasaidiane na watiane mwoyo na kuanzisha ushahidi unaodumu na uwepo wa Yesu Kristo katika jamii.
*(Matendo ya 14:23)*

## Hatua za Kwanza


©2005 e3 Partners Ministry



**5. KUZENI VIONGOZI:**
Paulo aliwateuwa na kuwafunza viongozi. Alijua asingeweza kufanya kazi peke yake, kwa hiyo alifanya kazi kwenye timu au na watu wengine, akianza na Barnaba. *(Matendo 14:23)*



**6. ZIDISHENI MAKANISA:**
Kanisa katika Antiokia lilianzisha makanisa mapya kupitia Paulo na timu yake ya huduma. Kanisa la Antiokia ni kielelezo kizuri cha kanisa linalozidisha. Hata liliwatuma viongozi wake wakuu kuanzisha makanisa mapya. *(Matendo ya Mitume 14:26-28)*

Hebu Mungu akutumie pamoja na kusanyiko lenu kwa uhodari leo, jinsi alivyotumia Paulo na timu yake katika karne ya kwanza. Kila mmoja katika nchi yenu asikie Injili ya ufalme wa Mungu na wawe na nafasi kumwamini kama Mwokozi wao wa kipekee. Hebu Mungu akutumie na kanisa lenu kama kituo cha kutoa mafunzo ya Tume Kuu duniani!

**Hatua za Kwanza**

**Je Bwana anakuita ufuate mfano wa Paulo na kuanzisha Kanisa jipía?** *Angalia swali la kwanza la mkakati wa utendaji kazi kwenye karatasi hapo mwisho wa kitabu hiki.*

Iwapo jibu lako ni ndiyo, "sehemu" iliyosalia ya kitabu hiki cha maelezo itakusaidia kutii amri za Yesu, na kufuata kielelezo cha Paulo, kwa kusimamisha kanisa jipya. Kila sura inalenga mojawapo ya sehemu za huduma ya Paulo: maombi, uinjilisti, ufundishaji wa wanafunzi, kukusanya waumini pamoja katika makanisa, kukuza viongozi wapya na kuanzisha makanisa mapya.

Kuna changamoto nyingi za "**Hatua za Kwanza**" katika kitabu hiki cha maelezo. Hatua hizo zitakufanya ukuze mpango mahususi wa kuanzisha kanisa jipya. Zimeorodheshwa pia katika mkakati wa utendaji kazi kwenye karatasi, hapo mwisho wa kitabu hiki. Andika chini majibu yako kuhusu changamoto za 'Hatua za kwanza kwenye mkakati wa utendaji kazi kwenye karatasi, vile timu yako ya kanisa inavyozizungumzia. Mtakapomaliza, mtakuwa na mpango wa kuweka katika matendo!

## HATUA ZINAZOFUATA

Soma kijitabu cha mwendo au mfumo wa kuanzisha kanisa uliochapishwa na Halmashauri ya tume ya kimataifa ya makubaliano ya Southern Baptist. Unaweza pia kuagiza nakala katika lugha yako kutoka mtandao wa *www.imb.org/resources* au watumie barua pepe kwa anwani hii: *resource.center@imb.org*.

**KWA NINI KUANZISHA KANISA JIPYA.**
Tazama Katika:
*http://www.dcpi.org/NewChurches/Starting/default.aspx*

**FUATA MFANO WA BIBLIA KATIKA HUDUMA.**
Tazama katika: *http://currah.info/www/paul-timothy/docs/bible_models_for_ministry.pdf*

**JIFUNZE ZAIDI KUHUSU UZIDISHAJI WA HIARI WA MAKANISA.**
Tazama katika: *http://currah.info/www/paul-timothy/docs/spontaneous_multiplication_of_churches.pdf*

**KWA KUSOMA ZAIDI.**
Kwa kusoma zaidi, juu ya maono ya kuanzisha makanisa yanayozalisha makanisa mengine, tazama masomo ya "omega" juu ya "maono" yanapatikana kwenye mtandao wa http://wwwalliancescp.org/resources/omegacourse.htm/:

**KITABU CHA MAELEZO CHA KWANZA:**
**Somo la kwanza** "Kufikiri kwa "Z"
**Somo la pili** "Tume kuu na uanzishaji wa kanisa"
**Somo la tatu** "Mzunguko wa uanzishaji wa kanisa"


**KITABU CHA MAELEZO CHA PILI.**
**Somo la tano** "Msingi wa kibiblia katika uanzishaji wa kanisa, ulio kamilika"

**KITABU CHA MAELEZO CHA TATU.**
**Somo la nane** "Maendeleo ya kwanza"
**Somo la Tisa** "Vitu vya asili vya mwendo au mfumo wa kuanzisha kanisa"

**KITABU CHA MAELEZO CHA NNE.**
**Somo la kumi na moja** "Dalili za mwendo" au "mfumo"

**KITABU CHA MAELEZO CHA TANO.**
**Somo la kumi na tatu** "Maono na kutazamia kwa darubini"

 ©2005 e3 Partners Ministry 





©2005 e3 Partners Ministry



**KUOMBA**

**KIDOKEZO CHA KUFUNDISHA**

Kuna ishara ya mkono ya kila mojawapo ya sehemu sita za huduma ya kuanzisha makanisa ya mtume Paulo. Ile sehemu ya “kuomba” imewekwa kwenye picha hapa juu. Wafunze wanafunzi wako ishara hizi za mkono. Zitawasaidia wanafunzi wako kukumbuka sehemu za huduma ya Paulo.


©2005 e3 Partners Ministry



# OMBENI KWA AJILI YA KUANZISHA MAKANISA

**MAWAZO MAKUU**
- Yesu alikuwa nje miongoni mwa watu alipowaamuru wanafunzi kuwaombea watendakazi
- Mnahitaji kutambua mahitaji na kuombea kihalisi shamba la mavuno ili uweze kulima na upenye kwenye ardhi yenye ugumu wa kiroho.
- Changamoto yako ya "Hatua za kwanza" ni kuwa na mkakati wa maombi ambao unawatoa watu wako nje miongoni mwa watu wanaotaka kuwafikia kwa ajili ya Kristo mnapoanzisha kanisa jipya.

## 1. FUMBO LA MAVUNO: OMBENI

Baada ya kuchunguza mashamba ya mavuno, mkulima huchagua mahali pa kuanzia. Kwa kawaida, udongo huwa mgumu sana, huwa na mawe mengi au umesongwa sana na magugu hata hauwezi kupokea mbegu. Unahitaji kutayarishwa kwanza.

> Mpanzi alitoka kwenda kupanda, mbegu zake. Alipokuwa akipanda mbegu, nyingine zilianguka karibu na njia ndege wakaja wakazila. Nyingine zikaanguka penye miamba pasipokuwa na udongo mwingi mara zikaota, kwa udongo kukosa kina, na jua lilipozuka ziliungua, na kwa kuwa hazina mizizi zikanyauka. Nyingine zilianguka penye miiba, ile miiba ikamea ikazisonga. Nyingine zikaanguka kwenye udongo mzuri, zikazaa moja mia, moja sitini, moja thelathini (Mathayo 13:3-8)

Katika fumbo la mpanzi, Yesu alieleza ya kuwa ustawi wa mavuno unaadhiriwa na aina ya udongo. Udongo ulioshikamana ni lazima ulegezwe, mawe na magugu lazima yaondolewe.

Vifaa vya mkulima ni jembe la kukokota, majembe na reki.
Kifaa cha kanisa ni mkakati, maombi yanayongozwa kwa Roho.

## 2. OMBENI KWA AJILI YA WATENDA KAZI WA MAVUNO

Katika injili ya Mathayo, Yesu alituamuru tufanye wanafunzi. Pia alituamuru kumuomba Baba awatumie wale wanafunzi kwenda katika shamba lake la mavuno.


©2005 e3 Partners Ministry

**SOMA MATHAYO 9:35-38**

35 Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. 36 Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji. 37 Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, "mavuno ni mengi lakini watendakazi ni wachache. 38 Basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake"

**2.1 Yesu alikuwa akifanya nini alipopeana amri hii?**

**Yesu aliendа.**
**Aliona.**
**Aliwatumikia.**
**Alikuwa na huruma.**

Yesu hakuwa akiketi ndani ya meli au upande wa mlima, akifunza kanuni. Hakuwa akitoa mafunzo darasani. Alikuwa akitembea miongoni mwa watu- akitafuta kujua, walikuwa akina nani,vile walivyo kuwa na kile walihitaji.

Alikoenda alitumikia mahitaji yao yalioonekana wazi. Alikuwa na huruma kuu kwao. Lakini aliona kuwa walikuwa wengi mno kwa mtu mmoja hata mwana wa Mungu, kwa hiyo aliwageukia wanafunzi wake na kuwapa agizo.

**2.2 Je Yesu Aliwapa wanafunzi wake agizo gani?**

Aliwaambia waombe, akawaambia ni nini haswa watakachoombea. Kumbuka ya kwamba kamwe Yesu hakutenda chochote kile hakuona Baba yake akitenda. Kwa hivyo alikuwa akiwaambia wanafunzi wake! "Baba yangu anataka nyinyi mmwulize watendakazi zaidi, ili aweze kuwatuma kutusaidia kukusanya hawa kondoo kwenye kundi na kuwapatia wachungaji."

Lengo la ombi hili ni uhamasishaji wa kanisa; Inasema, Amkeni, Kanisa! Enendeni nje mashambani na mwaanze kukusanya mavuno. Kila kitu kimeiva. "Sogeeni sasa, kabla hakijakauka na kuoza!"

Kile Yesu alisema basi kinatumika leo.

Maombi haya makuu ni msingi wa mkakati wa Mungu kufikia mataifa yote! Hebu bahatisha hili, sisi sio tu shujaa wa maombi tu. Sisi pia ni jibu kwa maombi yetu. Tunamlilia Mungu, "Tuma mtu." Katika kila kizazi Mungu anauliza, "Nitamtuma nani, na ni nani atatuendea?" Anataka tuitikie kama alivyofanya Isaya, akisema. "Mimi ndimi! Ni tume" (Isaya 6:8)

**2.3 Twawezaje kukuza huruma iliyo sawa na ambayo ilimtia Yesu motisha?**

Alienda, Aliwaona watu; na kwa wale ambao aliwaona, Aliwatumikia. Halafu, huruma ya baba ikainuka ndani yake. Sehemu yetu ni kwenda kuona na kusaidia,na kisha tumwamini Mungu atoe huruma.

## Hatua za Kwanza

## 3. WATENDA KAZI ZAIDI WAMO KATIKA MAVUNO

Katika kitabu cha Luka, Yesu aliwapa amri ile ile, kikundi kikubwa zaidi cha wanafunzi. Wakati huu, alikuwa akiwazungumzia wale sabini na wawili alipokuwa akiwatuma nje. Basi tutazame fungu hili na tuone jinsi amri yake ni tofauti wakati huu.

> **Soma Luka 10:1-3**
> 1 Basi, baada ya hayo Bwana aliweka na wengine sabini na wawili, akawatuma wawili wawili wamtangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe. 2 Akawaambia, mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake. 3 Enendeni, angalieni, nawatuma kama wana kondoo kati ya mbwa-mwitu.

**3.1 Ni wakati gani ambapo Yesu alitoa amri hii kwa wale sabini na wawili? Mbona hii ni ya maana?**

Hapa Yesu anawaambia wale sabini na wawili waenende nje wawili wawili wafanye uinjilisti. Baada ya kuwaambia waenende nje, anawaambia waombee, watenda kazi kwa ajili ya mavuno. Katika Mathayo, Yesu alitoa amri kuwaombea watenda kazi kabla ya kuwaambia wanafunzi waende nje. Halafu akawaambia wangekuwa majibu kwa maombi yao wenyewe kwa watenda kazi. Tofauti hii katika wakati huu ni muhimu.

Tunaamini kwamba Yesu alikuwa akiwaambia wale sabini na wawili ya kuwa waombe ili Mungu awape watenda kazi wapya kutoka kwa waumini wapya ambao wangewaleta kwa Kristo. Watenda kazi zaidi walikuwamo katika mavuno! Waumini wapya wanaofikiwa sasa wana uwezo wa kuwa watenda kazi wapya na viongozi wapya wa mavuno yajayo.

Twahitaji pia kuomba kuwa Mungu atatupa watenda kazi wapya wenye uwezo wa kuzalisha makanisa mapya, tunapofanya uinjilisti. Hii itatendeka tu tukiwafundisha waumini wapya!

## 4. MWOMBEENI MTU WA AMANI

Yesu alikuwa na maagizo zaidi kwa wale sabini na wawili alipowatuma nje.

> **Soma Luka 10:5-7**
> 5 "na nyumba yoyote mtakayoingia, semeni kwanza, Amani iwemo nyumbani humu. 6 na akiwamo mwana wa amani, amani yenu itamkalia,la hayumo amani yenu itarudi kwenu. 7 Basi kaeni katika nyumba hiyo hiyo, mkila na kunywa vya kwao, maana, mtenda kazi amestahili kupewa ujira wake; msihame-hame kutoka nyumba hii kwenda nyumba hii."

**4.1 Kwa nini kumtafuta mtu wa amani ni muhimu?**
Tunapojiunga na Mungu katika kile anachotenda, kutakuwa na mavuno tele. Njia moja ya kuona mahali ambapo Mungu anatenda kazi ni kumtafuta mtu wa amani. Mtu wa amani ni mlinda lango kwa jamii za pande zote.

## Hatua za Kwanza

 ©2005 e3 Partners Ministry 

### 4.2 Mtu wa amani ni nani?

**Wazi kwa injili.** Mtu wa amani aweza kuwa asiyeamini ambaye ametayarishwa na Roho Mtakatifu na yuko tayari kupokea Injili. Au mtu wa amani aweza kuwa bado ni muumini. Bali wao kwa kawaida huwa wazi kwa injili.

**Sifa:** Mtu wa amani anajulikana sana katika jamii yao. Iwe kwa uzuri au kwa ubaya. Wenye mifano ya kibiblia walikuwa na sifa nzuri, kama Kornelio. Wengine walijulikana vizuri kwa sifa zao mbaya, kama mwanamke. kwenye kisima. Walakini kila mmoja alipomkubali kristo, tabia zao zilibadilika kabisa. Mungu alipata utukufu kwa mabadiliko haya.

**Duara la ushawishi:** Mtu wa amani ni yule anayetaka kujulisha duara lake la ushawishi kwa Kristo. Wanawaambia wengine juu ya vitu vikuu Yesu amewatendea.

**Wa Msaada**: mtu wa amani yuko tayari kuwasaidia watenda kazi wa Kristo.

**Timu katika Slovenia ilikutana na mwanamke aliyeishi kijijini ambapo walikuwa wakianzisha kanisa jipya. Timu ilisafiri kwa lisaa moja kupitia njia hiyo ili wafike katika kijiji hicho. Huyu mwanamke mwenye neema aliwaalika kukaa kwake. Siku iliyofuata alimpokea Kristo. Alikuwa tabiri wa Kiisilamu ambaye alisoma majani ya chai na mashamba ya kahawa kutabiri wakati ujao. Kupitia duara lake la ushawishi, watu ishirini na mmoja walimpokea Kristo. Walianzisha kanisa la nyumbani hapo nyumbani mwake. Baada ya kusoma hadithi ya Lydia katika Biblia huyu mwanamke alibadilisha jina na kuitwa "Mama Lydia."**

**"Unapotenda kazi na Mungu kwa kwenda mahali pa kupokelewa kupitia watu wapokevu ambao ametayarisha, upo kwenye ajenda iliyokusudiwa na Mungu. Ni muhimu kukumbuka kuwa kwenye ajenda yake na sio yetu."**
*Carol Davis*

**"Mara nyingi uwanja wenye rotuba zaidi ambao wafaa kwa ajili ya kuanzisha kanisa hupatikana miongoni mwa watu wabaya."**
*George Patterson*

### 4.3 Ni watu gani wengine wa amani katika Biblia?

**Lidia** alikuwa Muyunani aliyeabudu Mungu. Alisikia zile kweli alizozinena Paulo, na Mungu akaufungua moyo wake. Hakuamini tu, lakini kama mwanamke wa ushawishi, aliweza kuwaleta watu wa nyumba yake yote kuamini. *(Matendo 16:14-15)*

**Kornelio** alianza kumtafuta Mungu kabla hajajua kwa kweli kuwa Mungu alikuwa nani. Mungu akampa maono kuwa alitakiwa kumwona Petro. Kornelio alikuwa mtu wa ushawishi mkuu na aliyezungumziwa vema miongoni mwa watu. Baada ya kuisikia Injili, Kornelio pamoja na nyumba yake waliamini. Kornelio alikuwa mtu wa amani aliyetayarishwa mbeleni na Mungu. *(Matendo 10:1-48)*

**Mwanamke kisimani.**
Alikuwa mtu wa amani aliyekuwa na sifa mbaya. Lakini wengi katika mji wake walimwamini Yesu kwa sababu ya ushuhuda wake. *(Yohana 4:4-41)*

**Hatua za Kwanza**

**Muulize Mungu akupe mtu wa amani kwa kusaidia kuanzisha kanisa lenu jipya.**
*Tazama swali la 4 (nne) la Mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

 ©2005 e3 Partners Ministry 

## 5. MFANO WA PAULO

Paulo alijua kuwa Yesu alisema kwamba Atalijenga na kuliongoza kanisa lake. Pia alijua kuwa Yesu alimwita Paulo awe moja wapo wa timu yake. Naye Paulo alitaka kuhakikisha kuwa alikuwa akitenda kile Yesu alitaka kitendwe wakati gani, mahali gani na jinsi gani. Kwa hivyo aliomba.

> **Soma Matendo 13:1-5**
> 1 Na huko Antiokia katika kanisa lililokuwapo palikuwa na manabii na waalimu, nao
> ni Barnaba, na Simioni aitwaye Nigeri, na Lukio Mkirene, na Manaeni aliyekuwa
> ndugu wa kunyonya wa mfalme Herode, na Sauli.
> 2 Basi hawa walipokuwa
> wakimfanyia Bwana ibaada na kufunga, Roho mtakatifu akasema, nitengeeni
> Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia.
> 3 Ndipo wakisha kufunga na kuomba,
> wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao.
> 4 Basi watu hao wakiisha
> kupelekwa na Roho mtakatifu wakatelemkia Seleukia, na kutoka huko wakasafiri
> baharini hata Kipro.
> 5 Na walipokuwa katika salami wakalihubiri neno la Mungu
> katika masinagogi ya Wayahudi, nao walikuwa naye Yohana kuwa mtumishi wao.

### 5.1 Je walikuwa wakifanya nini wakati Roho Mtakatifu alikatiza mkutano wao?

Kanisa na viongozi katika Antiokia walimtazamia Mungu. Walikuwa wanaomba na kufunga. Maombi yasiyokoma na kuabudu kila mara hutangulia mipango yenye nguvu.

Vivyo hivyo ilikuwa kweli katika Agano la kale. Yoshua aliabudu *(Yoshua 5:13-15).* Na baadaye Mungu akampa mpango ambao ulioshinda na kutawala Yeriko. *(Yoshua 6:2-21)*

Wanafunzi walimwabudu Yesu mlimani *(Mathayo 28:16-17)* Kisha Yesu akawapa mpango wake wa Tume Kuu, wa kuleta ufalme wa Mungu chini kutoka mbinguni hadi duniani *(Mathayo 28:18-20)*

### 5.2 Mungu alipatia kanisa la Antokia mpango gani?

Roho mtakatifu aliwapa maelezo wazi kuhusu **Nani, Nini na Wapi**. Kwanza, Aliwachagua wanaume wawili, Barnaba na Sauli. Pili, Aliwaambia walikuwa wakiitwa "kwa kazi ambayo nimewaitia," ambayo ilikuwa kuanziasha makanisa. Halafu, Aliwaelekeza kwenda Seleukia na Kipro.

**Hatua za Kwanza**

**Unawezaje kufuata mfano wa kanisa la kwanza? Unaanza kwa kujibu maswali machache:**

- **Kanisa lenu litaanza kuomba lini?**
  *Tazama swali la pili katika mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*
- **Je Mungu anataka uanzishe kanisa jipya wapi?**
  *Tazama swali la tatu katika mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*
- **Anamwita nani kuwa kwenye timu kusaidia kuanzisha kanisa jipya?**
  *Tazama swali la tano katika mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

**Hatua za Kwanza**

**Vizuizi gani vinahitaji kushushwa? Katika kanisa lenu? Katika eneo ambapo Mungu anakuita kuanzisha kanisa jipya?**
*Tazama swali la sita katika mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

- Hali ya kutojali kanisani
- Ngome ya dini
- Uzoevu wa kutumia dawa ya kulevya
- Dhambi za uzinifu
- Ufisadi/Ulafi
- Ufuasi wa Joseph Smith na kitabu Chake
- Uchawi
- Uisilamu
- Uoga
- Kulewa kupindukia
- Kutumia mwili vibaya
- Kusadiki kuwa hakuna roho, wala ulimwengu wa vitu visivyo onekana na akili zetu,ila huu tu.
- Ukosefu wa imani
- Mashahidi wa Yehova
- Madhehebu
- Vingine

**Hatua za Kwanza**

**Je, yafaa muanzishe mnara wa maombi kuandaa maombi kwa ajili ya anisa jipya?**
*Tazama swali la saba mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

### 5.3 Je mnara wa maombi ni nini?

Mnara wa maombi ni kundi la waumini wawili au zaidi ambao wanakusanyika na nia moja ya kwenda kuwahudumia na kuwaombea majirani zao.

> [14]Ninyi ni nuru ya ulimwegu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima………..
> [16]Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni. *(Mathayo 5:14,16)*

Maombi ni ufunguo wenye nguvu nyingi unao kuwezesha kuangaza nuru ya Mungu kutoka nyumba yako, au kanisa, ukiwaelekeza rafiki zako na majirani kwenye ukweli na makaazi mazuri yapatikanayo tu kwa Yesu.

### 5.4 Mnara wa kuanzisha makanisa uanzishwe wapi?

Ujirani unaolengwa kwa kanisa jipya, hasa wakati washiriki wa kanisa lililozaa jingine wanaishi hapo ni mahali pafaapo sana kuanzisha mnara wa maombi. Kwa namna nyingine, mwulize Roho mtakatifu akuongoze kwenye nyumba, shule afisi au mahali pengine pa kukusanyika ambapo amechagua.

### 5.5 Nani ahusishwe?

Washiriki wa kanisa, wale wanaoishi au wanatenda kazi katika mnara na waumini wengine wa eneo jirani ni bora. Mara tu Mungu anadhihirisha mtu wa amani katika eneo jirani, mhusishe mtu huyo katika mnara.

**Mkakati wa Mnara**

**Ombea:**
**Baraka tano** kwa **majirani watano** kwa **dakika tano,** kwa **siku tano,** kwa **majuma matano.**

## Hatua za Kwanza


©2005 e3 Partners Ministry

## 5.6 Mnara unatendaje kazi?

1. Kila mwombezi aanze kwa kutambua angalau majirani watano, watenda kazi,au marafiki katika eneo jirani ambao Bwana anamwongoza kuwaombea. Omba hasa Mungu apeane mtu wa amani katika eneo-jirani. Wenye kuomba waweze kuomba nyumba kwa nyumba kwa ajili ya hao ambao hawajakutana nao.

2. Jikabidhi kwa kuombea **BARAKA** tano kwa ajili ya watu watano kwa angalau dakika tano kwa siku, siku tano kwa juma, kwa majuma matano ( au mpaka harakati ya kuanzisha kanisa iaanze):

   **M**wili - Afya, Ulinzi, Chakula
   **U**tendaji kazi - mapato ya kazi, uhusiano mzuri wa kufanya kazi, uzalishaji
   **T**abia ya kihisia - Amani ya ndani, furaha, hekima, subirá
   **M**ambo ya uhusiano - uhusiano bora na jamaa na marafiki, kusuluhisha na maadui.
   **K**iroho - toba, wokovu, utiivu, shukrani, ukuaji wa kiroho na nafasi ya kushiriki injili na mtu huyo.

3. Tembea kupitia kwenye eneo jirani lako, ukiwaombea majirani zako ukitafuta nafasi kukutana nao. Waambie unawaombea, na uwaulize ikiwa kuna chochote dhahiri ambacho wangependa uombee. Ombea hali nyingine ambazo Bwana anakuonyesha unapotembea.

4. Weka kumbukumbu ya mahitaji yote ya maombi, ombea kila hitaji. Kumbuka kumshukuru Bwana kwa kila ombi lilojibiwa, na uandikishe majibu katika kumbukumbu lako.

5. Usishushwe moyo na hali inayoonekana kwamba hakuna matokeo. Shetani anapojaribu kukufanya ujihisi usiye na faida, na usiyefaa, mkumbushe kuwa Mungu anampenda kila mmoja katika eneo jirani na hujibu kila ombi kulingana na uzuri wake, hekima na rehema.

6. Tafuta nafasi kuonyesha upendo wa Kristo kwa kuthibitisha upendo na kuhusika kwako kwa majirani zako. Hudumia watu unaowaombea.

7. Unapokaribia kuanzisha uinjilisti na kufundisha wanafunzi, tafuta nafasi kuwaambia majirani zako kuhusu mambo yajao, watembelee na kuashirikisha injili. Ikiwezekana, waalike kwa mikutano itakayofanywa katika eneo jirani.

Mkakati huu umeazimwa kutoka jinsi ya kuanzisha na kuhifadhi mnara na huduma ya Tumaini. Kwa habari zaidi nenda kwa mtandao wa: www.hopeministries.org

> "Mungu alitupa mahali pa kuanzisha kanisa jipya. Tulianza kwa kupitia njia tofauti za mji tukiwaombea watu. Tulifanya hiyo kwa majuma kadha wa kadha. Tulipoanza uinjilisti, kila mmoja aliomba kupokea Kristo katika njia za mahali kanisa letu lilikuwa limeombea. Ni wachache waliomkubali Bwana katika njia za mji ambapo hatukuwa tumetembea na kuombea eneo hilo."
>
> **Mchungaji Santa Cruz, Bolivia**

## Hatua za Kwanza


©2005 e3 Partners Ministry

**HATUA ZA KWANZA**

**Hivi ni vifaa vya maombi ambavyo vinafuata -**

1. “Changamoto ya maombi ya nchi yako” unayoweza kunakili na kuwapa washiriki wa kanisa lako kuwatia changamoto kuomba maombi muhimu kimaandiko kwa ajili ya nchi yako.

2. “Baraka tano” kitabu kidogo unachoweza kunakili na kuwapa washiriki wa kanisa lako kuwasaidia kuanzisha minara ya maombi.

 ©2005 e3 Partners Ministry

**HATUA ZINAZOFUATA**

**Huduma za nguvu za maombi**, zina warsha na vifaa vyenye kichwa kuomba - ili kufanya tofauti. Kusudi la vifaa hivi ni kujifunza kutoka kwa Yesu, mwalimu mkuu kile kinachohitajika tukitaka maombi yetu yawe na tofauti – tofauti ya milele – katika maisha yetu na maisha ya wale tuwapendao. Unaweza kuwasilianan na huduma za nguvu za maombi kwenye anwani hii S.L.P. 801368. Dallas, Texas 75380-1368, mtandao huu: *www.learntopray.org*

**Mwongozo wa kuomba** na Dan Crawford
Unafafanua kuomba ukitembea kama muombezi katika mahali maalumu, penye habari, kwa kushirikiana, kinyume cha upinzani kwa kutukuzwa. Nakala hii ina maagizo na mswali tayari kurahisisha safari ya kuomba ukitembea kwa mkakati. Yaweza kutolewa chapa kwenye mtandao huu
*http://www.dawneurope.net/documents/prayerwalk%20walk%manual.pdf*

**Kuomba ukitembea kutunga ramani ya kiroho.**
Mwongozo huu unachukua kuomba ukitembea hatua moja mbele kwa kujishughulisha katika vita vya kiroho, kupitia kitu kingine ambacho kimekuja kujulikana kama "Kutunga ramani ya kiroho." Ina jumulisha hadithi za jinsi Mungu ametumia njia hii katika sehemu muhimu kote duaniani. Yaweza kutolewa chapa kwenye mtandao huu: *http://www.jwipn.com/pdf/cywtp_chapter28.pdf*

**Kutunga ramani (njia)** "Operation World" ni mtandao wa utafiti wa kimaombi ambayo utakupa habari muhimu kuhusu sehemu na aina za watu ambao miongoni mwao mngependa kuanzisha makanisa. Online at *http://www.gmi.org/ow/*

**Ramani ya ulimwengu wa kimataifa** inaweza kukusaidia kutambua maeneo muhimu ya kulenga katika nchi yako.Inapatikana katika mtandao:*http://www.gmi.org/*

**Kwa masomo zaidi**
Masomo ya "Omega" juu ya "maombi" yanapatikana katika mtandao wa
*http://www.alliancescp.org/resources/omegacourse.html*

**Kitabu cha maelezo cha kwanza**
  **Somo la tatu**."Jinsi ya kuendesha maombi"
**Kitabu cha maelezo cha tatu**
  **Somo la tano** " Maombi na kufunga"
**Kitabu cha maelezo cha tano**
  **Somo la kumi** "Kuendesha maombi kwa mwendo au mfumo wa kuanzisha Makanisa"



**KIFAA**

# CHANGAMOTO YA MAOMBI KWA AJILI YA NCHI YAKO

Ungependa kumwona Mungu akitenda kazi kwa njia ya miujiza katika nchi yako? Uko tayari kuikabili changamoto ya maombi ya muda mrefu kwa ajili ya nchi yako? Kwa hiyo mwulize Mungu atende katika nchi yako katika karne ya ishirini na moja kama alivyotenda katika karne ya kwanza!

Aya zifuatazo zinaeleza jinsi Mungu alivyotenda kazi katika karne ya kwanza. Omba ukitumia moja ya aya hizi kila siku kwa mwaka. Halafu mtazame Mungu akileta utukufu kwake mwenyewe anapobadilisha kabisa nchi yako.

**SIKU YA KWANZA**: Mwulize Mungu alete utukufu kwake mwenye kupitia jinsi Yesu atendavyo kazi kwenye kanisa katika nchi yako/yenu.
***Waefeso 3:21. . . "Naam atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele! Amina"***

**SIKU YA PILI**: Mwulize baba yetu wa mapenzi kuongeza waumini wapya kila siku kwa makanisa ya nchi yako.
***Matendo 2:47 ". . .wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote, Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."***

**SIKU YA TATU**: Mwulize muumba wetu, Mungu aongeze waumini wapya kwa wingi kila siku katika makanisa ya nchi yako.
***Matendo 5:14 "Walioamini wakazidi kuongezeka kwa Bwana, wengi, wanaume na wanawake"***

**SIKU YA NNE**: Ombeni kuwa Mungu awazidishe wanafunzi katika nchi yenu
***Matendo 6:1 "Hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakiongezeka hesabu yao……."***

**SIKU YA TANO**: Ombeni ili Mungu azidishe zaidi hesabu ya wanafunzi katika nchi yako.
***Matendo 6:7 "Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalem; jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile imani."***

**SIKU YA SITA**: Ombeni ili Mungu ajiletee utukufu kwa kuanzisha mwendo au mfumo wa kuanzisha makanisa mapya kila siku katika nchi yenu.
***Matendo 16:5 "Makanisa yakatiwa nguvu katika ile Imani, hesabu yao ikaongezeka kila siku."***

**SIKU YA SABA**: Msifuni Mungu kama Yule awezaye kujibu maombi haya, zaidi mno, na kwa utele sana, kuliko jinsi tuwezavyo kuuliza au kufikiri!
***Waefeso 3:20-21" Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu: Naam, atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele! Amina."***

## Hatua za Kwanza


©2005 e3 Partners Ministry

**JE NITAANZAJE?**

Anza kwa kusema ndiyo kwa Mungu. Omba ombi la (kujikabidhi), jinsi hii:

"Mungu mimi najua kuwa majirani zangu ni wa maana kwako, na kuwa umeniamuru kufanya 'maombi, sala, maombezi na kushukuru' kwa ajili yao. Kwa hivyo kwa kukutii wewe na kwa upendo kwa majirani zangu,ninajikabidhi kwa kuomba baraka zako kwa ajili yao kwa muda wa dakika tano kila siku,siku tano kila wiki, kwa muda wa wiki tano zijazo. Nitafanya haya kwa msaada wako, na kwa uwezo wangu wote. Katika Jina la Yesu, Amina."

Watu nitakaowaombea:
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
________________

Watu mtakaoomba nao ___________________________________

**Muda wangu wa kujikabidhi wa wiki tano**

Unaanza mnamo wiki ya_______________

Unaisha mnamo wiki ya________________

**Mawazo yangu nilipokuwa nikiomba**

_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________

**Kujitolea kwa Maombi**

Andika jina lako hapo chini ili kuweka sharti la kuombea majirani zako. Rudisha kijikaratasi hiki cha kujitolea kwa afisi ya kanisa lako.

Ndiyo! Mimi/sisi tutaomba kwa ajili ya baraka za Mungu kwa majirani zangu /zetu kwa dakika tano kwa siku, siku tano kwa wiki, kwa wiki tano.

Jina:_______________________________________________

KITABU CHA KUMBUKUMBU CHA KIBINAFSI CHA MAOMBI

| Maombi | Tarehe | Majibu | Tarehe |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**Vifaa vifuatavyo vinapatikana katika Nyumba za maombi kila (mahali)**

- Fanya nyumba yako iwe nyumba ya nguvu
- Nawezaje kuwaombea majirani zangu?
- Kijitabu cha kumbukumbu za maombi
- Nyumba za maombi: chokaa, vibao/mabango,au bendera
- Nyumba ya Nguvu – kijarida cha kila mwezi
- Kadi za salamu na maombi
- Viango vya mlangoni

Kwa kuagiza vifaa hivi na vinginevyo kutoka kwa ( yaani nyumba za maombi) kunao mshusho wa bei kwa maagizo ya kiasi kikubwa,tumia anwani hii:

S.LP 141312
Grand rapids, MI 49514
1-800-217-5200
*info@hopeminitries.org*
*www.hopeminitries.org*

Haki ya kunakili ©1999, HOPE.Mtu binafsi anaweza kuchapisha au kanisa la eneo kwa makusudi ya huduma.

# *BARAKA TANO*

*Njia rahisi,*
*na ya kirafiki ya kugusa*
*maisha ya jamii,*
*marafiki na majirani*
*kwa kuomba…*

***Baraka tano***

*kwa,*

***Majirani watano***

*kwa*

***Dakika Tano***

*kwa,*

***Siku Tano***

*kwa,*

***Wiki Tano***

**Maombi yanaweza kufanya nini katika jiji lako?**
Je, jiji lako laweza kufananaje ikiwa kila jirani na eneo-jirani wangeombewa kila siku? Lingekuwa jiji la kubadilishwa, watu wengi wakimjia Kristo! Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka.

> Haja ya moyo wake ni watu wote waweze kuokolewa na kwa sisi sote "kuishi kwa amani na utulivu katika utauwa wote na utakatifu" (1 Timotheo 2:1-2)

**Itagharimu nini?**
Mpango wa Mungu wa kubadilisha maisha ya watu binafsi na miji yote inahitaji maombi -waumini wakiwaombea majirani zao na hatimaye kupatikana karibu nao. Waweza kuleta tofauti kwa kuchagua Kirahisi tu, kuomba…….

- Baraka tano, kwa ajili ya
- Majirani watano, kwa
- Dakika tano kwa siku
- Siku tano kwa wiki , kwa
- Wiki tano

**Je, Jirani yangu ni nani?**
Jirani ni mtu aliyekaribu, jamaa yako, rafiki, mfanya kazi pamoja nawe, mwanafunzi mwenza au mchezaji mwenza. Katika Luka 10, Yesu anamweleza jirani kama mtu unayemkuta kwenye barabara ya maisha anayehitaji msaada wako.

**Je, ni "baraka' gani nitakayoiombea ?**
Waza kuhusu neno'BARIKI' ili uweze kukumbuka njia tano muhimu za kuwaombea majirani zako
Mwili – afya, ulinzi, nguvu
Kazi- kufanya kazi, mapato, usalama
Kihisia- furaha, amani, tumaini
Kihusiano – upendo, ndoa, jamii, marafiki,
Kiroho-Wokovu, Imani, neema.

**Mbona niwabariki majirani zangu?**
La kwanza, majirani zako ni wa muhimu kwa Mungu. Wao ni wana wa kiume na kike wa thamani kubwa, anaowapenda.

Mungu huhuzunika kuhuzu wale ambao wako kando naye, na anawataka warudi nyumbani. Maombi yatawasukuma kumwelekea Baba na mbingu zitafurahia wakati watakaporudi nyumbani.(Luka 15:7, 11-24)

La pili ni kuwa Mungu ameamuru kwamba"Maombi, sala, maombezi na shukrani" Zifanywe kwa ajili ya kila mtu."Kila mtu, yajumlisha pia majirani, ambao Mungu anawataka" waokolewe na kufikia kuujua ukweli."
(1 Timotheo 2:1,4) La tatu, unapowabariki wengine, nawe pia utabarikiwa.

**Je, niombe peke yangu au pamoja na wengine?**
Unaweza kuomba peke yako lakini mbona usiungane na muumini mmoja au zaidi- mke au mme wako, jamaa yako (waumini), wafanyi kazi wenza na muunde mnara wa Maombi.

**Mnara wa Maombi**
Ni kusanyiko la waumini wawili au zaidi wakifunganishwa pamoja kwa ajili ya kuomba, kushughulikia na kushiriki baraka za Kristo pamoja na wale, wanaoishi au kufanya kazi hapo karibu nao.

**Je, naweza kufanya zaidi ya kuomba?**
Ndiyo jiweke tayari kwa Mungu, na atakuongoza katika huduma za kushughulikia na kushirikiana. Utakuwa na matokeo mara tatu zaidi. Kwa kuomba utaachilia neema ya Mungu ndani ya maisha ya watu. Kwa kushughulikia, utayajenga madaraja ya upendo kwao. Kwa kushiriki injili, utawasaidia watu kumjua Yesu Kristo na waokolewe.

**Je, nawezaje kuunganika na majirani zangu?**
Njia rahisi sana ya kuunganika na majirani zako ni **kuwauliza tu juu ya haja za maombi**. Watu wengi siku hizi wanafurahishwa kwa kuulizwa. **Kutembea ukiombea** majirani wako au mahali pa kazi, itakusaidia kuombea "mahali penyewe na kwa undani". **Vibandiko vya milango** vitawajulisha majirani zako kuwa unawaombea.

**Maombi yangu kwa kweli yataleta tofauti.**
Ndiyo Tunapoomba Mungu hutenda! Biblia inasema," Maombi ya mwenye haki yana nguvu na yanafaa sana" (Yakobo 5:16).
Nguvu zote zilizopo katika maombi ni nguvu zake Mungu bali Mungu amechagua kuwa Nguvu zake zapitishwe kwa watu na mahali. Kupitia maombi yetu mambo yatatendeka unapoomba, ambayo hayangetendeka kama usingaliomba.

Kwa mfano, huko Michingan, wanachama wa 'Nyumba ya maombi" waliripoti kuwa katika maeneo ya ujirani waliyoombea, watu walikombolewa kutoka kwa madawa ya kulevya, watu wasio na kazi walipata kazi, baba mmoja aliacha kunywa pombe, watu wawili waliponywa kimiujiza, mtu mwingine akakombolewa kutokana na kupagawa na pepo mbaya, kikundi cha kusoma kujifunza Biblia kilianzishwa na watu watano walikuja kumjua Yesu Kristo.

Baada ya kanisa moja huko Mississippi kuanzisha **Nyumba za maombi**, mchungaji wao aliripoti, "Tulipoanzisha **nyumba zetu za maombi**, punde tu tuliona watu wakija kanisani ambao hawakuwa wakija kanisani kwa miaka mingi. Tunaona nyuso mpya karibu kila wiki. Kuhudhuriwa kwa shule ya Jumapili, kumeongezeka kwa asili mia arobaini (40) na kuhudhuriwa kwa ibaada kumeongezeka kwa asilimia thelathini (30), Uwepo wa Mungu wadhihirika kila wiki."

**Omba na moyo safi kila wakati**. Maombi ya **mwenye, haki** 'yana nguvu na yanafaa'


**Je, niombeje kila wakati?**

(Yakobo 5:16) Omba ukiwa na **huruma**. Uwe kama Kristo ambaye alisukumwa na huruma kuelekea kwenye mahitaji (Mathayo 9:36). Omba ukiwa na bidii. Mungu huwasikiliza wale wanaoomba kwa juhudi (Matendo 12:5; Yakobo 5:17).

## Hatua za Kwanza

 ©2005 E3 Partners Ministry 

 ©2005 E3 Partners Ministry 


KUOMBA
FANYENI UINJILISTI
FANYENI WANAFUNZI
KUSANYIKE NI PAMOJA
KUZENI VIONGOZI
ZIDISHENI



**FANYENI UINJILISTI**

# KUFANYA UINJILISTI

**MAWAZO MAKUU**

- Hadithi ya mwanamke kisimani inatuonyesha jinsi Yesu alimshuhudia akitumia mahitaji ya kimaumbile na kugeuza mazungumzo kwa mahitaji ya kiroho.
- Mwanamke kisimani ni mfano wa mtu mwenye amani ambaye aliwaelekeza watu wengi kwa Yesu.
- Ni muhimu sana kufahamu mambo ya maana ya msingi wa injili.
- Mnahitaji kifaa cha uinjilisti na mafunzo kusaidia kusanyiko lenu la waumini kujifunza jinsi ya kushiriki imani yao.

## 1. FUMBO LA MAVUNO: KUFANYA UINJILISTI

Baada ya mkulima kuvunjavunja udongo katika shamba lake, anatawanya mbegu kwa wingi. Mkulima anaelewa kwamba kuona mavuno maridhawa lazima apande mbegu nyingi, kwa vile si mbegu zote zitamea.

Mtume Paulo alifunza kanisa la Korintho kanuni hii aliposema, "kumbuka hii; Apandaye haba atavuna haba, apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu." *(Wakorintho wa pili 9:6)* Paulo alikuwa akiongea juu ya kupanda kifedha, bali kanuni hii ni sawa kwa uinjilisti-unapoweka mbegu nyingi ndani ya udongo mzuri,unaweza kutarajia, mavuno ya ajabu. Walakini, ukiweka mbegu chache katika udongo, unaweza kutarajia mavuno madogo.

Kutokana na haya tunajifunza ya kwamba kuimarisha kanisa, mnahitaji kupanda mbegu ya injili kwa wingi. Ukipanda mbegu zaidi yaani injili inapo wasilishwa zaidi- Ndipo mtawaona watu zaidi wakija kwa imani katika Kristo.

Bwana anatamani kwamba ujiunge naye katika kazi hii kwa kufanya uinjilisti katika jamii ambayo ina ushuhuda mdogo wa injili au haina kabisa. Kwa kutoka nje na kuingia ndani ya jamii na kushiriki injili kupitia uhusiano, mnapanda mbegu ya kiroho kwa matarajio ya mavuno makuu. Mkijaribu kuanzisha kanisa bila kupanda mbegu za injili kwa wingi, mtavuna kwa uchache.

 ©2005 E3 Partners Ministry 

## 2. MAJI YA UZIMA

Injili ya Yohana inatoa habari ya mwanamke aliyekutana na Yesu katika kisima cha Yakobo Siku moja.

**Soma Yohana 4:7-10**
7 Akaja mwanamke msamaria kuteka maji Yesu akamwambia," Waweza kunipa maji ninywe? 8 Kwa maana wanafunzi wake wamekwenda mjini kununua chakula. Basi yule mwanamke Msamaria akamwambia, imekuwaje wewe Myahudi kutaka maji kwangu, nami ni mwanamke Msamaria?" (Maana Wayahudi hawa changamani na wasamaria). 10 Yesu akamjibu, akamwambia, "kama ungalijua karama ya Mungu, naye ni nani akuambiaye nipe maji ninywe, ungalimwomba yeye,naye angalikupa maji yaliyo hai."

**2.1 Yesu alitaka nini kutoka kwake?**

Aliuliza kinywaji cha maji, haja nzuri ya siku zote kwa siku yenye joto na kavu. Walakini ilimshangaza huyu mwanamke.

**2.2. Mbona alishangazwa sana**?

Baada ya makabila ya Israeli kutengana katika siku za mfalme Daudi, Samaria ulikuwa mji mkuu wa Israeli, hali Yerusalemu ulikuwa mji mkuu wa Yudea. Kwa karne zote, falme hizi mbili ziliendelea kujitenga – kidesturi na kidini, hata kisiasa pia. Wayahudi walikuwa wakichukia Wasamaria, naye mwanamke alimtambua Yesu kama Myahudi.

Yesu walakini alikuja kuokoa kile kilichopotea, Myahudi na asiye Myahudi – na anatutaka tuvuke vizuizi vya kitamaduni.

**Soma Yohana 4:10 tena**
10 Yesu akajibu, akamwambia," kama ungalijua karama ya Mungu, naye ni nani akuambiaye, nipe maji ninywe, ungalimwomba yeye, naye angalikupa maji yaliyo hai".

**2.3 Yesu alimjibuje mwanamke?**

Yesu alikuwa na haja zaidi ya kuponya nafsi yake kuliko kukata kiu chake. Kwa hivyo alichukua nafasi ya kwanza kuelekeza tena mazungumzo yao, kutoka ya kawaida hadi ya kiroho. Mazungumzo yalivyoendelea, Roho mtakatifu alimfunulia Yesu historia ya mwanamke na Yesu alimfunulia mwanamke, yeye ni nani.

**Soma Yohana 4:28-30 na 39-41**
**28** Basi yule mwanamke akauacha mtungi wake, akaenda zake mjini, akawaambia
watu, **29**Njooni mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda: je, Haimkini
huyu kuwa ndiye Kristo? **30**Basi wakatoka mjini wakamwendea. **39**Na katika mji ule
wasamaria wengi walimwamini kwa sababu ya neno la yule mwanamke,
aliyeshuhudia kwamba. “Aliniambia mambo yote niliyoyatenda.” **40**Basi wale
wasamaria walipomwendea, walimsihi akae kwao, naye akakaa huko siku mbili.
**41** Watu wengi zaidi wakaamini, kwa sababu ya neno lake.

**2.4 Basi Mwanamke alimjibu Yesu namna gani ?**

Labda wanafunzi walimhofisha kwenda mbali waliporudi na chakula cha mchana,au pengine Baba alimfunulia ukweli, vile alivyofanyia Petero. Kwa hali yo yote alikimbia kwenda nyumbani, akamwambia kila mtu juu ya mtu wa kushangaza aliyekutana naye na kile alimwambia. Jiji liliitikia kwa kurudi naye kusikia na kujionea wenyewe.

Ufufuo ulitokea ghafla.Mwanamke huyu kisimani ni mfano wa “mtu wa amani” ambaye Yesu aliwambia wanafunzi wake baadaye kumhusu. Tazama aya ya maombi kwa habari zaidi kuhusu mtu wa amani.

## 3. INJILI NI NINI?

“Injili”- Ni neno la kidini linalomaanisha kwa wazi “habari njema” kueneza Injili, basi inamaanisha kirahisi tu, kuambia watu habari njema. Hili jambo rahisi laweza kubadili kabisa hali yako juu ya uinjilisti. Ndiyo, lakini injili hii halisi ni nini, hii habari njema ni nini? Pia, kuna jibu rahisi. Hapa kuna maneno ya mtume Paulo, akielezea injili ni nini”

**Soma Wakorintho wa kwanza 15:1-8**
**1**Basi ndugu zangu nawaarifu ile injili niliyowahubiria, ambayo ndiyo mlioipokea, na
katika hiyo mnasimama. **2**na kwa hiyo mnaokolewa ikiwa mnayashika sana maneno
niliyowahubiria isipokuwa mliamini bure.**3**kwa maana niliwatolea ninyi hapo mwanzo
yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi
zetu, kama yanenavyo maandiko.**4**na ya kuwa alizikwa nayakuwa alifufuka siku ya
tatu,kama yanenavyo maandiko.**5**na ya kuwa alimtokea Kefa, tena na wale
Thenashara.**6**baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja, katika hao wengi
wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala, **7**baadaye akamtokea Yakobo tena na
mitume wote **8**na mwisho wa watu wote,alinitokea mimi kama ni mtu aliyezaliwa si
kwa wakati wake.

Paulo anatumia maneno muhimu manne kueleza kwa ufupi Injili aliyoihubiri:

- Kristo **Alikufa** Kwa Dhambi Zetu
- **Alizikwa**
- **Alifufuliwa**
- **Alitokea**

Kwa ufupi, kifo cha kristo, kuzikwa na kufufuka ili kulipia dhambi zetu,ni INJILI au habari njema ya Yesu Kristo. Hicho ndicho kiini cha ujumbe wetu. Lakini Uinjilisti pia unahusisha kuwaalika watu kuweka imani yao na kuamini katika kugharamia kwa Kristo kwa ajili ya dhambi zao. Kwa hivyo mambo ya kimsingi ya kujifunza sana katika uinjilisti ni:

- Wewe ni mwenye dhambi,na dhambi hututenganisha na Mungu *(Warumi 3:23)*
- Kristo alifia dhambi zako na akafufuka *(Wakorintho wa kwanza 15:3-4)*
- Lazima umwamini Kristo tu kwa uzima wako wa milele *(Yohana 14:6 na Warumi 10:9)*

Kisanduku cha uinjilisti (EvangeCube®), kitabu kidogo cha kibinafsi cha kushuhudia, na vifaa hivi vya kutoa mafunzo vinakusudiwa kukusaidia uelezee sawasawa ujumbe huu wa wokovu. Pia vitakusaidia, katika hali mbili za changamoto zaidi ya uinjilisti wa kibinafsi:

- Kuanzisha mazungumzo juu ya toleo la Kristo la wokovu
- Kumkabili mtu na umuhimu wa kumkubali Kristo kibinafsi kama mwokozi

Mara nyingi tunawaambia watu juu ya Yesu, lakini hatujali kuwaalika kumwamini Yesu. Kama vile imesemwa”

**TAARIFA** bila **MWALIKO** ni **ELIMU** tu, na bali

**MWALIKO** bila **TAARIFA** ni **USHAWISHI** tu,

**TAARIFA** na **MWALIKO** ni **UINJILISTI**

Uinjilisti kibiblia unaeleza kifo, kuzikwa na ufufuo wa Kristo NA kuwaalika watu kumwamini Kristo kama njia yao tu ya uzima wa milele na Mungu

**Hatua za kwanza** Utatumia njia gani ya uinjilisti kushiriki injili?
*Tazama swali la nane la mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

**Hatua za kwanza** Utafunza kanisa lako lini kutumia njia hii ya uinjilisti?
*Tazama swali la tisa la mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

## Hatua za Kwanza

**HATUA ZA KWANZA**

**Hivi ni vifaa vya uinjilisti vinavyofuata**

1. Kujifunza kushiriki injili ukitumia kisanduku cha uinjilisti
2. Maagizo ya kisaduku cha uinjilisti
3. Kijitabu kidogo cha Uinjilisti
4. Jinsi ya kutumia kijitabu kidogo cha uinjilisti
5. Vitu vitano vya kukamilisha kwa kila matembezi
6. Jinsi ya kuandaa ushuhuda wako wa kibinafsi

**HATUA ZINAZOFUATA**

Ikiwa kanisa lako ( au eneo lako la kushirikiana, au dhehebu la kitaifa ) lingependa Mafunzo ya nyongeza ya Uinjilisti, Huduma ya E3 partners Ministry inaweza kusaidia. Huduma ya "E3 Partners Ministry" inatoa kwa sasa warsha yenye msingi wa kisanduku cha uinjilisti kwa muda wa masaa matatu juu ya uinjilisti wa mmoja kwa mmoja, kwa kutumia (kisanduku cha uinjilisti). Unaweza kuwasiliana na Huduma ya e3 Partners Ministry kwenye mtandao wa www.e3partners.org au kwa 214.440.1101 (U.S.A.)

Hapa kuna habari kuhusu mifumo tano ya kiasili ya kidini au kitamaduni.

**1. UISLAMU**

- *http://www.answering-islam.org/*
- mwongozo wa kikristo wa tume kwa uislamu: *http://www.christianmission.net/islam/*
- mtandao wa ukristo wa kiajemi : *http://www.farsinet.com*
- Njia nzuri: *http://www.the-good-way.com*
- Siku 30 za kulenga maombi kwa waislamu: *http://www.30-days.net/*
- *http://www.namb.net/atf/cf/%7BCDA250E8-8866-4236-9AOC-C646DE153446%7D/BB-Islam.pdf*

**2. DINI YA KIHINDI**

Dini ya Kihindi ni zaidi ya utamaduni ama ustaarabu kuliko dini. Ni ya utofauti kufikiriwa kuwa dini moja. Nifikira tu za kimagharibi za kawaida kwa wanaoamini kuwa ni dini moja.

- Dini ya Kihindi kutokana na mwelekeo wa kikristo : *http://www.gospelcom.net/oci/hinduism.htm*
- Utangulizi wa jumla wa dini ya kihindi na OMF kimataifa kwenye : *http://www.us.omf.org/content.asp? idx=9290*
- Mtandao wa jumla kuhusu India: *http://www.samachar.com* yenye habari ya usaidizi na rasilmali with helpful news and resources.
- *http://www.namb.net/root/resources/beliefbulletins/religious/hinduism.asp*

**3. UBUDHA (BUDDHISM)**

- Rasilmali ya kufahamu Ubudha na kuhudumia wafuasi wa Budha, na OMF kimataifa kwenye resources for understanding Budhism and ministering to Buddhists by OMF International at *http://www.onebillionwait.org/*
- *http://www.christianaswers.net/evangelism/beliefs/buddhism.html*
- *http://www.christianaswers.net/q-aiia/aiia-buddhism-harris.html*
- *http://www.christianaswers.net/q-aiia/letter-buddhisminterview.html*
- *http://christianliteratureandliving.com/march2004/sharingwithbuddihst2html*
- *http://www.johnankerberg.org/Articles/apologestics/AP 0102W3.htm*
- *http://www.namb.net/atf/cf1%7BCDA250E8-8866-4236-9AOC-C646DE153446%7D/BB_Buddhism.pdf*
- *http://answers.org/CultsAnd Religions/buddhisn.html*

**4. MAKABILA (TRIBALS)**

- Maelezo ya kuwa vitu vyote vina roho yanaweza kupatikana kwa ushirika wa umishonari wa ngambo kwenye mtandao: *http://www.us.omf.org/content.asp?idx=9286*

**5. DINI YA KIYAHUDI (JUDAISM)**

- *http://www.namb.net/atf/cf1%7BCDA250E8-8866-4236-9AOC-C646DE153446%7D/BB_Judaism.pdf*
- *http://www.ariel.org/sby.htm*

Kwa masomo zaidi tazama mfululisho wa masomo ya omega kwenye uinjilisti; yanapatikana kwenye mtandao wa:
*http://www.alliancescp.org/resources/omegacourse.html*

**Kitabu cha maelezo cha kwanza**

**Somo la kwanza** “Utangulizi wa Uinjilisti”

**Somo la pili/na tatu “**Kuendeleza ushuhuda wako wa kibnafsi”

**Kitabu cha maelezo cha pili**

**Somo la nne** “Uinjilisti na kuanzisha makanisa”

**Somo la tano** “Vizuizi vya uinjilisti unaofaa”


**Somo la sita/saba** “Njia ya kutubu au kubadilika”

**Kitabu cha maelezo cha tatu**

**Somo la nane** “Uinjilisti kwa njia ya uhusiano”

## Hatua za Kwanza

# KIFAA KUJIFUNZA KUSHIRIKI INJILI

| PICHA | NENO | SENTENSI | AYA |
|---|---|---|---|
|  | MUNGU | MUNGU anakupenda | **Yohana 3:16**<br>*Yohana wa kwanza 4:8* |
|  | WEWE | WEWE ni mwenye dhambi | **Warumi 3:23**<br>*Warumi 6:23* |
|  | YESU | YESU alifia dhambi zako | **Warumi 5:8**<br>*Yohana 3:16*<br>*Petero wa kwanza 2:24* |
|  | ALIZIKWA | YESU alizikwa | **Wakorintho wa kwanza 15:4** |
|  | ALIFUFULIWA | Mungu Alimfufua Yesu! | **Wakorintho wa Kwanza 15:4** |
|  | NJIA (MOJA) | Yesu ndiye NJIA ya kwenda kwa Mungu | **Yohana 14:6** |
|  | IMANI | Lazima uweke IMANI yako katika Yesu | **Waefeso 2:8-9**<br>*Yohana 1:12, 3:16-18*<br>*Wagalatia 2:16* |

**MAOMBI: Warumi 10:9**

## Hatua za Kwanza

*KISANDUKU CHA UINJILISTI*

**KUFUMBUA JIBU KWA FUMBO KUU LA MAISHA.**

Jinsi ya kumwongoza mtu kwa Yesu Kristo ukitumia kisanduku cha uinjilisti

1 **Onyesha " mtu aliye dhambini ametenganishwa na Mungu.**

**PICHA**

- Alama hii isiyokuwa na mkazo kwenye upande wa kulia ina wakilisha Mungu.
- Mungu ni mkamilifu na bila dhambi.
- Mungu anatupenda.
- Mungu hataki tuangamie bali tuwe na uzima wa milele.
- Lakini dhambi zetu lazima ziondolowe ili tuwe na uzima wa milele pamoja na Mungu.
- Kielelezo hiki upande wa kushoto kinawakilisha kila mtu kama mimi na wewe.
- Giza inawakilisha dhambi zetu. Dhambi ni chochote Mungu ametuambia tusitende.
- Biblia inasema"Wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu ( Warumi 3:23)
- Dhambi zetu zinatutenganisha na Mungu.

2 **Weka wazi kuelekea kwa "Kristo msalabani)**

**PICHA**

. Mungu alitupenda sana hata akamtuma mwana wake Yesu Kristo ulimwenguni kama mtu.

- Mungu alimfanya Yesu afe msalabani ili atulipie dhambi zetu kwa damu yake. Alichukua dhambi zetu mwilini mwake msalabani ili tuje kwa Mungu. 1 Petro 2:24, 3;18
- Biblia inasema ya kwamba "Mungu aliupenda Ulimwengu sana hata akamtoa mwanawe wa pekee Yesu, ili yeyote amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele"( Yohana 3:16)
- Biblia inasema Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu yakwamba wakati tungali wenye dhambi Kristo alitufia" ( Warumi 5:8)

3 **Weka wazi kuelekea kwa "kaburi"**

**PICHA**

- Watu walimzika Yesu kwenye kaburi.
- Walibingirisha jiwe kubwa mbele yake.
- Askari walilinda kaburi

4

**PICHA**

4. Mungu alimtuma malaika kubingirisha mbali hilo jiwe na kuwatisha askari.

- Mungu alimfufua Yesu kutoka wafu
- Punde baadaye, Mungu alimpeleka Yesu mbinguni tena.
- Yesu amelipa gharama ya dhambi zetu, na Yesu ameshinda kifo.

5 **Weka wazi kuelekea kwa "kuvuka daraja"**

- Yesu ndiye njia pekee ya kwenda kwa Mungu.
- Yesu alisema katika Biblia " mimi ndimi njia, na kweli , na uzima, mtu haji kwa baba (Mungu) ila kwa njia ya mimi" ( Yohana 14:6)
- Kupitia kwa Yesu, tunaweza kusamehewa dhambi zetu zote na kuwa na Mungu milele
- Lakini kujua tu kuhusu vitu hivi haitoshi! Lazima tuchague tuweke imani yetu katika Yesu, kumwamini atuokoe dhambini.
- Usipochukua hatua ya kumwamini Yesu, basi dhambi zako hazijaondolewa! (Waebrania 4:2)

6 **Weka wazi kuelekea "Mbinguni na kuzimu"** picha

- Biblia inasema yeyote amwaminiye Yesu anao uzima wa milele na hahukumiwi. Bali yeyote asiyemwamini Yesu amekwisha kuhukumiwa na ghadhabu ya Mungu inamkalia! " Yohana 3:16, 18,36)
- Ghadhabu ya dhambi ni kifo, bali uzima wa milele kupitia Yesu ni zawadi ya bure kutoka kwa Mungu.
- Ni chaguo gani utafanya?
- Mwamini Yesu Kristo akusamehe na uwe na uzima wa milele ( elekeza mbinguni).
- Ama umkatae Yesu Kristo na uteseke ghadhabu ya milele motoni (elekeza kuzimu).

**LIULIZE HILI SWALI**

Ungependa kumwamini Yesu sasa hivi na uokolewe?

Ikiwa NDIYO, endelea) Biblia yasema "**ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka**.Warumi 10:9

**Ninaweza kukuongoza kwa maombi kwa Mungu.Kumbuka, Siyo kusema maneno yatakayokuokoa, Mungu anatazama moyo wako, kwa imani ya kweli katika Yesu, uko tayari? (ikiwa ndiyo hebu tuombe:**

"Mungu, asante kwa kunipenda. Ni nakiri kuwa nimetenda dhambi kwako/ninaamini kuwa mwanao Yesu! Alikufa msalabani/kulipia dhambi zangu na kuwa ulimfufua Yesu kutoka kwa wafu. Sasa naweka imani yangu kwa Yesu tu kunisamehe na kuniokoa kutoka kwa dhambi zangu. Ninakiri kuwa Yesu ni Bwana! Asante kwa kipawa cha uzima wa milele. Ninaomba katika jina la Yesu, Amina"

## Hakikisho la Wokovu

**Onyesha Picha "mbinguni na kuzimu"**

picha

- Ikiwa ulichukua hatua hiyo ya kumwamini Yesu Kristo leo.
- Hapa kuna vile Biblia inasema juu yako"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika **watoto wa Mungu** ndio wale walioliamini jina lake" (Yohana 1:12)
- (Elekeza kwenye mikono) Yesu pia alisema" kondoo wangu waisikia sauti yangu, nami nawajua, nao wanifuata, nami nawapa uzima wa milele, wala hawatapotea kutoka katika mkono wangu" (Yohana 10: 27,28)

**HATUA YA HIARI**

**Onyesha Picha "kuvuka daraja"**

picha

- Yesu pia alisema, "yeyote alisikiae neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele,wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani" (Sogeza kidole chako juu kwenye daraja kwenye mwanga kuonyesha " kuvuka kutoka mauti kuingia uzima " Yohana 5:24.

## Hatua kwa wafuasi wa Kristo

Itumie kusaidia mwumini mpya kukua katika Kristo.

picha

**MPENDE Mungu na watu wote**

"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni , mpende jirani yako kama nafsi yako" (Mathayo 22:36-40)

picha

**SOMA Biblia (neno la Mungu ) kila siku**

Anza na injili ya Yohana soma sura moja kila siku. "kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu "(Petro wa kwanza 14:23)

"mtu akinipenda atalishika neno langu"Yesu akasema katika (Yohana 14:23)

picha

**MWOMBE Mungu daima**

Katika maombi waweza kumshukuru na kumwabudu Mungu, uliza usaidizi wake, tubu dhambi zako, na uwaombee wengine "msijisumbue kwa neno lolote, bali katika kila neno, kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru haja zenu na zijulikane na Mungu ( Wafilipi 4:6-7)

picha

**KUTANENI mara kwa mara na wakristo wengine.**

Mungu anaamuru kuwa wakristo wakutane mara kwa mara kwa kuabudu, maombi masomo ya Biblia na kusaidiana. "Wala tusiache kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi ya wengine, bali tuonyane" (Waebrania 10:25)

picha

**WAAMBIE wengine habari njema juu ya Yesu**

Mungu anataka tuwaambie watu wengine Jinsi ya kuwa na uzima wa milele kwa Mungu kwa kumwamini Yesu awaokoe kutoka kwa dhambi. Unaweza kutumia karatasi hii unapowazungumzia wengine kuhusu Yesu! "Akawaambia (Yesu) enendeni ulimwenguni wote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe" Mariko 16:15

picha

Tafadhali tupe ushuhuda wako:
testimony©evangecube.org
Kwa habari zaidi wasiliana na: EvangeCube International 317 Main Street rankling G 791-7886 888-354-941


## HATUA ZA WAFUASI WA KRISTO



**KUPENDA Mungu na watu wote.**

*"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni kwanza Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako." Mt. 22:36-40*

**1 Kor. 13, 1 Yn 4, Kol. 3:12-14, Efe. 4:15, 5:2**



**KUJIFUNZA Biblia(Neno la Mungu) kila siku.**

**Uanze na Injili ya Yohana: soma sura moja kila siku. *"Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu…" 1 Pet. 2:2***
*"Mtu akinipenda atalishika neno langu" Maneno ya Yesu Yn. 14:23*

**2 Tim. 3:16-17, Yak.. 1:21-22, Zaburi 119, Ebr. 4:12**



**KUSALI na kumwomba Mungu daima.**

**Katika kusali unaweza kushukuru na kumwabudu Mungu, ukimwomba msaada, na kuungama dhambi, pamoja na kuombea wengine.**
*"Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu." Flp. 4:6-7*

**Mt. 6:9-13, 1 The. 5:17, Kol. 4:2, Yak. 5:16, 1 Pet. 4:7**



**KUKUSANYIKA pamoja na Wakristo wengine.**

**Ni amri ya Mungu Wakristo wakusanyike mara kwa mara kwa ajili ya ibada, maombi, mafundisho ya Biblia, na kusaidiana.**
*"…tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine…" Ebr. 10:25*

**Mt. 18:20, Mdo. 2:42,46, 1 Kor. 14:26**





**KUWAAMBIA wengine habari njema ya Yesu.**

**Ni mapenzi ya Mungu tuwaambie wengine Jinsi ya Kupata Uzima wa Milele na Mungu kwa kumwamini Yesu na kuokolewa na dhambi zao. Wewe unaweza kutuk\mia karatasi hii wakati wa kuwaambia wengine habari njema!**
*"(Yesu) Akawaambia, 'Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.'" Marko 16:15*

**1 Pet. 3:15, Rum. 1:16, 10:14, Kol. 4:2-6**

# Je, Una Uhakika Kuwa Una Uzima wa Milele Pamoja na Mungu?

## Jinsi Ya Kuwa Na Uzima Wa Milele Pamoja Na Mungu

| | | |
|---|---|---|
|  | 1. Je, unaamini kuwa Mungu anakupenda na anataka uwe na uzima wa milele? | **Yn. 3:16** |
|  | 2. Je, unaamini kuwa umetenda dhambi?<br>3. Je, unaamini kuwa dhambi zako zimekutenganisha na Mungu?<br>4. Je, unaamini kuwa dhambi zako zitasababisha upate mateso ya milele?<br>5. Je, unaamini kuwa kutenda matendo mazuri kunaweza kukuokoa kutoka kwenye dhambi zako? | ***I Yn.1:8, 10***<br>**Rum. 3:23**<br>***Rum. 6:23***<br>**Efe. 2:8,9** |
| <br> | 6. Je, unaamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu?<br>7. Je, unaamini kuwa Yesu alikufa kwa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu ?<br>8. Je, unaamini kuwa Mungu alimfufua Yesu kutoka kwenye kifo siku ya tatu? | ***Yn. 20:31***<br>**Rum. 5:8**<br>**I Kor. 15:3-4** |
|  | 9. Je, unaamini kuwa Yesu ndiye njia pekee ya kwenda kwa Mungu//Mbinguni?<br>10. Yesu pekee ndiye anaweza kuokoa kutoka kwa dhambi zako na kukupa uzima wa milele. Lakini habari hizi njema kuh kuhusu Yesu hazikusaidii ila tu ukiweka imani yako kati kwa Yesu.<br>• **Je, unataka kuweka imani yako kwa Yesu ili akuokoe ?** | ***Yn. 14:6***<br>**Yn. 3:16,18** |
| | 11. (Kama jibu ni ndiyo) Biblia inasema katika Warumi 10:9: "Ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoa." Hiyo ni ahadi ya Mungu kwa ajili yako!<br>• **Je, unataka kumwambia Mungu kuwa sasa hivi unaweka imani yako kwa Yesu Kristo ili akuokoe na dhambi zako?** | |
|  | 12. **(Kama jibu ni ndiyo)** Nitakusaidia kuongea na Mungu kwa kukuongoza kwenye maombi. Si kwamba maneno yenyewe yanaweza kukuokoa, la, bali ni imani yako katika Yesu Kristo iwezayo kukuokoa. Wakati unapoomba, Mungu anaangalia nia ya moyoni mwako kama kweli unamwamini Yesu Kristo. Saa hii, naomba nikuongoze ili tumuombe Mungu. Ufuatane na mimi ukisema maneno yafuatayo:<br>**Mungu, / asante kwa kunipenda mimi. / Najua kwamba mimi nimefanya dhambi. / Nimekukosea./ Naamini kwamba Yesu Kristo mwana wako / alikufa msalabani / kwa ajili ya dhambi zangu / na ulimfufua / kutoka kwenye kifo / Saa hii ninaweka imani yangu / katika Yesu tu / anisamehe / na kuniokoa na dhambi zangu. / Ninakiri kwamba Yesu ni Bwana. / Asante kwa zawadi yako ya uzima wa milele. / Naomba katika jina la Yesu, / Amin** | |
| | 13. Kwa vile sasa umemwamini Yesu, je unaamini kuwa Mungu amekusamehe dhambi zako na amekupa uzima wa milele? | **Yn. 6:47**<br>**Rum. 10:9** |

# MHUTASARI

| | | | |
|---|---|---|---|
|  | UPENDO | Mungu **anakupenda** na anataka wewe uishi milele pamoja naye. | **Yohana 3:16** |
|  | **DHAMBI** | Lakini, **dhambi** zako zimekutenganisha wewe na Mungu na malipo ya dhambi ni mateso ya milele. | **Rum 3:23** |
|  | **MSALABA** | Ni Yesu Kristo pekee ndiye awezaye kukuokoa kutoka kwa dhambi zako.<br>1. Mwana wa Mungu Yesu alikufa **msalabani** kwa dhambi zetu.<br>2. Yesu alizikwa.<br>3. Mungu alimfufua Yesu kutoka kwenye kifo siku ya tatu. | **Rum 5:8** |
|  | **UAMUZI WA IMANI** | Ni lazima uweke imani yako kwa Yesu pekee ili uokolewe.<br>**Uamuzi** wako ni upi?<br>Mpokee Yesu kwa imani au mkatae. | **Efe. 2:8,9**<br>**Yohana 3:18** |

# Mistari Mingine Ya Biblia Kwa Maswali

1. **1 Yn. 4:8-10, 16 2 Petro 3:9, 1 Tim. 2:3-4, Rum. 6:23, Efe. 2:4-9**
2. **Gal. 3:22, Rum. 3:10, 23, Isaya 53:6**
3. **Isaya 59:2, Ebr. 7:22, 26, 1 Yn. 1:5-6, 1 Yn. 3:4-8, Mt. 5:48**
4. **Yn. 3:36, 2 The. 1:8-9, Ufu. 20:14-15, 21:8, Yak. 2:10, Ebr. 9:27**
5. **Tit. 3:5, Gal. 2:16, 2:21, 3:10-11, Rum. 3:20, 3:28, 4:5, 2 Tim. 1:9, Mt. 5:20, Flp. 3:9, Ebr. 10:4, Yak. 2:10**
6. **Mk. 1:1, Mt. 16:15-17, Kol. 2:9, Yn. 1:1,14, Yn. 17:1-3, Flp. 2:5-8**
7. **1 Pet. 2:24, 3:18, Kol. 1:20, 2 Kor. 5:21, Ebr. 10:10, Efe. 1:7, Isaya 53:5-6, Flp. 2:5-8**
8. **Gal. 1:1, 1 The. 1:10, Mt. 28:5-6, Rum. 10:9, 2 Tim. 2:8**
9. **Mdo. 4:10-12, 1 Tim. 2:5-6, Yn. 10:7-9, Gal. 1:8, Ebr. 10:4, 19**
10. **Ebr. 4:2, Mdo. 16:31, Rum. 3:22, 28, Gal. 2:16, Yn. 3:36, Flp. 3:9**
11. **Rum. 10:13, Yn. 1:12, Mt. 10:32, Flp. 2:11, 1 Yn. 4:15**
12. **Rum. 10:13, Yn. 1:12, Mt. 10:32, 1 Sam. 16:7, Mt. 12:36-37**
13. **Gal. 3:26, Yn. 1:12, 5:24, 10:27-29, 11:25,26 1 Yn. 5:11-13, 4:15, 5:1**

**Ili kujifunza zaidi:**

# JINSI YA KUTUMIA KIFAA (KIJITABU CHA e3 PARTNERS)

KIFAA

1. **Uliza maswali kwenye jalada la kijitabu "una uhakika una maisha ya milele na Mungu?**
   - Msikilizaji akijibu "la" kisha sema tukuonyeshe kutoka kwa Biblia jinsi unavyoweza kuwa na maisha ya milele na Mungu?
   - Msikilizaji akijibu "ndiyo" basi sema" una amini nini ili upate maisha ya milele?"
     - Kama jibu si Yesu Kristo, basi sema" Biblia inasema kuna njia moja tu ya kuwa na maisha ya milele. Tafadhali tunaweza kushiriki hiyo njia moja nawe?
     - Kama jibu ni 'Yesu' basi mwulize msikilizaji lini na jinsi gani alivyomwamini Kristo?

2. **Endelea na kijitabu, kutoka swali moja hadi lingine**.
   - Kama una kisanduku cha uinjilisti, eleza kila swali na picha kwenye kisanduku cha uinjilisti

3. **Siku zote mwonyeshe mtu maandiko makuu kwenye aya zilizo andikwa kwa herufi nzito zilizopigwa mstari.**
   - Tunataka watu wajue kwamba hili ni neno la **Mungu**, si tu kwa kuwasilisha kibinadamu. "Basi imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la kristo" Warumi 10:17
   - Hata ikiwa msikilizaji akijibu kisahihi bado anahitajika kuona maandiko ya uimarishaji wa alama hizi muhimu. Kusema kweli anaweza kuwa haelewi lakini, aweza kuwa na ubashiriaji mzuri."
   - Msifu kwa kusema "hiyo ni sawa! kwa sababu Biblia inasema………" halafu mwonyeshe aya katika Biblia.

   **Namna ya kuonyesha mtu Aya**
     - Shika Biblia vile msikilizaji anapoweza kuona aya,jinsi vile watu wawili wanavyoshiriki kitabu cha nyimbo.
     - Onyesha aya. Ni vizuri Kusisitiza aya katika Biblia yako. Waweza kutaka kuweka alama kurasa hizo katika Biblia yako kwa kuzipata haraka.
     - Usimlazimishe msikilizaji kusoma – aweza kuwa bila elimu. Akianza kusoma kwa sauti ya ukakamavu vizuri- kwa hiyo mpe nafasi. Lakini akikisia au kusoma kwa ukimya basi soma aya kwa sauti, ukilifuata kwa kidole, mkiiona pamoja.

4. **Wakati wowote mtu akipeana jibu lisilo sawa, sisi huhitaji, kumwonyesha aya**
   - Usiseme "umefanya makosa" tutaiacha Biblia iseme.
   - Kwa upendo' sema, hebu nikuonyeshe vile Biblia inasema juu ya hiyo, halafu onyesha Aya

5. **Sehemu za Muhtasari na Aya za ziada ni za usaidizi wako inavyohitajika**
   - Muhtsasari:
     - Msikilizaji akiwa na haraka, fanya tu alama za muhtasari na shiriki aya moja kwa kila moja.
     - Halafu nenda moja kwa moja sehemu # 10 ya kijitabu (sentensi na swali)
   - Aya za ziada:
     - Hizi zimehesabiwa zikiambatana na maswali 13 ya Kijitabu
     - Ni vizuri kutumia baadhi ya aya hizi kwenye vitu muhimu hasa swali #5
     - Kama msikilizaji ana shida ya kuelewa, au kutoelewa, tumia aya hizi kwa usaidizi zaidi.
     - Tumia tu aya nyingi unavyofikiria unazihitaji, si lazima uzitumie zote

6. **Kusema maombi (sehemu ya #12 ya kijitabu)**
   - Kwanza soma maombi kikamilifu ili mtu aelewe maneno ya maombi
   - Kisha mwulize mtu kama maneno ya maombi yangu yanasema vile wanasikia moyoni mwao
   - Wakisema "ndiyo" waulize warudie maombi baada yako!
   - Komea kila alama ya mstari wa mkazo na wakubalie warudie msemo huo

7. **Uhakika wa wokovu (swali la #13 baada ya maombi)**
   - Kama mtu hana hakika, kwamba ameokoka baada ya kuamini Yesu, tumia sehemu ya muhtasari kurudia injili na utumie aya za ziada kwa swali la #3 la kijitabu.

## KUMALIZIA ZIARA

**Mtu akifanya ungamo la imani**:

1. Anzisha ziara ya kufuatilia mara moja!
2. Chukua jina la mtu na habari ya taarifa ya mawasiliano, (anwani, nambari ya simu na kadhalika ) kwa kufuatilia
3. Mwachie kijitabu kidogo. Mtie moyo kurejelea maswali na hasa injili "muhtasari'' na pia alama za ufuasi zilizo nyuma. Waweza kurejelea haya mara moja ikiwa mtu ni msikivu.
4. Mwalike mtu kwa tamasha au mkutano wa jioni. Andika maelekeo, kama vile mahali maalum, wakati, usiku, nambari ya simu ya kiongozi na kadhalika kwenye kijitabu.

**Kama mtu hana wakati wa kusikiliza, au hafanyi ungamo la Imani**:

1. Mwachie kijitabu kwa njia ya urafiki. Mwonyoshe unampenda.
2. Mwalike mtu kwa mkutano wa jioni (uwe na maelekeo ya yaliyo andikwa upande wa kijitabu)

## Mwongozo

**Nia ya ziara iwe upendo (2 Wakorintho 5:14)** Upo hapo kumshughulikia mtu, kwa sababu Mungu anawajali kwa undani.Unataka wajue kuwa Mungu anawapenda na anatamani kuwa naye milele.Waambie haya na uangazie kutoka kwa nafasi yako. Ndiyo utakuwa wa kuaminika kuhusu dhambi na kuzimu, lakini siyo kwa hali ya kuhukumu. Ongea **ukweli** katika **upendo** (Waefeso 4:15) tabasamu na mwenye urafiki.

**Kijitabu hakikusudiwi kuwa cha ukaguzi wa Ndiyo/La** Huhitajiki kuandika chini majibu yao.Tumia kijitabu kama kifaa kuwa na mazungumzo yaliyo ya kawaida siyo kama mwandiko unaosomwa na mashine iliyo fanywa kama mtu (Roboti)

**Usiwahi Kubishana!**
Iwapo Utakutana na watu wabishi au wapinzani, toa majibu vile Bwana atakavyokuongoza. Acha Biblia inene kwa kusema, "Hebu nikuonyeshe kile Biblia inasema juu ya hiyo" Ikiwa pingamizi linaendelea washukuru wasikilizaji kwa upole kwa kukupatia muda wao na kuwaalika kwa mkutano wa jioni. Halafu endelea mbele.

**Usaidizi kwa kijitabu sehemu ya #2:**
Kama msikilizaji anasema hajawahi tenda dhambi, Usiende kwa aya mara moja. Kwanza **eleza dhambi ni nini?** "Dhambi ni chochote ambacho Mungu ametuuliza tusitende kama vile kuwa na wivu, kulaani, kutotii wazazi wetu na kudanganya.Je umewahi tenda chochote cha hivi vitu?" Ikiwa msikilizaji bado anasema hajawahi tenda dhambi basi nenda kwenye aya (Yohana wa kwanza 1:8-10).

**Usaidizi kwa kijitabu sehemu ya #10:**
Kama msikilizaji hataki kuweka imani yake katika Kristo:
-Kwanza, angalia kuona ikiwa **alielewa** injili kwa kutumia sehemu ya muhtasari
Mifano: UPENDO: Je unaelewa kuwa Mungu anakupenda?
DHAMBI: Je unaelewa kuwa dhambi yako imekutenganisha na Mungu?
- Pili – kama bado anasema 'La' kwa Kristo, uliza kile kinamzuia kumwamini Yesu.

**Usaidizi kwa kijitabu sehemu ya #11 & 12**
-Kama msikilizaji anaaibika kuomba mbele ya wengine, pendekeza kuhamia mahali faraghani.
-Kama msikilizaji angali anaaibika kuomba muulize kufumba macho yake na amwombe Mungu kwa kimya akirudia mafungu ya maneno uliyoomba kwa sauti.

**Usaidizi kwa kijitabu sehemu ya #13 (Hakikisho na ufafanuzi wa Imani)**
- Kila mara onyesha aya moja au zote.Ni vizuri kumfunza mtu huyo huyo hizo.

Yohana 6:47 – Yesu akawaambia, yeyote - - - afanya nini? - - - - -afanya matendo mema? Amwomba kwa Maria ?n.k. La! Alisema kuwa "Yeyote ANIAMINIYE" Yuna uzima wa milele Je, Yesu alisema UNAWEZA kupata uzima wa milele? LA Anasema UNAO sasa hivi!

Warumi 10:9- Je ulimkiri Kristo kama Bwana? (msikilizaji alisema fungu hili katika Maombi). Je unaamini kuwa Mungu alimfufua kutoka kwa wafu? (alisema 'ndiyo' katika kijitabu sehemu ya # 8). Biblia INAAHIDI ya kwamba yeyote atendaye vitu hivi Kwa kweli ataokolewa!

# VITU VITANO (5) VYA KUTIMIZA KWA KILA ZIARA

**KIFAA**

**1. UTANGULIZI**

Changua mtu mwingine kama mnenaji mkuu. Mnenaji mkuu atambulishe kila mtu kwa mfano, “Jambo, huyu ni rafiki yangu ‘John Doe’.Tunatembelea manyumbani mwenu leo katika jamii.Ungeturuhusu kwa muda wa dakika chache ili ‘John’ ashiriki hadithi maalum nawe? Ni hadithi ya kile Yesu Kristo ametenda maishani mwake.”

Ni muhimu kurejelea tena utambulizi huu na watenda kazi Wenzio kabla ya kuanza ziara yenu.Wakati wa kujitambulisha, hifadhi mawasiliano ya macho, tabasamu na tafuta kusalimiana kwa mikono kama salamu za kirafiki.

**2. USHUHUDA**

Shiriki ushuhuda wako wa jinsi ulivyopata kuwa mkristo. Ikiwa unafanya kazi na mtu ambaye anaongea lugha nyingine, endelea na haya kwa wakati, kupitia kwa ushuhuda ukibadilisha zamu kati ya kiingereza na lugha ya mahali palepale.Kumbuka maandiko yanasema kuwa neno la ushuhuda wako ni silaha ya kiroho na inaweza kutumiwa kwa nguvu na Roho mtakatifu.Mwishoni, mwulize mtu unayemtembelea ikiwa waweza kuwauliza maswali kadha wa kadha yanayohusu uhusiano wao na Mungu pamoja na Yesu Kristo.

**3. KIJITABU CHA SANDUKU LA UINJILISTI (EVANGECUBE®)**

Tumia sanduku la uinjilisti na kijitabu kushiriki Injili, ambayo ni nguvu zaMungu kwa wokovu! Shiriki na uonyeshe haya kutoka kwa Biblia kwa njia ifaavyo. Mwombee mtu unayemshuhudia unaposhiriki naye, Habari Njema.

**4. MWALIKO KWA MKUTANO WA JIONI**

Mpatie mtu unayeongea naye habari juu ya mahali maalum pa mkutano wa jioni. Watie moyo kwa ukunjufu waje na jamaa na marafiki zao na pia waulize wawe wageni wako maalum kwenye mkutano.

**5. HABARI YA KUFUATILIA**

Andika chini jina la mtu, anwani na nambari ya simu.Habari hii ni ya maana sana kwa kuhifadhi mavuno.Uwe na hakika ya kukusanya habari kamili.

 ©2005 e3 Partners Ministry 

**KIFAA**

# TAYARISHA USHUHUDA WAKO

Utahitaji kutayarisha ushuhuda wako na uwe tayari kushiriki na watu unapowaambia kuhusu Yesu. Hapa kuna mawazo kadhaa:

**Kabla ya kumfuata Yesu**: Gusia tu maisha yako ya dhambi juu juu. Hutaki msikilizaji ashinde akiwazia dhambi zako. Kueleza hisia ni ya msaada k.m. uchungu, upweke, utupu, kutokuwa na uhakika kuhusu milele, n.k.),lakini epukana na maelezo ya dhambi yasio na maana ukisema, " Nilikuwa (mwizi, n.k. )", Basi, msikilizaji anaweza kudhania," mimi si mbaya sana- simhitaji Kristo vile anavyomhitaji" mueleze juu ya dhambi," basi msikilizaji anaweza kutambua kwa kufikiria, " nadhania alikuwa mlevi kama mimi." Na mwishowe, usichukue dakika tano kuzungumzia dhambi, ukilinganisha na sekunde thelathini tu, kuhusu wokovu na maisha yako mapya!

**(Jinsi nilivyofanyika Mkristo):** Hakikisha kuwa sehemu hii inapeana injili. Ushuhuda wako huenda ukawa ndiyo nafasi ya kipekee ya mtu kusikia injili. Injili ni: sisi ni watenda dhambi wanaookolewa tu, wakati tunaweka imani yetu katika Kristo aliyefia dhambi zetu, akazikwa akafufuliwa. Maandiko hayasemi kuwa tuliokolewa kwa kutembea na kuingia kanisani, au kumwuliza Yesu aje ndani ya mioyo yetu ama kwa lugha yoyote ya kidini, kuwa dhahiri. Epukana na maneno ya kidini.

**Hii leo, maisha yangu kama Mkristo ni:** Hii sehemu inahitaji kuonyesha manufaa, siyo shida! Zungumzia furaha, amani na msamaha Yesu alipeana. Ikiwa ni lazima utaje shida hizo, sema tangu nimwamini Yesu, amenipa nguvu na amani, hata wakati ule nimekuwa na shida."

## USHUHUDA KIOLEZO

**Tumia hii kama mwongozo wa kuandika ushuhuda wako. Jinsi umekaribishwa kutumia baina ya vifungu sawa na hivi!**

**Hujambo, jina langu ni** Joe DeCitezen

**Ninaishi katika** jiji la Dallas, jimbo laTexas huko Marekani.

**Kabla ya kumfuata Kristo**, Nilijaribu kuwa na furaha kwa kutafuta (kuchuma) fedha, kuenda kwa karamu nyingi, na kuishi nilivyopenda. Lakini vitu hivi vyote vilinifanya tu kuwa mtupu. Nilijua nilikuwa nikitenda dhambi kinyume na Mungu

**Nikagundua kuwa nilimuhitaji** Mungu kuniokoa kutokana na dhambi zangu.

**(Jinsi nilivyofanyika Mkristo)** baadaye marafiki wengine wakanionyesha kuwa Biblia inasema kuwa Mungu alitupenda sana sana, hadi akamtuma mwanawe Yesu Kristo kutufia msalabani, kugharamia dhambi zetu. Yesu alizikwa na baada ya siku tatu, Mungu alimfufua kutoka kwa wafu. Biblia inasema kuwa wale wanaomwamini Yesu husamehewa dhambi zao. Watakuwa na uzima wa milele pamoja na Mungu. Kwa hivyo siku hiyo, nikaweka imani yangu katika Yesu pekee, kuzisamehe dhambi zangu.

Hii leo maisha yangu kama mkristo yamejaa furaha, amani na ndiyo kusudi nina jua kuwa Mungu ananipenda na amenisamehe. Zaidi ya yote, ninajua kuwa ninao uzima wa milele na Mungu.

**Je, ungependa kujua jinsi unavyoweza kuwa na uzima wa milele na Mungu?**

## SASA ANDIKA USHUHUDA WAKO BINAFSI

Ushuhuda wako ni **kifaa cha muhimu** utakachotumia unaposhiriki injili. Uandike ushuhuda huu kwa kifupi hapa chini. Baadaye, fanya mazoezi ya **kuambia** wengine. Mungu atatumia **kazi yake maishani** mwako kuwavutia wengine kumwamini yeye.

**Hujambo, jina langu ni** ______________________________________________

**Ninaishi katika** ______________________________________________________

**Kabla ya kumfuata Kristo**, ______________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

**Nikagundua kuwa nilimuhitaji** ____________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

**(Jinsi nilivyokuwa Mkristo – ongeza mahubiri MAFUPI ya Injili)** ______________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

**Mungu?**__________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

**Leo hii maisha yangu kama Mkristo ni** ________________________________


__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

**Je ungependa kujua jinsi unavyoweza kuwa na uzima wa milele na Mungu?**

 ©2005 e3 Partners Ministry 


KUOMBA
FANYENI UINJILISTI
ZIDISHENI
KUZENI VIONGOZI
FANYENI WANAFUNZI
KUSANYIKE NI PAMOJA



**FANYENI WANAFUNZI**

**KIDOKEZO CHA KUFUNZA**

**Michezo Ya Kuzidisha**

Waulize watu wawili wajitoe Kwa hiari yao kuwa wachungaji. Mwulize kila mmoja achague mtu mmoja kutoka kwa wasikilizaji. Hii inasimamia uinjilisti. Halafu eleza kikundi ya kwamba mchungaji **A** anahubiri kwa mwaka lakini mchungaji **B** anahubiri na kumfunza aliyemwamini Yesu kwa mwaka mmoja. Mwishoni mwa mwaka mchungaji **B** na mwanafunzi wake kila mmoja anamteua mtu mmoja zaidi kutoka kwa wasikilizaji. Awamu nyingine, mchungaji **A** anaenda na kumteua mtu mmoja zaidi kutoka kwa wasikilizaji. Mchungaji **B** na kila mmoja wa wanafunzi wake waenda na kumteua mtu mmoja zaidi kutoka kwa wasikilizaji. Fanya hivi kwa vizazi kadha wa kadha mpaka watu wote miongoni mwa wasikilizaji wachaguliwe. Baada ya vizazi vitano au sita kufanya wanafunzi kwenye kikundi cha mchungaji **B**, kikundi hiki kitakuwa kikubwa sana kuliko kikundi kinachoongozwa na mwinjilisti mchungaji **A.**

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ongezeko: | 1 + 1 = | 2 + 1 = | 3 + 1 = | 4 + 1 = | 5 + 1 = | 6 + 1 = | 7 + 1 = | 8 |
| Kuzidisha: | 1 x 1 = | 2 x 2 = | 4 x 2 = | 8 x 2 = | 16 x 2 = | 32 x 2 = | 64 x 2 = | 128 |
| Kizazi: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |

**Je, mchezo huu wa kuzidisha unatuonyesha nini?**

- Uinjilisti ni huduma ya ongezeko
- Kufanya wanafunzi ni huduma ya kuzidisha. Mabadiliko kwenye vizazi vichache vya kwanza si tofauti sana. Utofauti unakuwa mkumbwa zaidi na mkubwa zaidi kwa kila kizazi kingine cha ziada.
- Kila mtu anataka huduma ya kuzidisha si ongezeko.

## Hatua za Kwanza



# FANYENI WANAFUNZI

**MAWAZO MAKUU**

- Yesu anatuamuru kufanya wanafunzi.
- Yesu na Paulo walifanya wanafunzi kupitia uhusiano, si darasani.
- Changamoto yako ya "Hatua za kwanza" ni kufanya wanafunzi ambao wanampenda na kumtii Yesu Kristo na kufanya wanafunzi zaidi peke yao.

## 1. FUMBO LA MAVUNO: FANYENI WANAFUNZI

Wakati ulio mgumu sana kwa mmea ni baada ya mbegu, kutoka nje, kwa kuvunja udongo. Kwa sababu utaratibu wake wa mizizi ungali mchanga, jua jingi sana, na maji machache sana yanaweza kuufanya mmea ukauke na kufa. Kwa upande mwingine, mvua nyingi sana inaweza kumomonyesha udongo na kung'oa mche kwa msimu huu, mimea michanga inahitaji kuangaliwa kwa karibu na kutunzwa kwa uangalifu.

Katika Mathayo sura ya kumi na tatu, Yesu aonya kuwa waumini wapya, pia wanaweza kuwa katika hali ya kutofahamu, kupata taabu na mateso, wasiwasi wa maisha, udanganyifu wa mali. Lakini pia alitupa mtazamo mdogo wa faida ya ajabu ya wanafunzi:

> Bali aliyepokea mbegu iliyoangukia udongo mzuri ni mtu ambaye analisikia neno na kulielewa. Anatoa mazao yapatayo mia sitini au thelathini mara ya zile zilizopandwa. (Mathayo 13:23).

Tunawaangalia na kuwalea waumini wapya kwa kuwekeza muda na nguvu zetu, kutayarisha roho zao na kuwaandaa kutoa mavuno tele iwezekanavyo.

## 2. MWANAFUNZI NI NINI?

**Soma Luka 14:25-33**

**25**Makutano mengi walipokuwa wakifuatana naye, aligeuka, akawaambia, **26**"kama mtu
akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake na wanawe; na
ndugu zake, na mke wake na wanawe; na ndugu zake waume na wake; naam, na hata
nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. **27**Mtu yeyote asiyechukua
msalaba na kuja nyuma yangu, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. **28**Maana ni nani
katika ninyi, kama akitaka kujenga mnara asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama,
kwamba anavyo vya kuumalizia? **29**Asije akashindwa kuumaliza baada ya kuupiga
msingi, watu wote waonao wakaanza kumdhihaki. **30**Wakisema, mtu huyu alianza
Kujenga, akawa hana nguvu za kumaliza. 31Au kuna mfalme gani akitaka kwenda
kupigana na mfalme mwingine , asiyeketi kwanza na kufanya shauri, kwamba yeye
pamoja na watu elfu kumi ataweza kukutana na yule anayekuja juu yake na watu elfu
ishirini. **32**Na kama akiona hawezi, hutuma ujumbe kutaka sharti za amani, mtu yule
akiwa mbali. **33**Basi kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo hawezi
kuwa mwanafunzi wangu."

### 2.1 Ungemfafanuaje mwanafunzi?

Mwanafunzi ni mwamini ambaye aula yake ya kwanza ni kuwa mwanafunzi kwa muda mrefu maishani na mfuasi wa Kristo.

**"Mwanafunzi ni msomi wa muda mrefu na mfuasi wa Kristo"**

Yesu hakuwahi kukosa tumaini kuhusu wanafunzi kiasi cha kushusha maisha ya viwango vyake juu ya wanafunzi! Alitarajia kitu siyo chini ya hayo wanafunzi wake yafaa waache kila kitu ndivyo waweze kumaliza vema!

Je wanafunzi wako, wako tayari kuacha kila kitu kumfuata Yesu? Je, na wewe? Ikiwa la, kiwango alichoweka Yesu kitakuwa kimeshushwa.

## 3. CHAGUA MWANAFUNZI

**Soma Luka 6:12-13**

12 .Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu. 13 Hata kulipokuwa mchana aliwaita wanafunzi wake, akachagua kumi na wawili miongoni mwao, ambao aliwaita mitume.

### 3.1 Je, Hatua ya Kwanza Ya Yesu Kufanya Wanafunzi Ilikuwa Nini?

Yesu alitaka kuchagua wanafunzi wanaofaa, kwa hivyo alitumia usiku mzima akiomba. Wakati huo, Baba yake alimwonyesha wanaume ambao waliofaa wachaguliwe, ambao ndani mwao Yesu alitakiwa kuweka rasilmali kuu ya wakati na bidii yake. Katika mwanga wa Tume Kuu, kufanya wanafunzi lazima sharti iwe aula ya kwanza. Kuwa mwangalifu usiangalie tu katika sifa za nje za mtu unapochagua mwanafunzi. Wanafunzi bora zaidi ni wale Roho Mtakatifu amewaanda kumtii Kristo.

**Hatua za kwanza**

**Ni akina nani wanaume na wanawake thabiti ambao Mungu amekuandalia kuwafanya wanafunzi?**

*Tazama swali la kumi kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi*

## 4. WEKEZA WAKATI

**Soma Marko 3:14**

14 Akaweka watu kumi na wawili. . . wapate kuwa pamoja naye na kwamba awatume kuhubiri . . .

### 4.1 Je, Njia ya Kimsingi ya Yesu kufanya wanafunzi ilikuwa gani?

Aya hii inasema kuwa mkakati wa Yesu ulikuwa " kuwa nao" Yesu alipowaita wanaume hawa, alisema, " Nifuate," siyo "soma kitabu changu" au "Andika muhtasari mzuri katika darasa langu," Ufuasi ni wa kufaa sana katika uhusiano wa kibinafsi wenye upendo. Wanafunzi waliishi na Yesu, walisafiri naye, walimsikiliza na kumtazama na mwishowe wakaenda nje na kutenda namna ile walivyokuwa wameona akitenda.

 ©2005 e3 Partners Ministry 

Yesu aliwapa habari lakini muhimu zaidi, alijipeana kwao na muda wake.

**Hatua za kwanza**

**Utawekaje rasilmali ya wakati katika wanafunzi wako na ujenge uhusiano nao?**
*Tazama swali la kumi na moja ya mkakati wa ukurasa na utendaji kazi*

## 5. WAFUNZE WANAFUNZI KUMTII YESU

**Soma Yohana 14:15**
[15] **"**Mkinipenda, mtazishika amri zangu."

**5.1 Yesu alisema nini kilichokuwa jaribio la upendo wa wanafunzi wake kwake?**

Yesu alidhihirisha wazi kuwa upendo wetu kwake unadhirishwa ifaavyo zaidi kupitia utii wetu kwake. Waumini tunaowafunza watajifunza kumtii kwa kutazama utii wetu. Kwa hivyo kuwafunza wanafunzi wetu kutii amri za Yesu ni muhimu sana. Utahitaji utaratibu au mpangilio kuwafunza wanafunzi wako amri za Yesu. Tazama "hatua zinazofuata" kikao cha mwisho cha sura kwa ajili ya mashauri.

Hatua za kwanza

**Ni vifaa gani vya ufuasi utatumia kuwafunza wanafunzi jinsi ya kumtii Yeso?**
*Tazama swali la kumi na mbili la mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

## 6.

**Soma Yohana 13:2-15**
[2]Hata Wakati Wa Chakula cha jioni naye ibilisi amekwisha kumtia Yuda, mwana wa
Simoni Iskariote, moyo wa kumsaliti, [3]Yesu hali akijua ya kuwa Baba amempa vyote
mikononi mwake, na ya kuwa alitoka kwa Mungu. [4]Alipondoka chakulani akaweka
kando mavazi yake akatwaa kitambaa, akijifunga kiunoni. [5]Kisha akatia maji katika
bakuli, akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa
alichojifunga. [6]Hivyo yuaja kwa Simoni Petro, Huyo akamwambia, Bwana! Wewe
wanitawadha miguu mimi? [7]Yesu akajibu, akawambia nifanyalo wewe hujui sasa lakini
utalifahamu badaadye. [8]Petro akawmwambia, wewe hutanitawadha miguu kamwe. Yesu
akamwambiaa, kama nisipokutawadha, huna shirika nami. [9]Simoni Petero akamwambia,
Bwana si miguu yangu tu, hata na mikono yangu na kichwa changu pia. [10]Yesu
akamwambia, yeye aliyekwisha kuoga hana haja ila ya kutawadha miguu, bali yu safi
mwili wote, nanyi mmekuwa safi, lakini si nyote. [11]Kwa maana alimjua yeye atakaye
mslaliti, ndiyo maana alisema, si nyote mlio safi. [12]Basi alipokwisha kuwatawadha
miguu, na kuyatwaa mavazi yake, na kuketi tena akawambia, Je mmeelewa na hayo
niliyo watendea? [13]Nanyi mwaniita, mwalimu, na Bwana, nanyi mwanena vema, maana
ndivyo nilivyo. [14]Basi ikiwa mimi niliye Bwana; na mwalimu mimewatawadha miguu,
imewapasa vivyo kutawadha miguu ninyi kwa ninyi. [15]kwa kuwa nimewapa kielelezo ili
kama nilivyo watendea, nayi mtende vivyo.

## Hatua za Kwanza

**6.1 Ni njia gani kuu Yesu alitumia kuwafunza wanafunzi wake jinsi ya kufanya huduma?**

Ilipowezekana Yesu aliwapa wanafunzi wake mfano ama kielelezo. Wakati mwingine alifunza kupitia hadithi au mafumbo. Lakini mara nyingi sana na ifaavyo sana- Alifunza kwa kuufanya mfano mwenyewe.

Hawangewahi kusahau sura ya masihi aliyeahidiwa, mwana wa Mungu, aliyejivua hadi kiunoni akitawadha miguu yao michafu kama mtumishi mnyenyekevu.

Aliwafunza kuhusu sala kwa kuomba, uinjilisti kwa kuihubiri injili ya ufalme na huduma kwa kukutana na mahitaji ya watu.

- **HADITHI YA FELIPE**

Felipe alikuwa mzee wa kanisa katika Kanisa Lake, walipomwuliza asaidie kuanzisha kanisa jipya, kwa furaha alikaribisha kikundi kufanya hivyo. Siku baada ya siku kikundi kilienda mlango kwa-mlango katika Brena kitongoji cha Lima, wakishiriki injili kila siku, watu walikubali msamaha na upatanisho ulionunuliwa kwa ajili yao na mwana wa Mungu. Na kila jioni kikundi hicho kilikutana na waumini wapya katika mojawapo wa makao yao.

Mwishoni mwa juma la kazi kikundi hicho kilirudi kwenye jiji lao la makao na Felipe akaanza kuchunga kundi hili dogo jipya.

Miezi minane baadaye kiongozi wa kikundi hicho alirudi kutembelea hili kanisa jipya. Nyumba waliyopangisha ilifurika watu sitini walisongamana katika hicho chumba, wakijipanga ukutani na kujaza milangoni karibu ishirini walikuwa wamempokea Kristo wakati wa kampeni za kueneza injili, na mavuno yakaendelea.

"Nilifanya kile ulichoniambia, Felipe mkunjufu alimwambia Mike, Kiongozi wa kikundi Miezi miwili kabla ya kampeni ya kueneza injili, Mike alikuwa amefunza hizi kanuni za hatua za kwanza katika mkutano wa uongozi kwa Felipe, wachungaji wengine na wafanyikazi wa kanisa. Felipe alitumia habari hiyo mara moja. Alianza kuwafundisha wanaume watano na vifaa alivyopokea. Hawa wanaume watano walijifunza jinsi ya kufundisha wengine kwa kufundishwa na Felipe.

Baada ya juma la uinjilisti, Felipe aliwachukua wale wanafunzi na wote pamoja wakaanza kuwafundisha waumini wapya. Wale wanafunzi watano walianza kurudi wao wenyewe kuwatembelea waumini wapya wakionyesha uaminifu.

Kwa wastani, Felipe alikumbuka, walikuwa warudi kwa kila mwumini mpya mara kumi kabla ya wao kuja kwa mkutano. Lakini bidii yao na maombi yalilipia, walikuwa wamesaidia kuanzisha kanisa ambalo sasa linajiendeleza na linawasha mwako wa moto ambao unaweza kuenea kwa mfumo wa kuanzisha makanisa.

 ©2005 e3 Partners Ministry 

**6.2 Kwa nini Yesu alinawisha miguu ya wanafunzi wake?**

Akiwa anaongoza kwa mfano, alitaka kuwafunza kwamba mamlaka hayafai kutumiwa vibaya na kwamba kuwa mtumishi ni kitu bora zaidi kuliko kutawala juu ya watu, na ya kwamba kanuni muhimu ya ufalme wake ni kwamba mdogo zaidi ndiye atakayefikiriwa kuwa mkubwa.

**Hatua za kwanza**

**Ni shughuli gani za kihuduma waweza kushiriki na wanafunzi wako kuwawezesha kujifunza kwa kukutazama?**
*Tazama swali la 13 kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi*

## 7. HUSISHA WENGINE KWENYE HUDUMA

**Soma Luka 10:1-7**

1 Basi, baada ya hayo, Bwana aliweka na wengine, sabini akawatuma wawili, wawili wamtangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe.
2 Akawaambia, "Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache, Basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake. 3 Enendeni, angalieni,
nawatuma kama wana kondoo kati ya mbwa-mwitu 4 Msichukue mfuko wala mkoba,
wala viatu, wala msimwamkie mtu njiani 5 Na nyumba yoyote mtakayoingia, Semeni
kwanza Amani iwemo nyumbani humu 6 Na akiwamo mwana wa amani, amani yenu
itamkalia, la hayumo, amani yenu itarudi kwenu. 7 Basi,kaeni katika nyumba hiyo hiyo,
mkila na kunywa vya kwao, maana ,mtenda kazi amestahili kupewa ujira wake. Msihamehame kutoka nyumba hii kwenda nyumba hii."

**7.1 Baadaa ya Yesu kuonyesha jinsi ya kufanya huduma, Yesu aliwataka wanafunzi wake wafanye nini?**

Kama walimu wa shule wanavyotumia warsha na safari za nje kuwapa wanafunzi wao nguvu na uelewaji wa masomo yao, Yesu aliwatuma wanafunzi wake watumie mbinu za utendaji walizojifunza. Kujifunzia kwenye kazi na uanagenzi (apprenticeship) ni njia zinazofaa kujifunza (au kujifunza kwa kutazama) walikuwa wamemwona akifanya uinjilisti. Aliwaambia sasa waende wafanye uinjilisti (Aya ya kwanza) walikuwa wamemsikia Yesu akiomba. Aliwaambia sasa waombee usaidizi zaidi. (Aya ya pili)

**Hatua za kwanza**

**Majukumu gani ya huduma waweza kuwakilisha wanafunzi wako ili wakue?**
*Tazama swali la 14 kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

## 8. SIMAMIA KAZI

**Soma Luka 10:17-20**
[17] Ndipo wale sabini waliporudi kwa furaha wakisema, Bwana hata pepo wanatii kwa
jina lako. [18] Akawaambia, Nilimwona shetani, akianguka kutoka mbinguni kama
umeme [19] tazama nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule
adui wala hakuna kitu kitakachowadhuru. Lakini msifurahi kwa vile pepo
wanavyowatii, bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni.

**8.1 Yesu alifunza je somo muhimu linalohusu ujuzi wa uanagenzi wa wanafunzi?**

Wanafunzi walipata uzoefu mkuu wa kufaulu ambao ulileta majaribu ya kuwa na kiburi na kumnyang'anya Mungu utukufu wake. Kwa hivyo Yesu aliwaongoza kwa upole kuelekea shukrani, kwa kuwakumbusha kwamba furaha yao ilingane na ukweli kuwa Mungu aliwateua wawe wake. Yesu aliwasimamia wanafunzi wake walipoanza huduma. Hakuwaacha pekee kufanya huduma. Aliwasimamia ili wafanye kazi bora.

**Hatua za kwanza**

**Wahitaji kusimamia wanafunzi wako juu ya kitu fulani sasa? Unahitaji kuwasaidia iwapo wana shida?**
*Tazama swali la 15 kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

## 9. MAONO YA KUZIDISHWA

***Soma Mathayo 28:18-20***
[18] Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia "nimepewa mamlaka yote mbinguni
na duniani.[19] Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza
kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu. [20] Na kuwafundisha kuyashika yote
mliowaa muru ninyi na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa
dahari Amina."

**9.1 Kitu gani muhimu ambacho Yesu alikitarajia kutoka kwa wanafunzi wake?**

Yesu alijua kwamba hali ya kuzidisha ndiyo ilikuwa ufunguo wa ongezeko, na alitarajia wanafunzi wake kufanya wanafunzi wengine zaidi. Kwanza alifanya kielelezo. Halafu akawaamuru kwenda kokote na kufanya vile vile.


> **Soma 2 Timotheo 2:2**
> 2 Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.

**9.2 Paulo anataja vizazi vingapi vya wanafunzi?**

Paulo alikuwa na maono sawa ya kuzidisha wanafunzi kama yale Yesu alikuwa nayo. Tunaona hayo katika Timotheo wa pili 2:2 Paulo anaongea hapa juu ya vizazi vinne vya wanafiunzi: 1) Paulo alifunza 2)Timotheo, ambaye aliweka vitu alivyojifunza kutoka kwa Paulo kwa 3) watu waaminifu, ambao wanaweza kufundisha 4) wengine pia.

Neno lililotumiwa katika aya hii “kabidhi” au “weka” ni neno litokanalo na huduma za benki linalomaanisha “ kuwekeza.”

Tunapowekeza ndani ya wanafunzi wetu, tuwatarajie kuongezeka kwa kufanya wanafunzi wengine. Tunapowekeza muda wetu, maarifa, hekima, upendo na bidii ya moyo katika watu waaminifu kundi la wafanya kazi linaloongezeka kila wakati hutokea na Ufalme wa Mungu hupokea faida kubwa mno juu ya kitego cha uchumi wetu wa asili.




**9.3 Paulo alimwaambia Timotheo awekeze ndani ya watu wa aina gani?**

Paulo alimwaambia Timotheo alenge kwa watu wa kutegemewa. Kama vile Yesu aliyekuja kabla ya yeye (Paulo), Paulo hakuchagua yule mkamilifu, bali yule mwaaminifu tu!

**Hatua za kwanza**

**Tumefika wakati wa mwanafunzi wako kupata mwanafunzi wake kibinafsi? Je, ni mabadiliko gani yanahitajika kufanya hali ya kufanya wanafunzi iwe na alama kuu katika huduma yako?**
*Tazama swali la kumi na sita kwenye Mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi*

## Hatua za Kwanza

## 10. KUJIFUNZA KWA MIFANO

**ETHIOPIA –** Wanaotayarisha wanafunzi wanatumia mwelekeo wa mmoja- kwa – mmoja. Kila wakati "Paulo" afundisha somo fulani kwa "Timotheo". Mwanafunzii hawezi kuendelea kwa somo la pili mpaka awe amefundishwa somo la kwanza kwa mwanafunzi wake. Kwa hiyo mwanafunzi siyo tu anajifunza mwenyewe, lakini pia natii akifundisha wengine.

Halafu, Timotheo anapopokea somo la pili, lazima tena alifunze kwa wanafunzi wake kabla hajaweza kupokea somo la tatu. Mwanafunzi wa pili lazima afuate mtindo sawa. Na vile vile, kiwango baada ya kiwango. Mwanafunzi baada ya mwanafunzi. Njia hii ilianza kwa udogo na wachungaji wakuu wanne waliokuwa wawili wawili.

Baada ya miaka mitano imeongezeka kwa mamia ya makanisa. Kwa miaka mitano idadi ya vifaa elfu ishirini na tano (25,000) vya kufanya mwanafunzi katika lugha tatu vinashirikishwa mmoja – kwa – mmoja kwa kuongezea katika maneneo mengi mashambani 20-50-1000 nakala zilizoandikwa kwa mikono vimefanywa kutoka kwa idadi nyingi zilizochapishwa.

Mchungaji mmoja mwenye kipawa cha kubuni hata ameendeleza alama za mkono, Aya za kumbukumbu na michoro inayoweza kuchorwa katika udongo kusaidia wasioweza kusoma kukumbuka ukweli wa ufuasi na kuushiriki na wengine. Wanafunzi wanakua kwa kutumia neno la Mungu, na kupitisha mara kwa mara. Mwanafunzi wa Yesu Kristo anakua katika urafiki ulio wa karibu sana na Mungu katika kutii neno la Mungu, kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Na kwa ujuzi na ujasiri kuhudumia wengine. Lakini la muhimu zaidi wanafunzi kutoa-tena, wanaotayarisha wanafunzi zaidi.

**Mnyororo wa ufuasi**

Hapa kuna njia ya ajabu juu ya umuhimu wa kuwa na vizazi vya wanafunzi. Mwulize kila mmoja asimame na waunganishe mikono yao pamoja wakiunda mnyororo mrefu kupitia eneo la mafunzo. Sasa tembea kwa mtu mwingine katikati ya mnyororo na uvunje ungo lake na waulize wale wote walio nyuma yake waketi. Eleza kuwa mwanafunzi mmoja anaposhidwa kuwekesha kwa wengine anavunja mnyororo wa neema inayoenea kupitia rika na kutotii kwake huwazuia wale ambao wangekuja baada yake! Mnyororo wa neema unaendelea kwa wakati wote wa historia. Viungo vyake ni wanafunzi watiifu wakishiriki - Injili na kujitoa tena wenyewe. Kila kiungo kina pande mbili moja kushika na nyingine kushikiliwa. Tunapokosa kufanya wanafunzi kutoa tena wakristo, tuna wanyaganya furaha ya huduma na tuna nyangaya kanisa rasilmali yake ya dhamana zaidi.

**PERU**
Mchungaji mmoja anatumia njia ya muda wa kujifunza. Anawachukua waumini wapya pamoja naye kufanya huduma ya kufikia watu ili wajifunze kwanza kwa kutazama. Kwa wakati fulani, aliwapa jukumu zaidi mpaka wengi wakawa wachungaji wa makanisa yao ya nyumbani.

**INDIA:**
Katika mfumo mmoja wa kuanzisha makanisa, kiongozi wa nyumba anafusa familia yake mwenyewe kama kiongozi anavyomfundisha yeye. Katika njia hii familia nzima zinafuswa na kuimarishwa, na viongozi wapya hutokea kwa urahisi kupitia mafunzo kwenye kazi. Kama vile kiongozi wa nyumba akiwaleta wengine katika mfumo wake wa uhusiano, yeye huwa mwalimu na anafuata kielelezo sawa.

**VIKUNDI VIDOGO:**
Viongozi wengine kote duniani wanatumia vikundi vidogo, vikundi vya nyumbani kufusa waumini wapya na wale wanaokomaa. Wengine wanatumia vikundi vya kusikiliza.na wanaosikiliza fungu la Biblia lililorekodiwa huweza kujadiliana juu ya kile wanachosikia.

## Hatua za Kwanza

**HATUA ZA KWANZA**

**Hivi ni vifaa vya kufanya wanafunzi vinavyofuata -**

1. Amri za msingi za Yesu (ufuasi bora wa somo la kwanza kwa waumini wapya)
2. Ulimwengu wawezaje kuja haraka kwa Yesu (kuzidisha kukilinganishwa na ongezeko)

**HATUA ZINAZOFUATA**

Utahitaji mtalaa (curriculum) mzuri kuwasaidia wanafunzi wako wakue. Kuna mitalaa mingi tofauti inayo patikana kwenye lugha nyingi. Hapa pana mbili bora

- Maisha mapya katika Yesu, Juzuu ya kwanza (Vol. 1)
- Maisha mapya katika Yesu, Juzuu ya pili (Vol. 2)
- Vifaa hivi vinapatikana katika lugha nyingi kwenye mtandao katika *http://www.nuevavidaencristo.org/*

Kitabu bora kusoma ni mpango stadi wa uinjilisti kilichochapishwa na Robert Coleman. Pengine waweza kupata Nakala katika duka maalumu la kikristo la vitabu.

Campus Crusade For Christ imetafsiri hatua kumi za ukomavu wa mkristo katika lugha tofauti. Waweza kufikia waraka wa uinjilisti huu wa uanafunzi kwenye mtandao: *http:www.10basicsteps.com/*

Wafunze wanafunzi wako Amri Kuu za Yesu na ujifunze zaidi juu ya ushauri. Tazama katika mtandao: *http://www.mentorandmultiply.com/*

Sehemu muhimu za Biblia katika mtandao ni funzo kwa waumini wapya kuwasaidia kuwa na uzoefu na maandiko matakatifu na jinsi ya kujifunza. Inapatikana katika kiingereza, Bengali, Kihindi na Kichina. Mtandao: *http://www.biblekeysonline.com/*

Recursors espanol: en Espanol: *http://www.obrerofiel.com*

**Kwa mafunzo zaidi**:
Mafunzo ya Omega juu ya “Kufanya Wanafunzi” yanapatikana kwenye mtandao katika: *http://www.alliancescp.org/resources/omegacourse.html*

**KITABU CHA MAELEZO CHA TATU**

**Somo la Kwanza**“Utangulizi wa Kufanya Wanafunzi”
**Somo la pili** ”Kazi Yako Kwenye Kuwafanya Wanafunzi”
**Somo la tatu** “Ujue Lengo lako, Watu Wako”
**Somo la nne** “Kuwasaidia Wanafunzi Wakue Kiroho”
**Somo la tano** “Utaratibu wa Mitindo ya Kufanya wanafunzi.

**KIFAA**

# AMRI ZA KIMSINGI ZA YESU

Yesu alifunza vitu vingi wakati wake ulimwenguni. Mtume Yohana asema kwamba kama vitu vyote Yesu alivyotenda, vilirekondiwa, basi vitabu vyote duniani havingeweza kutoshea. (Yohana 21:25)

Kwa hivyo basi jinsi gani sisi kama viongozi twatii Amri za Yesu "kufunza kila kitu ambacho nimeamuru"? Ingawa inaonekana kama jukumu lisolowezekana, Amri zote za Yesu zinaingiana kwenye vikundi saba tunavyoita "Amri za Kimsingi za yeso." Wafunze wanafunzi wako kuzikumbuka, kuzitumia na kutoa tena Amri hizi saba za kimsingi. Zungumzia umuhimu wa Amri na mpitie maandiko matakatifu pamoja. Waweza kutilia nguvu kufunza huku kwa kuonyesha jinsi Amri zote za Yesu ambazo zimerokodiwa katika maandiko matakatifu zimo ndani ya moja ya vikundi hivi:

1. Tubu, Amini na upokee Roho Mtakatifu uweze kubadilika.
   Mjadili kile Yesu anamuru katika aya zifuatazo:
   Mariko 1:15, Yohana 3:16, 20:22

2. Ubatizwe na uthibitishe toba na maisha mapya katika Yesu:
   Mjadili ni nini Yesu aaamuru katika Aya zifuatazo: Mathayo 28:18-20

3. Mpende Mungu, wanafunzi wenzako, Jirani, wanaohitaji na Adui zako:
   Mjadili kile Yesu anaamuru katika aya zifuatazo: Luka 10:25-37,
   Yohana 13:34, Mathayo 6:14-15

4. Uvunje mkate katika ushirika na mwabudu Mungu:
   Mjadili kile Yesu anaamuru katika aya zifuatazo Mathayo 26:26-28

5. Omba wakati wote kupitia maombezi ya familia na ibada ya kibinafsi, uponyaji na vita vya kiroho:
   Mjadili kile Yesu anaamuru katika aya ifuatayo: Yohana 16:24

6. Patiana usimamizi wa wakati wako, hazina na vipawa:
   Mjadili kile Yesu anaamuru katika aya ifuatayo: Luka 6:38

7. Wafanye wanafunzi kwa kuwa mshahidi, kufunza neno la Mungu, Uchungaji wa waumini wapya na kufunza viongozi:
   Mjadili kile Yesu anaamuru katika aya zifuatazo: Matendo 1:8,
   Yohana 21: 15-17

*Imetolewa kwa ruhusa kutoka kwa kifaa cha George Patterson katika mtandao wa:
*www.mentorandmultiply.com*

**ULIMWENGU UNGEKUJAJE HARAKA KWA YESU**

KWA ONGEZEKO

- Mhubiri mmoja anawaleta **watu 3000 Kwa Yesu kila siku** (kama siku ya pentekosti katika Matendo 2:41)

KWA KUZIDISHA

- Mkristo mmoja huleta watu wawili kwa Yesu kwa mwaka wa kwanza .
- Kila mwaka baadaye **kila** mkristo huleta watu wawili zaidi.

| Mwaka | Wakristo mwanzo wa mwaka | Watu waliookoka kila mwaka | Wakristo mwanzo wa mwaka | Watu waliokoka kila mwaka |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | Milioni 1.1 | 1 | 2 |
| 2 | Milioni 1.1 | Milioni 1.1 | 3 | 6 |
| 3 | Milioni 2.2 | Milioni 1.1 | 9 | 18 |
| 4 | Milioni 3.3 | Million 1.1 | 27 | 54 |
| 5 | Milioni 4.4 | Milioni 1.1 | 81 | 162 |
| 6 | Milioni 5.5 | Milioni 1.1 | 243 | 486 |
| 7 | Milioni 6.6 | Milioni 1.1 | 729 | 1,458 |
| 8 | Milioni 7.7 | Milioni 1.1 | 2,187 | 4,374 |
| 9 | Milioni 8.8 | Milioni 1.1 | 6,561 | 13,122 |
| 10 | Milioni 9.9 | Milioni 1.1 | 19,683 | 39,366 |
| 11 | Milioni 11.0 | Milioni 1.1 | 56,049 | 118,098 |
| 12 | Milioni 12.1 | Milioni 1.1 | 177,147 | 354,249 |
| 13 | Milioni 13.2 | Milioni 1.1 | 531,441 | Milioni 1 |
| 14 | Milioni 14.3 | Milioni 1.1 | Milioni 1.6 | Milioni 3 |
| 15 | Milioni 15.4 | Milioni 1.1 | Milioni 4.8 | Milioni 9.5 |
| 16 | Milioni 16.5 | Milioni 1.1 | Milioni 14 | Milioni 28 |
| 17 | Milioni 17.6 | Milioni 1.1 | Milioni 43 | Milioni 86 |
| 18 | Milioni 18.7 | Milioni 1.1 | Milioni 129 | Milioni 258 |
| 19 | Milioni 19.8 | Milioni 1.1 | Milioni 387 | Milioni 774 |
| 20 | Milioni 20.9 | Milioni 1.1 | Bilioni1.1 | Bilioni 2.3 |
| 21 | Milioni 22.0 | Milioni 1.1 | Bilioni 3.5 | Bilioni 7 |
| Endelea _ _ _ _ | Endelea . . . | Endelea . . . | | |
| , , , , , , , , | ………. . | ………. . | | |
| 5,480 MIAKA | Bilioni 6 | Milioni 1.1 | | |

ONGEZEKO LA Wakristo 3000 **kila siku** huchukua zaidi ya **miaka 5,480** kufikia watu bilioni 6 !


- Kwa mtindo huu kufanya kazi watu wengi wahitaji KUWA HAI KWA MIAKA 5,480 na idadi Ya watu duniani HAIWEZI kukua.
- Kwa hiyo, mtindo wa ongezeko HAUWEZI kufanya kazi ifanyike!

Lakini UZIDISHAJI hufikia WATU BILIONI 10.5 KWA MIAKA 21 TU!

- UZIDISHAJI ndio tu njia ya kufikia ulimwengu!
- Hii inamaanisha kwamba **KILA** mmoja wetu lazima afuate amri za Yesu katika Mathayo 28:19, ambayo

**KUFANYA WANAFUNZI!**

 ©2005 e3 Partners Ministry 


KUOMBA
FANYENI
UINJILISTI
ZIDISHENI
KUZENI
VIONGOZI
FANYENI
WANAFUNZI
KUSANYIKE
NI PAMOJA



**KUSANYIKENI PAMOJA**



# KUSANYIKENI PAMOJA

**MAWAZO MAKUU**

- Makanisa yenye afya huzidishwa.
- Kanisa ni “kikundi cha Waumini waliobatizwa chenye kiongozi mmoja au wengi. Wanaokusanyika pamoja mara kwa mara kutii amri za Kristo.”
- Unahitaji mpango kuimarisha sehemu zenye udhaifu za kanisa lako.
- Unahitaji mpango kuanzisha kanisa jipya.

## 1. FUMBO LA MAVUNO: KUSANYENI PAMOJA

Siku mkulima alioiona katika maono kutoka mwanzoni imekuja - maono yaliyomuweka akifanya kazi kwa bidii siku baada ya siku kwenye jua kali akimtegemea Mungu kwa ukuzi, wakati ambapo hangeona akiendelea mbele..

Mazao sasa ni meupe. Ni wakati wa kuvuna! Hathubutu kukawia:

> Pia akasema, “Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbega juu ya nchi. Akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. Maana nchi huzaa yenyewe, kwanza jani,tena suke, kisha ngano pevu katika suke. Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika.”(Mariko 4:26-29)

Wakati wa mavuno ni mara mbegu inapoiva kukawia kwa aina yoyote kunahatarisha mazao na ni usimamizi mbaya wa mbegu ambayo Mungu ametukabidhi.

Mara ikishavunwa mazao huletwa katika ghala. Kanisa ni ghala inayohifadhi mavuno. Kuacha mazao mapya yaliyovunwa huko shambani yatanyauka na kukauka, kuoza au kuliwa na wadudu. Kuacha mwamini mpya peke yake duniani baada ya kumkubali Yesu ni kuhatarisha maisha yake, atakauka na kuanguka na kumalizwa na maadui wa Mungu.

## 2. KIELELEZO CHA KANISA LA YERUSALEMU

Kanisa la karne ya kwanza huko Yerusalemu ni mfano mkuu wa kanisa lenye afya na lifaalo. Hebu tutazame kwa nini?

**Soma matendo 2:42-47**
42 Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume na katika ushirika , na katika kuumega mkate, na katika kusali. 43. Kila mtu akaingiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume 44. Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja na kuwa na vitu vyote shirika, 45. Wakiuza mali zao, na vitu vyote walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja. 46 Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu,wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, 47. Wakimsifu Mungu , na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.

**2.1 Ungependa kitu gani bora kama ungalikuwa mshiriki wa kanisa hili?**

Ebu wazia jambo hili! Kila mmoja karibu nawe yuko imara katika imani. Unafundishwa na wale watu ambao walikuwa na Yesu kuanzia mwanzoni mwa vitu vyote ambavyo Yesu aliwafundisha. Kanisa lenu ni kama familia iliyo ya karibu na yenye upendo, wanaokula na kuomba pamoja. Ninyi nyote mnamcha Bwana, ambaye maandiko yanasema ni mwanzo wa hekima na maarifa, ninyi nyote mna kila kitu mnachohitaji, kuongezea-muko na furaha pamoja na uwezo wa kushiriki na wengine. Hambishani juu ya mafundisho ya dini au mambo hafifu. Ninyi nyote ni wakarimu, mkiutumia wakati pamoja katika nyumba ya kila mmoja. Mnafurahia kumsifu na kumwabudu Mungu pamoja mkiwa na kibali cha kila mmoja karibu nanyi, na sasa hivi kanisa lenu halikomi kukua!

**2.2 Twawezaje kutambua kanisa lenye afya?**

Tunajua mmea au mti una afya kwa sababu unakua na kuzaa matunda. Ni sawa na kanisa. Washiriki waliendelea kukua katika neema, nguvu, kibali na ukomavu na idadi ya washiriki iliendelea kukua katika ukubwa.

**2.3 Hebu tuchukue swali fupi: kulingana na fungu hili, kanisa hili lenye afya na la kukua kwa haraka katika Yerusalemu lilikuwa na kitu gani?**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Waumini | Ndiyo | Hapana |
| 2. Viongozi | Ndiyo | Hapana |
| 3. Ushirika | Ndiyo | Hapana |
| 4. Ibada | Ndiyo | Hapana |
| 5. Uinjilisti | Ndiyo | Hapana |
| 6. Ufuasi | Ndiyo | Hapana |
| 7. Huduma | Ndiyo | Hapana |
| 8. Meza ya Bwana | Ndiyo | Hapana |
| 9. Kiongozi aliyefunzwa katika Seminari | Ndiyo | Hapana |
| 10. Fedha | Ndiyo | Hapana |
| 11. Jengo la kanisa | Ndiyo | Hapana |
| 12. Mchungaji anayelipwa | Ndiyo | Hapana |
| 13. Idadi ya washiriki kiasi | Ndiyo | Hapana |
| 14. Idadi ya washiriki ya chini kabisa | Ndiyo | Hapana |

* *(Majibu yanapatikana katika ukurasa wa 83)*

## Hatua za Kwanza

**2.4 Vitu hivi ni vya lazima? Au ni vyenye msaada vinapopatikana?**

**Viongozi waliofundishwa katika seminari** – Viongozi wawe tayari kufunzwa na wawe tayari kujifunza kila mara. Lakini shahada ya Seminari si sharti la Agano Jipya kwa Yesu na kwa Paulo, tabia na utiifu vilikuwa vitu muhimu zaidi.

**Jengo la kanisa** – Kanisa la mwanzo walikutana katika jengo la umma kama hekalu na katika nyumbani mwa watu binafsi. Mahali pa kukutana pa aina hii ni pazuri kwa ujenzi wa kanisa, kwa kuwa hakuna kutengemea mikopo mikubwa ya fedha. Hamna hitaji la vibali vya kiserikali na hakuna ukusanyaji wa pesa wa kila mara.

**Kulingana na Matendo 2:42-47, tunaweza kufafanua kanisa kama "Kikundi** cha Waumini waliobatizwa chenye kiongozi mmoja au zaidi, wanaokusanyika mara kwa mara kutii amri za Kristo."

**Mchungaji wa kulipwa** – Kuwa na pesa za kulipa mchungaji na watumishi kunaweza kuwa baraka, lakini si amri. Waumini ni waumini kama wana mchungaji na sio mkurugenzi mkuu. Wachungaji wengi sana lazima wafanye kazi nyinginezo na wasimamie vyema (hasa wanapofahamu na kufanya mazoezi na kanuni za ufuasi) kanisa jipya.

**Idadi ya chini ya washiriki iliyo sawa** – kwa kufafanua, Yesu alisema kwamba panapokusanyika wawili au zaidi katika jina lake………hapo kuna kanisa. Wanaweza kuwa wachache sana kujisaidia,lakini si wachache sana kuzalisha!

**2.5 Kanisa lako lina Afya kiasi gani?**
*(vingirisha jibu kwa kila mmoja)*

| | Dhaifu | | | enye nguvu | |
|---|---|---|---|---|---|
| Uinjilisti | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| Ufuasi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| Ibada | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| Ushirika | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| Huduma | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| Ukuzi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

**Hatua za kwanza**

**Hatua gani wahitaji kuchukua kuimarisha sehemu dhaifu kanisani mwako?**
*Tazama swali la 17 kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi*

**Hatua za kwanza**

**Utawakusanyaje waumini wapya Pamoja kuanzisha kanisa jipya?**
*Tazama swali la 18 kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi*

Sisi sote twataka kuwa mojawapo wa kanisa ambalo ni la ajabu kama kanisa la karne ya kwanza huko Yerusalemu. Kwa hiyo wewe na timu ya huduma yako mwahitaji

kujadiliana na kuamua kwamba, hali inayoendelea kukua yenye furaha, upendo na kujifunza, katika kanisa jipya unaloanzisha, ipo.
Unahitajika kutumia vifaa vinavyoweza kufanya kazi vema zaidi katika hilo eneo, ambapo mnaanzisha kanisa jipya. Katika maeneo mengine,vikundi vya kujifunza na kusoma Biblia vinafanya kazi vema zaidi. Au labda, vikundi vidogo vitatimiza kazi hiyo. Wengine, huanzisha vile vinavyoitwa " vikundi vya kusikiza" ambapo washiriki husikiza nakala ya Biblia kwenye kanda ya kaseti na baadaye kujadili yale waliyosikiza.

**Hatua za kwanza**

**Ni mahali gani, ambapo hicho kikundi kipya watakutania? Je, ni nyumbani? Au mahali pengine?**
*Tazama swali la kumi na tisa kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

**Hatua za kwanza**

**Je, hicho kikundi kipya watakutana mara ngapi? Je, ni siku gani (Na) Ni wakati gani kwa kila siku?**
*Tazama swali la ishirini kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi*

**HATUA ZA KWANZA**

**Vifaa vifuatavyo ni vya kukusaidia kukusanya pamoja waumini wapya**

1. Maelezo ya kuanzisha mikutano kwa ajili ya vikundi (vidogo vya nyumbani).
2. Manufaa ya kuanzisha kanisa jipya kutokana na kanisa lililopo.
3. "Kuanzisha kanisa la kimsingi" linaoweza kutumiwa nanyi, kuweka katika matendo kanuni katika kijitabu hiki cha maelezo ya matumizi- Hatua Za Kwanza.

**HATUA ZINAZOFUATA**

Mafunzo ya Paulo na Timotheo (*http://www.paul-timothy.net/*) yamestawisha vifaa kadhaa vilivyo rahisi vya kukusaidia na kukupa mwongozo unapoanzisha makanisa mapya.

**"Anzisha kanisa lako mwenyewe"** ni nakala ambayo inatoa orodha ya mada muhimu na maswali ya kukuongoza kupitia njia ya kuimarisha kanisa jipya. Hiki kifaa kinaweza kutolewa chapa katika mtandao huu: *http://currah.info/www/paul-timothy/docs/ptt_start_your_own_church.pdf*

**"Kuza jamii na seli"** Ni mwongozo wa majadiliano wa kuongoza timu yako kuwa na uanzishaji wa makanisa kupitia kwa kubuni mikakati ya kuimarisha kanisa jipya. Hiki kifaa kinaweza kutolewa chapa kutoka kwa mtandao huu: *http://currah.info/www/paul-timothy/docs/develop_community.pdf*

**"Mwongozo wa kimsingi"** Hutoa orodha ya mada muhimu, kumi na tatu (13) ambazo zinahitajika kufunzwa wakati ambapo makanisa mapya yanaimairishwa. Hiki kifaa kinaweza kutolewa chapa kwenye mtandao huu: *http://www.harvestimpact.org/eng/BasicChurchGuide.doc*

**"Kuanzisha kanisa la kimsingi"** Ni nakala rahisi mno inayotoa maelezo ya ukuzaji na ya kuimarisha kanisa la kinyumbani. Kimeandikwa na ("Harvest Impact") .Hiki kifaa kinaweza kutolewa chapa kutoka kwa mtandao huu: *http://www.harvestimpact.org/eng/BasicChurch-HowtoStart.doc*

## Hatua za Kwanza

**HATUA ZA KWANZA**

**Kwa mafunzo zaidi:**
Vipindi vya masomo ya "Omega course" juu ya "vikundi vya seli" vinapatikana katika mtandao huu: *http://www.alliancescp.org/resources/omegacourse.html*

**Kitabu cha maelezo cha pili**

| | |
|---|---|
| **Somo la kwanza** | " Kazi na manufaa ya vikundi vya seli." |
| **Somo la pili** | " Kanuni za uongozi wa kikundi cha seli." |
| **Somo la tatu** | " Kuanzisha kikundi cha seli." |
| **Somo la nne** | " Uinjilisti wa kikundi cha seli." |
| **Somo la sita** | "Filosofia ya Huduma ya kikundi cha seli." |

**Kitabu cha Maelezo cha tatu**

| | |
|---|---|
| **Somo la saba** | "Kuendesha mazungumzo ya kikundi cha seli." |
| **Somo la nane** | "Kushughulikia watu katika kikundi cha seli." |
| **Somo la tisa** | "Kufunza viongozi wapya wa kikundi cha seli." |

**Kitabu cha maelezo cha nne**
**Somo la kumi na moja** " Kuzidisha kikundi cha seli."

**Kitabu cha maelezo cha tano:**
**Somo la kumi na mbili** "Seli zinajaa kupitia kwa makanisa ya asili.
**Somo la kumi na Tatu** "Kusimamia seli."

*Mifululizo ya masomo ya "Omega course" juu ya "kanisa" vinapatikana kwenye mtandao huu: http://www.alliancescp.org/resources/omegacourse.html*.

**Kitabu cha maelelezo cha kwanza**

| | |
|---|---|
| **Somo la kwanza** | "Misingi ya kibiblia kwa ajili ya kanisa" |
| **Somo la pili** | "Kusudi la kanisa" |
| **Soma la tatu** | "Umbo na utendaji" |
| **Somo la nne** | "Kufafanua kanisa la kimsingi |

**Kitabu cha maelezo cha pili:**
**Somo la tano** "Asili ya kanisa"

**Jibu la swali 2.3 kwenye ukurasa wa 80: Kulingana na kifungu hiki cha maneno, ni 1 hadi 8 pekee vinavyohitajika. Vipengele 9 hadi 12 huenda vikawa msaada, lakini si lazima.**

KIFAA

# MAELEKEZO YA MKUTANO WA KIKUNDI CHA SELI

**1. MAKARIBISHO**

Msaidie kila mtu kumjua mwezake na ajisikie amestarehe. Mwulize kila mmoja ajibu maswali yafuatayo:

> *Jina lako ni nani? Uliishi wapi kati ya umri wa miaka saba na kumi na miwili? Ulikuwa na watu wangapi katika familia yako?*

Unapoenda kandokando ya mviringo mfanye kila mmoja arudie jina la mtu ambaye anamfuata. Muwe na furaha kwa kuufanya wakati huu kama mchezo.

**2. KUABUDU**

Tuwe na mtu aongoze wimbo rahisi. Uufunze wale wapya. Msiwaaibishe wageni, wafanye wajistareheshe kwa kuwafundisha wimbo na kuwatarajia kujiwazia wenyewe.
Omba ombi lililo rahisi kwa Roho Mtakatifu kutoa ufahamu wakati wa mkutano.

**3. NENO**

Tumia somo la kwanza la masomo ya ufuasi unayotumia.

- Kwanza wafundishe waumini wapya jinsi ya kutumia Biblia.
- Waonyeshe jedwali la yaliyomo. Wafundishe jinsi ya kutafuta kitabu cha Biblia kilichotajwa katika maswali. Waonyeshe sura ni nini na aya ni nini. Pitia maswali kadhaa ya kwanza na uwe na watu tofauti, kusoma sura na kujibu maswali.

Baada ya kumaliza kujadili maswali matatu au manne, wasilisha Injili kwa wale wasioamini kwa kutumia kijitabu cha “e3 PARTNERS” Ama unaweza kutoa ushuhuda wako kuwasilisha Injili baadaye tumia ombi katika kijitabu cha “e3 PARTNERS” kuwaongoza kwa Kristo.

**4. KAZI**
“Una ndugu, marafiki , au majirani ambao wangependa kusikia kuhusu Biblia na Yesu Kristo? Tunaweza kukutana nao lini?”

Waombee watu hawa. Halafu jaribu kupanga tarehe za kuwatembelea watu hawa.

Ongea na kila mmoja kibinafsi kabla hawajaondoka. Mpe kila mtu usikivu maalumu.

## JINSI YA KUTUMIA VIKUNDI VYA SELI KUJENGA KANISA

**Kwa kawaida vikundi vya seli vinatumika kukuza na kupanua makanisa yalioko. Pia ni njia moja yenye nguvu sana ya kuanzisha kanisa jipya. Anzisha kikundi kidogo cha seli katika eneo ambapo kanisa lako linataka kuanzisha kazi mpya. Kama ukitumia" mnara wa maombi", mkakati uliotajwa katika sura ya maombi, kikundi cha seli ni njia moja nzuri ya kuendeleza kikundi cha maombi, ndani ya kazi mpya ambayo siku moja itakuwa kanisa jipya.**

## NI MAELEKEZO GANI YA KUANDAA MKUTANO WA KIKUNDI?

**MAKARIBISHO YA** *(dakika 15)*

- Msaidie kila mtu ajuane na mwezake na astarehe. Mwulize kila moja ayajibu maswali yafuatatyo:
    1. Jina lako ni nani?
    2. Swali la mwanzo
- Tumia maswali ya mwanzo yasiyopendelea upande wowote.
- Mfanye kila mtu aongee. Kiongozi kuweka mfano, kwa kusema yeyé ni nani.
- Wapate watu wanaohusiana.

**KUABUDU** *(dakika 15)*

- Mpate mtu afunze wimbo mmoja au nyimbo mbili rahisi kwa kikundi chote kama hakuna yeyote anayeufahamu. Fanya hivi, ili usichague wageni, usiwaaibishe kwa sababu hawaujui wimbo.
- Tumia maombi au sala iliyo rahisi kwa Roho Mtakatifu aweze kupeana ufahamu wakati wa mkutano.

**NENO** *(dakika 30-40)*

- Hakikisha kwamba kila mtu ana Biblia.
- Kwanza wafundishe waumini wapya jinsi ya kutumia Biblia.
- Waonyeshe jedwali la yale yaliyomo.
- Wafundishe jinsi ya kutafuta kitabu cha Biblia kilichotajwa kwenye maswali.
- Waonyeshe sura ni nini na aya ni nini.
- Pitia "maswali ya majadiliano" na uwe na watu tofauti wakusoma mafungu na wakujibu maswali.
- Kwa mbinu, ongoza majadiliano ili kusiwe na mtu wa kuongea wakati wote, bali kila mtu awe na nafasi ya kushiriki, lakini usimwaibishe yeyote ambaye hana moyo wa kushiriki. Usifuate mpangilio kwenye mviringo.

**KAZI** *(dakika 15-20)*

- Huu ndio wakati wa kushirikisha maono. Tupo hapa ili kuwafikia majirani na injili.
- Waulize ikiwa yeyote ana hitaji la maombi. Mtu akiwa na hitaji, mara ile waulize kama kuna mtu ambaye anataka kumwombea mtu huyo. Kama hakuna aliyejitolea, kiongozi amwombee mtu huyo.
- Watie watu moyo kuombeana kwa kutaja majina na kuyataja mahitaji yenyewe. Endelea mpaka mahitaji yote yameombewa mara moja na kwa kila mmoja.
- Waulize watu kutaja watu wanao wajua kwamba wanahitaji Kristo, halafu waombewe.
- Funga kwa maombi mafupi.
- Ongea na kila mtu kabla hajaondoka. Jaribu kumpa kila mtu usikivu wa kipekee.

## MAHALI GANI TWAANDAA MAPISHI HAYA?

- Nyumbani kwa washiriki ni sehemu zilizolengwa na ni bora, kwa vile hazina hatari nyingi.
- Familia inayokaribisha iwe na sifa nzuri.
- Huenda kukawa na hitaji la kubadilisha wanaokaribisha kwa zamu.
- Hali ya mkutano iwe ya kawaida - mpangilio wa viti uwe wa dwara.

## TWAANDAA MAPIHI HAYA LINI?

- Kila jioni wakati wa kampeni ya kueneza injili.
- Mara moja kwa juma baada ya hiyo kampeni – weka wakati kila juma.
- Pangia lisaa moja na nusu hadi masaa mawili.
- Chagua wakati Fulani jioni ulio bora katika tamaduni yenu – ikiwezekana uwe sawa kama ibada nyingine za jioni.

## TWAMWANDALIA NANI MAPISHI

- Kila mmoja anayefanya ungamo la imani.
- Shirikisha washiriki wengine wa kanisa zazi.
- Amua kama mtashirikisha watoto katika mkutano wenu au kuwaandalia mkutano mwingine wa kivyao.
- Wenyeji wahusishwe katika mkutano watachukuliwa kama viongozi kwa sababu mkutano upo katika nyumba yao.

## KWENDELEZA MAPISHI YAKO MWENYEWE

**1. Kukiandaa chakula chenyewe**

(a) Chagua fungu kutoka kwenye Biblia kama vile fumbo au hadithi kutoka kwa vitabu vya Injili au sehemu kutoka kwenye Nyaraka. Pengine ni fungu kutoka katika mahubiri yako ya Jumapili.
(b) Fikiria kuhusu fungu katika sehemu tofauti na utunge swali litakalowafanya wana kundi kujadili kile fungu linasema. Maswali matatu au manne yatatosha.
(c) Tunga swali au maswali mawili ambayo yatalifanya fungu lilingane na jinsi tunavyoishi maisha yetu ya kila siku.
(d) Sasa unao msingi wa majadiliano ya dakika kidogo.
(e) Tunga swali lisilo la kiroho ambalo yeyote anaweza kulijibu kama ni mkristo au la - ambalo linalenga fungu. Kusudi la swali hilo ni kumfanya kila mmoja ajistareheshe, na kushiriki kwenye majadiliano.
(f) Sasa unacho kile'chakula"

**2. Orodha ya Vyakula**

(a) Gawanya karatasi moja kwenye sehemu nne na uzipe vichwa:
1) Makaribisho 2) Ibada 3) Neno 4) Kazi
(b) Toa maagizo kwa kila sehemu.
(c) Katika sehemu ya "Makaribisho" kila mmoja yafaa apeane jina lake na ajibu swali la kustarehe kumhusu yeye, mwenyewe. Kusudi ni kufanya hali isiyo rasmi ambayo kila mmoja anapata kuongea. Fanya mchezo kutokana na hali hii.
(d) Katika sehemu ya "Ibada" wafundishe watu wapya jinsi ya kumwimbia Mungu sifa kwa kuwafundisha pambio moja au mbili. Waweza kuchagua nyimbo rahisi zinazoambatana na fungu lililosomwa.
(e) Katika sehemu ya "neno" , watie moyo wote katika kikundi kushiriki wakati wa mjadiliano ya fungu lile la Biblia.
(f) Katika sehemu ya Kazi muruhusu Roho Mtakatifu afanye kazi. Kila mmoja aliye na ombi ajisikie mwenye kupendwa na kuazwa wakati mtu mwingine katika kikundi hicho anapomwombea hapo hapo kwa kumtaja jina. huku akiliinua hitaji lake kwa Bwana. Tazama majibu kwa maombi ambayo Mungu anatoa kupitia kikundi.

**3. Kufuasa (Kufanya Wanafunzi)**

(a) Fanya nakala za orodha za vyakula za kutosha kwa wanaume na Wanawake waliokomaa katika kanisa lenu. Waweke nakala moja inayopatikana katika jalada zao kwa urahisi.

(b) Kila Juma tayarisha ukurasa wa "chakula" wenye maswali ya majadiliano juu ya fungu la juma hilo.

(c) Kwa kila "mwanafunzi" (msaidizi) enenda nao kwa angalau majuma matatu(93). Juma la kwanza ,fanya mfano wa njia, kwa kuongoza kikundi wewe mwenyewe. Juma la pili uache mwanafunzi wako aongoze kikundi kwa usaidizi wako. Juma la tatu angalia tu na ushiriki fafanusi ushauri wako kwa mwanafunzi wako baada ya mkutano.

(d) Weka wakati wa taratibu kila Juma kukutana na wanafunzi wako. Wakati huo, kila mtu asimulie kile kilifanyika katika mkutano uliopita- kile kilichofundishwa, maswali yoyote ambayo yaliyojitokeza, mahitaji ya maombi (kwa kanisa kufikiri na kushughulikia). Halafu gawanya ukurasa wa chakula wa mkutano kwa Juma lijalo, na ujadili fungu na maswali. Waombee wanafunzi na mahitaji ya kikundi.

**4. UZAZI**

(a) Mtie moyo mwanafunzi wako (msaidizi) kumchagua msaidizi mwingine ndani ya kikundi kusaidia kuongoza mikutano ya kikundi.

(b) Watie moyo watu katika kikundi waje na jamaa, marafiki na majirani katika mikutano ya kikundi.

(c) Kifanye kikundi kielewe kuwa kikundi kinapokua kutoka watu kumi na mbili hadi kumi na sita wale wanafika kila wakati, itakuwa wakati wa kugawanya kikundi hiki viwe viwili. "Msaidizi" mpya atakuwa yuko tayari kuongoza mojawapo wa vikundi hivi viwili. Kila kiongozi achague msaidizi mpya ili uanafunzi uweze kuendelea.

 ©2005 e3 Partners Ministry 

**KIFAA**

# MANUFAA YA KUANZISHA KANISA JIPYA

Kwanza lazima tujibu maswali ambayo kila mchungaji huuliza, kwanza, kwa nini kuanzisha kanisa jipya, kwa nini tusikuze kanisa letu wenyewe?

Ndiyo Mungu anataka kanisa lenu lililoko likue! kila kanisa lenye afya huendelea kukua. Lakini lengo hili lenyewe halijakamilika. Kuna kama sababu 7 za kibiblia, sababu za kutayarisha mikakati kwa kanisa la eneo fulani kuweza kuanzisha makanisa mapya, kuliko tu kuendelea kupanuka.

**1. NI UTARATIBU WA MUNGU. Mungu ana maono, na kanisa ni kifaa chake cha kutimiza au kufikia maono hayo!**

- "Nitajenga kanisa langu,"Yesu kasema" msemo mkuu katika Mathayo 16:18
- Mpangilio wa habari ya kanisa la mwanzoni katika kitabu cha Matendo ya Mitume yaonyesha wazi kwamba mitume na waumini walitii na kufuata maagizo ya Yesu kwa kuhubiri Injili na kukusanyika pamoja ndani ya makanisa mapya ya mahali pale pale.
- Ingawa nyaraka kwa hakika zinafundisha watu binafsi jinsi ya kuishi maisha ya kikristo, karibu nyaraka hizi zote zimeandikiwa makanisa.

**2. MUKTADHA WA KITAMADUNI.**

- Makanisa mapya lazima yaambatane na utamaduni wa mahali pale pale. Hii inatimizwa vizuri kama yameanzishwa na makanisa yalioko ndani ya utamaduni huo.
- Makanisa mapya yanayoshiriki utamaduni wa mahali pale na lugha, yana nguvu zaidi na yanafaulu katika uinjilisti na ujenzi wa kanisa kuliko yale yaliyozinduliwa kutoka nje.
- Makanisa mapya yaliyojengwa na makanisa yaliyoko, kwa kawaida yanarithi maono ya kujizidisha kwa kuanzisha makanisa mapya.

**3. Inaunga LENGO LA KUFIKIA WATU kwa ajili ya kanisa lililopo.**

- Makanisa mengi yalioko yanalenga mahitaji yao wenyewe na huduma. Lakini Yesu atuita "kufungua macho yetu tuyatazame mashamba yamekwisha kuwa tayari kwa mavuno *(Yohana 4:35)*.
- Yesu alitoa kielelezo cha huduma ya kuendelea kutoka mbinguni na kuendelea kuzuru miji yote na vijiji *(Luka 4:43, Mathayo 9:35)*
- Lengo la kufikia watu linasaidia kuzuia hali ya kukwama katika makanisa yaliyoko.
- Lengo la kufikia watu linainua hadhi ya uhamasisho wa waumini katika makanisa yaliyopo.

**4. Ni njia moja nzuri ya KUTAMBUA NA KUWAKUZA VIONGOZI WAPYA**

- Makanisa mapya yatoa namna ya kipekee katika kufunza viongozi wapya wa kanisa kazi, na wanaendelea kukomaa. Kwa kawaida viongozi wachanga na walio na uwezo wa kuwa viongozi, hawapewi majukumu ya kutosha kuongoza na kukua kanisani mwao. Makanisa mapya huwatolea nafasi ya kuendelea, na nafasi ya kukua na kupanua huduma zao.
- Wakati makanisa mapya yameanzishwa na makanisa yaliyoko, viongozi, wapya hunufaika kwa usaidizi, kutiwa moyo na mwelekeo wa viongozi wenye ujuzi kwenye kanisa zazi.

**5. Ni njia moja madhubuti na ya kufaa KUBADILISHA JAMII na kufanya uinjilisti Ulimwenguni.**

- Paulo anatangaza katika 2 wakorintho 5:17 "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya ya kale yamepita tazama yote yamekuwa mapya!"

## Hatua za Kwanza

 ©2005 e3 Partners Ministry 

- Jamii zinazozunguka makanisa mapya zinabadilishwa wakati “viumbe vipya” vinatii Tume kuu ya Kristo ya kuwafanya wanafunzi wapya na kuanzisha makanisa mapya zaidi.
- “Viumbe vipya” vya Mungu ni chumvi ya dunia (Mathayo 5:13), mmeitwa kusaidia na kukutana na mahitaji ya jamii kupitia elimu, utunzaji wa kiafya, kuwatunza mayatima, kulisha maskini; kuwaweka huru waliodhulumiwa na kadhalika.

**6. Kutoa tunda la Kudumu linalotukuza Mungu.**

- Badala ya kuacha kila mkristo kutawanyika katika jamii, kuwakusanya pamoja ndani ya kanisa jipya la eneo fulani, husaidia kuendeleza huduma na kuzaa tunda linalodumu.
- Makanisa mapya yanaendelea kukua jinsi yanavyoendelea kutunzwa na makanisa mama.
- Ufuasi unaoendelea wa waumini wapya na waumini wanaokomaa katika makanisa mapya yaliyoanzishwa yawezesha tunda la roho kubaki.

**7. Ni utaratibu wa kuzindisha na kuendeleza ndani ya kanisa linalojiendesha lenyewe katika mfumo wa kuanzisha makanisa.**

- Maelfu ya majirani kwenye miji na vijiji bado hawajawa na ushahidi wa kiuinjilisti, au kufikiwa na injili.
- Kwa sababu ya upungufu wa usafiri, lazima wapelekewe kanisa hatuwezi kuwangojea wapate njia yao kwenda katika kanisa la mahali fulani.
- Lazima tuzindishe mwendo wa upandaji au uanzishaji wa makanisa mapya ndani ya maeneo haya, chini ya uongozi mkuu wa Mungu, utoaji (mali) na mwongozo.
- Upanuzi huu si lazima ungojee ujenzi wa majengo mapya ya makanisa.

# KUANZISHA KANISA LA KIMSINGI

**KIFAA**

**JE, UNA NIA YA KUANISHA KANISA LA KIMSINGI?**

- Waumini wawili au watatu wanaweza kuanza kwa kuwaleta marafiki au jamaa pamoja, hata wale bado hawajaamini kwa ajili ya sherehe au ushirika (kama karamu, chakula cha mchana, kiamsha kinywa n.k.). Mkristo binafsi anaweza kuanza hivi na wale ambao hawajaamini, na kufanya kanisa la kimsingi, watu binafsi wanapomgeukia Kristo.
- Ongezea vile vitu vingine vya kiasili punde tu au pole, pole, kimoja hadi kingine (kama unavyohitaji) kwa kufuata mpangilio, uliopo hapo chini, kwa mwendo unaofaa kwa kikundi hicho.
- Waumini wanahitajika kwa ajili ya ubatizo na meza ya Bwana. (#5) kufikia mahali hapo wingi wa washiriki huenda wakawa wale wanaotafuta tu.
- Tafuta kushiriki uongozi baina ya washiriki, mnapokutana (kama kushirikiana,kusoma Biblia, kuomba n.k.) Washiriki wanapoamua kumfuata Kristo, waweza kumwuliza mtu mwingine akusaidie kuichunga kundi hilo, lakini sio jambo la muhimu / maanani hapo mwanzoni.
- Wakati ambapo kiini cha kikundi fulani kimeamua kumfuata Kristo na mmeshaanza kutenda kazi kama mwili wa Krsito kwa kuhudumiana na kuwafikia wale waliopotea, basi mmeshakuwa kanisa la kimsingi lililoimarika, na yafaa muombe na kutenda kuelekea kuanzisha makundi mengine.
- Wingi wa makundi hayo yafaa yazae makanisa mapya ya kimsingi wanapofikia idadi ya watu sita hadi 8 ambao wanashiriki kila mara bila kukoma. Ni vyema zaidi kuruhusu watu wawili au watatu kuwa timu ya kuanzisha kikundi kipya. Umuhimu wa vikundi vidogo ni urafiki wa ndani, na ushirika wa karibu, lakini huweza kupotea katika vikundi vinavyozidi watu wanane (8).

**1. KUENI NA USHIRIKA**

Njia moja ni kuzungumza na kustarehe mnapo kula. Panga shughuli yoyote ambapo marafiki na jamaa zako watahusika/shwa na kupata wepesi wa kuongea. Fanya matayarisho ya vyakula au vinywaji kuwa rahisi ikiwa hamkutani kwenye mkahawa / hoteli fulani. Baada ya mkutano wa kwanza shirikianeni kuhusu ununuzi wa bidhaa au majukumu ya maandalizi. Fanya mazoezi ya maandiko katika Agano Jipya" yanayohusu mmoja kwa mwingine," au kanisa kama " mwili wenye uzima" jinsi inavyoelezwa katika Wakorintho wa kwanza Milango ya 12 hadi 13, na pia kwenye mlango wa kumi na nne,kifungu cha ishirini na sita (14:26)

**2. SIKIZENI NENO**

Tangulia na mafumbo na hadithi za Kristo. Ikiwa washiriki wanao mtazamo wa kidunia/ kiulimwengu usiotoa maana yoyote, au pengine ufahamu uliopotoka uliopofoka wa maneneo kama "Mungu", "takatifu", "dhambi" , "adhabu inayostahili", " ukombozi", wokovu, mbingu " na hukumu". Basi itakubidi uweze kuweka msingi wa mawazo/maneno haya kwa kuanza na hadithi za kimsingi kwenye Agano la kale. Soma au hadithia kwa hisia na kumaanisha, kutoka kwa Biblia.

Kwa wale wanaoanza, hadithia hadithi zinazolenga amri Saba za kimsingi za Kristo (zilizoorodheshwa hapo chini). Fanya hili punde tu waumini wapya au wanaotafuta, Wanapoweza kuelewa umuhimi wake. Wakati watu wageni/wapya wanapo kuwa waumini baadaye, mwulize, mtu mmoja ajifunze amri za Yesu pamoja nao kwa wakati usio wa kawaida kukutana, ili wanakikundi (washiriki) wasichoshwe na marudio yasiyobadilika.

Wakati ambapo hicho kikundi kinakomaa, mnaweza kijiifunza kutoka kwa moja au zaidi ya vitabu vya injili, baadaye kwenye nyaraka au vitabu vinginevyo vya Bibila; ukijumlisha na vifungu ambavyo sio hadithi.

**Tumia maswali kujadili/kujifunza Biblia. Wengine huyapata maswali haya kuwa ya msaada/muhimu.**

1. Je ni kitu gani ulichokifurahia sana kuhusu hiyo hadithi au kifungu cha Biblia?
2. Na, ni kitu gani ambacho hukuelewa?
3. Je,ni kitu gani tunaweza kujifunza kutoka kwa kifungu hicho kuhusu asili na mahitaji ya watu?
4. Je, twaweza kujifunza nini kumhusu Mungu kutoka kwa kifungu hicho (Mungu baba, Yesu mwanawe, na Roho mtakatifu)?
5. Je,. Wewe binafsi ulijifunza nini kuhusu jinsi Mungu anavyokutaka wewe kuishi?

**3. MBENI**

Mwombeane wenyewe kwa wenyewe. Muwaombee hasa marafiki na jamma ambao hawajamwamini Yesu. Kila mtu anaweza kutoa au kupeana haja za maombi kuombewa na wengine kuwaonbea. Mara nyingi wale ambao sio wakristo wanaguzwa kiroho kwa kuwa na mtu wa kuwaombea.

**4. MSIFUNI MUNGU**

Kama ratiba/,au mpagilio au hali, inaruhusu, mwimbieni Mungu sifa. Labda mtu mmoja anaweza kufuata uimbaji huo kwa kinanda au,ngita (zeze) au chombo kinginecho cha musiki . Ikiwa hakuna mcheza, vyombo (awezaye kucheza vyombo), mwaweza kuimba pamoja na chombo cha kucheza CD.

 ©2005 e3 Partners Ministry 

Katika hali /mipangilio mingine, ni vyema (ni jambo la hekima), kumsifu Mungu polepole/taratibu, bila kutumia muziki. Mnaweza kusoma zaburi, tenzi, kutoa ushuhuda, kumsifu Mungu kwa ajili ya mojawapo au zaidi ya tabia zake kuu na za kipekee (mwenye msamaha, mwenye nguvu, mtakatifu, mwenye huruma n.k) soma shairi n.k.

**5. Kusherehekea Ubatizo na meza ya Bwana**

Waumini wapya wanastahili kubatizwa haraka iwezekanavyo kama hatua ya kwanza hadharani katika maisha ya kumfuata Kristo, na pia kama kukiri kwa ishara inayoonekana wazi, kuhusu imani yao. Kikamilifu, ubatizo wahitajika kufanywa na mtu au watu waliohusika sana katika kumwongoza mwumini mpya kwa Kristo. Mamlaka ya kubatiza ni (sehemu) ya ile Tume kuu, iliyotolewa na Yesu kwa wafuasi wake wote, katika Mathayo 28:18-20

Mnaweza kuandaa meza ya Bwana kwa kila mkutano na pasipo kufuatana kwa karibu ikiwa kikundi hicho kitapendelea hivyo. Uwe mwepesi kuhisi hisia za wasioamini ambao labda watakuwa wakihudhuria. Ifanye iwe rahisi. Fikiria kuhusu kuandaa meza ya Bwana baada ya chakula chenu na wakati wa kushirikiana mwanzoni mwa mkutano. Hakuna haja ya mahubiri au mafundisho kabla yake. Epukana na maelezo marefu ya zile ishara. Eleza tu kwa urahisi kuwa Yesu alitwambia kuwa tule na tunywe kwa ukumbusho wa kifo chake msalabni. Wacha fubo hilo lisimame.

**6. Wakati ambapo kundi hilo limeimarika wafundishe kutoa kwa ukarimu na kwa uchangamfu kwa kumtii Yesu.**

Msikusanye mafungu ya kumi na sadaka hadharani hadi kundi hili liwe tayari kutii amri hii ya kristo. Kisha kwa uangalifu:

- Ruhusu kikundi hicho kiamue jinsi matumizi yatakavyohudumiwa, na kuhakikisha kuwa munafuatilia mahitaji kamili. Tumia sadaka kwa ajili ya shughuli za kanisa la kimsingi. (ushirikiano, uinjilisti, mafunzo) mahitaji ya watu unaohudumia, huduma au makanisa ambayo kwa namna fulani wanasaidia au husaidia kanisa lenu la kimsingi.
- Kupitisha kikapu au mfuko wa kukusanya sadaka huenda ikawa ya kufedhehesha kwa kikundi kidogo. Yaweza kuwa kwazo kwa wageni. Weka sanduku au kikapu rahisi katika pahali mnapokutania na kufundisha waumini kupeleka sadaka zao hapo.

**Mambo ya kukumbuka**


- Ikiwezekana, msikutane kila wakati kwa nyumba ya kiongozi au mwumini mkomavu ni vema kukutana kwa nyumba au mahali palipopangwa na waumini wapya au wanaotafuta kujua.
- Ni vyema zaidi ikiwa waumini wakomavu wanawatia moyo waumini wapya na watafutao, kuwaalika jamaa, marafiki, wafanya kazi wenzi au majirani.
- Waumini wakomavu wanastahili kuwa waangalifu kwa kuongea machache na kusikiza zaidi, ili kuwaaruhusu waumini wachanga kukua katika kikundi hicho. Uepo wa waumini wakomavu au viongozi labda unaweza kutatanisha vikundi vingine. Katika hali kama hizo, waumini wachanga wanafaa kuongoza mkutano, wakipokea mashauri na himizo katika vipindi vya mafunzo pamoja na kiongozi au mwumini mkomavu kwa wakati mwingine.
- Ifanye kuwa rahisi. Tenda kila kitu kwa njia ambayo watu katika kikundi hicho wataiga kwa urahisi na kurudia wenyewe wakati wataanzisha makundi mapya. Waulize wengine kuongoza badala ya kumtazamia kiongozi mmoja wiki baada ya wiki. Hata wasio wakristo wanaweza kuongoza nyakati za kustarehe na kushirikiana. Wafundishe kando pasipo kujulikana.
- Fanya hali iwe ya kawaida. Munaweza kutana nyumbani (mkahawa au katika afisi wakati wa mapunziko ya chakula cha mchana).
- Wakati wa mkutano msiweke nia zenu kwa mtu mmoja (atafutaye au mwumini mpya). Ni vyema kundi lote liwadilike na kumsaidia kila moja kuhusika kwa jinsi fulani.

**Amri saba (7) za kimsingi za Kristo,na hadithi ambazo Zinazozihusu:**

1. **Tubuni , amini na kupokea Roho mtakatifu** (Mariko 1:15; Yohana 20:21-23) **Hadithi:** Mwana mpotevu, Luka 15:11-32 Mazungumzo ya Yesu na Nikodemo, Yohana 3;1-17; Kuamini kwa Paulo, Matendo 9:1-31
2. **Batizeni** (Mathayo 28:18-20) H**adithi:** ubatizo wa Yesu, Mathayo 3; Amri ya Yesu ya kubatiza, Mathayo 28:18-20(yule) mlinzi wa jela na jamii yake Matendo 16:16-34
3. **Mega mkate (Meza ya Bwana) kwa ajili ya kumbukumbu ya kifo cha Yesu** (Mathayo 26:26-28) H**adithi:** ile karamu ya pasaka ya asili Kutoka 12; Yesu anautoa mwili wake uliwe na kuwaudhi Wafuasi wake, Yohana 6:24-63.
4. **Mpende Mungu, watu wengine, samehe maadui n.k. (Mathayo 22:33-40; Luka 6:27-33)** **Hadithi:** msamaria mwema. Luka 10:25-42; Upendo wa Ruthu kwa mama-mkwe wake aitwaye Naomi, Ruthu 1
5. **Ombeni** (Yohana 16:24) **Hadithi**: Maombi ya Ibrahimu kwa jamii ya Lutu, Mwanzo 18:20-33, Maombi ya mtoza ushuru, Luka 18:9-14
6. **Toa kwa Ukarimu** (Luka 6:38) H**adithi:** Abigaili awalisha askari wa Daudi walio kuwa na njaa. 1 Samuel 25: (Tabitha awatengenezea mavazi walio maskini, Matendo 9:36 -43; Baranaba auza shamba lake kuwapa maskini ( walio na mahitaji), Matendo 4:32-37)
7. **Wafanyeni Wanafunzi** (Mathayo28:18-20) **Hadithi**: Yesu awachagua wale kumi na wawili Kumfuata, Mariko 3:13-19; Mitume wafundisha waumini katika kanisa la kwanza huko Yerusalem, kuzitii amri za kimsingi za Yesu, matendo 2:37-47; Prisila na Akwila wanafunza kiongozi Apolo, Matndo 18:24-28

Kifaa hiki, kinatoka kwa huduma iitwayo “Impact Japan” mnaweza kuwafikia katika mtandao wa : mail@impactjapan.org . Hii nakala yaweza kutolewa kwenye mtandao wa *www.hereshope.com/tools*

 ©2005 e3 Partners Ministry 




## Hatua za Kwanza



**KUZENI VIONGOZI**



# KUZENI VIONGOZI

**MAWAZO MAKUU**

- Kunayo heshima (faida) na majukumu mengi ya viongozi wa kiroho.
- Tunataka kukuza viongozi wa kiutumishi kama Yesu.
- Unalo hitaji muhimu kutambua na kukuza viongozi wa kiutumishi wa siku za usoni.
- Changamoto yako ya kwanza ni kushauri viongozi wapya kwa kuwahusisha kwenye timu za huduma.

## 1. FUMBO LA MAVUNO: KUZENI VIONGOZI

Wakati ukiwa sawa, mkulima huenda shambani na kukusanya matunda ya mavuno yake na kuyapeleka katika ghala lake. Pale, hukusanya mbegu mpya kwa msimu ujao wa upanzi-mbegu zaidi kuliko alizozianzia, kwa hivyo mavuno yake huongezeka kila mwaka.

Mavuno yakiwa zaidi, ndivyo watendakazi zaidi wanahitajika. Kwa bahati zuri, wale watendakazi wa ziada wamo mavunoni,waumini wapya wa leo wanakua katika kristo kupitia ufuasi . Wanaendelea kukua na kuhitimu kuwa/watendakazi viongozi na wachunagaji kupitia ushauri.

Viongozi wazuri hawatukii tu. Huitwa na Mungu, ndiyo, lakini hawawezii kutimiza mwito wao wa ajabu mpaka wapate mafunzo.

Mwendo wa kuanzisha kanisa hautawahi pita hitaji lake la viongozi wapya, ambao wametambuliwa na kupewa mafunzo na viongozi waliopo. Mafunzo ya uongozi, ni mojawapo ya changamoto muhimu sana katika kuanzisha makanisa mapya.

## 2. VIONGOZI WA KILIMWENGU –VIONGOZI (WA KIUNGU)

**Soma Mathayo 20:25-28**

[25]Lakini Yesu akawaita, akasema mwajua ya kuwa wakuu wa mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. [26]lakini haitakuwa hivyo kwenu, bali mtu yeyote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu, [27]na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu, [28] kama vile mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na, kutoa nafisi yake iwe fidia ya wengi”

**2.1 Ni viongozi wawili wa aina gani Yesu anaelezea hapa?**

Viongozi wa kidunia ambao Yesu anawaeleza kama “watawala wa mataifa,” huwatawala watu kutoka juu. Ni wa majivuno, walio mbali na watu na ambao hupendezwa sana katika kutumia mamlaka yao, huwatawala watu kwa mkono wa chuma. Katika kielelezo cha dunia, viongozi wapo juu na wenye kuongozwa chini.

Uongozi wa ufalme (wa Mungu) ni kinyume. Yesu kiongozi wa viongozi ndiye msingi yaani kitako cha uongozi wa Ufalme. Husaidia na kumwinua yeyote yule. “Serikali ipo begani mwake” Isaya 9:6.Yeye ni yule kiongozi mtumishi na yeye ndiye atakuwa kielelezo chetu cha uongozi.

**Soma 3 Yohana 9-10**
9 Naliliandikia kanisa neno, lakini diotrefe apendaye kuwa wa kwanza kati yao
hatukubali 10 Kwa hiyo, nikija nitayakumbuka matendo yake atendayo, atoavyo upuzi juu yetu kwa maneno maovu; wala hatoshwi na hayo, ila yeye mwenyewe hawakaribishi hao ndugu na wale watakao kuwakaribisha, huwazuia na kuwatoa katika kanisa.

**2.2 Diotrefe alikuwa kiongozi wa aina gani?**

Diotrefe alikuwa wa kutawala, akitumia uzoefu wa mkazo wa juu ya watu. Alikuwa wa majivuno. Alipenda kuwa wa kwanza na kutaka kuwa na chochote kuhusu viongozi wakristo wengine.

Ubaya zaidi alikuwa mdaku wa kudhuru. Alieneza habari tu ambayo haikuwa shughuli yake, na alipanda masingizio kwa faida yake mwenyewe.

Hakuwaongoza watu, aliwaendesha. Hakuwa mbele yao na gongo mkononi mwake, alikuwa nyuma yao na mjeledi.

Aliongozwa na tamaa ya makuu siyo Roho mtakatifu, na kwa hivyo alihukumiwa kuangamia.

Hatutaki kuwa kiongozi kama Diotrefe, je, twataka? Wala hatutaki kuzalisha viongozi wapya kama yeye?

Kwa kinyume, katika usiku wake wa mwisho kabla ya kusulubiwa, alilipa kanisa lake kielelezo wazi cha kiongozi mtumishi.

Mtu ambaye anajua yu karibu kufariki huchagua maneno yake ya mwisho kwa makini sana huongea kuhusu vitu vilivyo vizito kwenye moyo wake na ya juu zaidi katika mawazo yake. Hebu tutazame maneno hayo.

**Soma Yahana 13:1-7 tena**
[1] Basi kabla ya sikukuu ya Pasaka, Yesu hali akijua ya kuwa saa yake imefika, atakayotoka katika ulimwengu kwenda kwa Baba, naye ali amewapenda watu wake katika ulimwengu, aliwapenda upeo. [2] Hata wakati wa chakula cha jioni, naye ibilisi amekwisha kumtia Yuda mwana wa Simoni Iskariote, moyo wa kumsaliti . [3] Yesu hali akijua ya kuwa Baba amempa vyote mkononi mwake na ya kuwa alitoka kwa Mungu naye anakwenda kwa Mungu , [4] aliondoka chakulani, akaweka kando mavazi yake, akatwaa kitambaa, akajifunga kiunoni [5] Kisha akatia maji katika bakuli, akanza kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga [6] Hivyo yuaja kwa Simoni Petro . Huyo akamwambia "Bwana! wewe wanitawadha miguu mimi? [7]Yesu akajibu akamwambia "Nifanyalo wewe hujui sasa lakini utalifahamu baadaye" . [8] akamwambia, "Wewe hunitawadha miguu kamwe "Yesu akamwambia " kama nisipokutawadha huna shirika nami "[9] Simoni Petro akamwambia Bwana si miguu yangu tu, hata na mikono yangu na kichwa changu pia . [10] "Yesu akamwambia " aliyekwisha kuoga hana haja ila ya kutawadha miguu bali yu safi mwili wote , nanyi mmekuwa safi lakini si nyote . [11] Kwa maana alimjua yeye atakaye msaliti ndiyo maana alisema , si nyote mlio safi .[12] Basi alipokwisha kuwatawadha miguu na kuyatwaa mavazi yake na kuketi tena , akawambia ,"Je mmeelewa na hayo niliyowatendea ? [13] Nyinyi mwaniita mwalimu, na Bwana nanyi mwanena vema maana ndivyo nilivyo. [14] Basi ikiwa mimi nimewatawadha miguu imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi [15]kwa kuwa nimewapa kielelezo, ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo [16] Amini, Amini nawaambia ninyi mtumwa si mkuu kuliko Bwana wake wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka. [17] mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda.

**2.3 Yesu alifanya nini kuwasaidia wanafunzi wake kujifunza juu ya uongozi wa kiutumishi?**

Mbele ya macho yao yaliyo stajabishwa Masihi aliyeahidiwa alijigeuza mwenyewe kuwa kama mfano wa watumwa wa kiwango cha chini sana. Halafu akatekeleza kazi ya kiwango cha chini ifanywayo na mtumwa, yaani kunawisha miguu michafu ya watu.

Aliwapa picha ambayo itakaa nao maisha yao yote, licha ya hali za kuogofya ambazo wao walikuwa karibu kushuhudia.

Ilikuwa imemzidi Petero. Miguu yake ilikuwa migumu michafu, na iliyotoa harufu mbaya ya samaki. Na yeye alikuwa nani ya kuwa mtu ambaye Baba alikuwa amejifunua kibinafsi kwa mvuvi, kama Mwana wa Mungu angefanya kazi kama hii?

Imetuzidi sisi wengine pia tunapokumbuka ya kuwa Yesu pia alinawisha miguu ya Yuda msaliti.

Hasa hii, ilikuwa mfano mtamu wa upendo wake mpole kwetu.Alijua ya kwamba mara tupitapo fedheha ya kumuona Yesu akinawisha miguu, ingekuwa rahisi kidogo kwetu kufanya kitu kama hichohicho. Hilo ndilo lilikuwa jambo haswa. Ni kitu kimoja "kujua mambo haya." Lakini Yesu anasema, "mmebarikiwa mkiyafanya haya!"

## Hatua za Kwanza

## 3. BARANABA NA SAULI: KUZIDISHA KWA KUSHAURI

Paulo alikuwa kiongozi mkristo mkuu. Hebu tutazame mmoja wapo wa wanaume Mungu alitumia kumkuza Paulo kuingia katika uongozi- Baranaba.

**Soma Matendo ya Mitume 4: 36-37**
36 Na Yusufu aliyeitwa na mitume Barnaba (maana yake mwana wa faraja), mlawi
asili yake, ni mtu wa kipro, 37 alikuwa na shamba akaliuza, akaileta fedha, akaiweka
miguuni pa mitume.

**Soma matendo ya Mitume 11: 22-24**
22 Habari hizo za watu hao zikafika masikioni mwa kanisa lililokuwa katika
Yerusalemu wakamtuma Baranaba, aende hata Antiokia. Naye, alipokwisha kufika
na kuiona neema ya Mungu akafurahi, akawasihi wote waambatane na Bwana kwa
kusudi la moyo. 24 Maana alikuwa mtu mwema amejaa Roho Mtakatifu na imani
watu wengi wakaongezeka upande wa Bwana.

### 3.1 Barnaba alikuwa kiongozi wa aina gani?

Baranaba alikuwa mfariji, mwanaume ambaye aliona yaliyowezekana katika watu na aliwasaidia kuyafikia. Uangalifu wake ulikuwa kwa wengine, siyo kwake mwenyewe.

Bidii yake ilikuwa juu ya kuwasaidia wengine wafurahi si kwa yeye kufaulu. Baranaba alikuwa mkarimu. Tena, alipenda kuwatunza wengine kuliko yeye mwenyewe kwa furaha na bila kulazimishwa alitoa kile kilikuwa cha haki kwake kusaidia kukutana na mahitaji ya wengine.

Hakuwa kiongozi mchoyo. Aliwatia moyo watu wengine. Aliliuza shamba lake na kulipeana kama toleo kwa kanisa.

Yose katika kiyunani ni Yosefu, maana yake "Yehova aniongezee." Lakini mitume waliona ya kwamba tabia yake kweli haikuwa upande wa kupokea kutoka kwa Mungu. Ilikuwa imetengwa kwa ajili ya kuwainua wengine. Kwa hivyo wakabadilisha jina lake kuambatana na asili yake.

Inasemekana kweli kwamba "unafunza kile unacho jua, lakini una zaa namna yako"

Hatua ya kwanza katika kuwashauri viongozi wapya ni kuwa imara, kiongozi wa kiungu, kiongozi afananaye na Kristo yeye mwenyewe.


©2005 e3 Partners Ministry

**Hatua za kwanza**

**Nani aliye muhimu sana maishani mwako? Wewe? Au Mungu na wanafunzi wako? Mabadiliko gani unahitaji kufanya ili uwe mshauri bora kwa viongozi wapya?**
*Tazama swali la ishirini na moja (21) ya mkakati wa utendaji kazi.*
.

**Soma Matendo 9:26-28**
26 Na sauli alipofika Yerusalemu alijaribu kujiunga na wanafunzi, nao walikuwa
waki mwogopa wote , wasisadiki ya kuwa yeye ni mwanafunzi. 27 Lakini Barnaba
akamtwaa, akampeleka kwa mitume, akawaeleza jinsi alivyomwona Bwana njiani
na ya kwamba alisema naye, na jinsi alivyohubiri kwa ushujaa katika Dameski kwa
jina la Yesu. 28 Naye akawa pamoja nao katika Yerusalemu akiingia na kutoka.

**3.2 Barnaba alimsaidiaje sauli?**

Wakristo walimwogopa Sauli, mtesaji. Waliposikia ya kuwa amemwamini Kristo kama mwokozi wake, hawakuiamini habari hiyo. Walifikiri ulikuwa mtego hodari kuwavuta nje na kuwakamata.

Lakini Baranaba aliona ushahidi wa kile Mungu alikuwa ametenda ndani ya Sauli akasawishi viongozi wengine kukubali ndugu yao mpya. Barnaba akawa mtetezi wa Sauli.

**Soma Matendo ya mitume 11:25-30**
25 Kisha akatoka akaenda Tarso kumtafuta Sauli, 26 hata alipokwisha kumwona na
kumleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na
kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa wakristo kwanza hapo
Antiokia. 27 Siku hizo hizo manabii walitelemka kutoka Yerusalemu hata Antiokia.
28 Na tulipokusanyika akasimama mmoja wao, Jina lake Agabo, akaonyesha kwa
uwezo wa Roho Mtakatifu kwamba njaa kubwa itakuja karibu katika dunia nzima,
nayo ikatukia katika siku za Klaudio. 29 Na wale wanafunzi kila mtu kwa kadiri ya
alivyo fanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi.
30 Wakafanya hivyo, wakawapelekea wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli.

 ©2005 e3 Partners Ministry 

### 3.3. Barnabas alimsaidiaje Sauli kukua kama kingozi?

Mara tu Barnaba alipopewa wajibu wa uongozi katika kanisa jipya, alimwandikisha Sauli. Huku akifanya kazi bega kwa bega na Barnaba, Sauli alijifundisha jinsi ya kuhudumia waumini. Barnaba alimpa Sauli fursa za kuhudumu. Alimpa Sauli wajibu zaidi ili akue kama kingozi.

Timu hii ya huduma ilikuwa na kishindo kikubwa mno katika jiji la Antokia. Watu waliona mabadiliko hayo ya ajabu katika maisha ya waumini na kuwataja au kuwaita "Wakristo," inayomaanisha "Kristo wadogo."

**Hatua za kwanza**

**Wewe utamtetea nani kama kiongozi mpya?**
**Ni wakina nani utakaokaribisha?**
**Kama watu walio na uwezo wa kuwa viongozi wapya ili kusaidia kuanzisha kanisa jipya?**
*Tazama swali la 22 katika mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

**Soma Matendo ya mitume 13:1-7**
1 Na huko Antiokia katika kanisa lililokuwako palikuwa na manabiii na walimu, nao
ni Barnaba na Simioni aitwaye, Nigeri, na Lukio Mkirene, na Manaeni aliyekuwa
ndugu wa kunyonya wa mfalme Herode, na Sauli. 2 Basi hawa walipokuwa
wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho mtakatifu akasema, Nitengeeni
**Barnaba na Sauli** kwa kazi ile niliyowaitia. 3Ndipo wakiisha kufunga na kuomba,
wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao. 4Basi watu hao, wakiisha
kupelekwa na Roho Mtakatifu wakatelemkia Seleukia, na kutoka huko, wakasafiri
baharini hata Kipro. 5Na walipokuwa katika Salami wakalihubiri neno la Mungu
katika masinagogi ya Wayahudi, nao walikuwa naye Yohana kuwa mtumishi wao.
6Walipokwisha kupita katikati ya kisiwa chote mpaka Pafo, wakaona mtu mmoja
mchawi, nabii wa uongo, Myahudi jina lake Bar-Yesu, 7Mtu huyo alikuwa pamoja na
liwali Sergio Paulo, mtu mwenye akili. Yeye liwali akawaita **Barnaba na Sauli** waje
kwake, akataka kulisikia neno la Mungu.

### 3.4 Kulikuwa na uhusiano gani kati ya Barnaba na Sauli?

Maandiko yataja hawa wawili pamoja kama timu. Waliitwa na Mungu kama timu, wakatenganishwa kutoka kwa viongozi wengine kama timu, wakatumwa nje kama timu, na wakafanya kazi pamoja.

Angalia pia kwamba Barnaba anaorodheshwa kwanza kama kiongozi wa timu. Lakini hayo yote yanakaribia kubadilika.

## Hatua za Kwanza

**Soma Matendo 13:8-16**
**8**Lakini Elima yule mchawi (maana ndiyo tafsiri ya jina lake) akashindana nao
akitaka kumtiaYule liwali moyo wa kuiacha ile imani. **9**Lakini **Sauli, ambaye ndiye
Paulo,** akijaa Roho Mtakatifu, akamkazia macho, **10**Akasema Ewe mwenye kujaa
hila na uovu wote ,mwana wa ibilisi ,adui wa haki yote, huachi kuzipotoza njia za
Bwana zilizonyooka? **11**Basi ,angalia mkono wa Bwana u juu yako, nawe utakuwa
kipofu, usilione jua kwa muda, mara kiwi kikamwangukia na giza,
akazungukazunguka na kumtafuta mtu wa kumshika mkono na kumwongoza.
**12**Ndipo yule liwali, alipoyaona yaliyotendeka, akaamini, akiyastaajabia
mafundisho ya Bwana. **13**Kisha **Paulo na wenziwe** wakang'oa nanga wakasafiri
kutoka Pafo, wakafika Perge katika Pamfilia, Yohana akawaacha akarejea
Yerusalemu. **14**Lakini wao wakatoka Perge wakapita kati ya nchi wakafika
Antiokia, mji wa Pisidia, wakaingia Katika Sinagogi siku ya sabato
wakaketi.**15**Kisha baada ya kusomwa Torati na chuo cha manabii, wakuu wa
Sinagogi wakatuma mtu kwao, na kuwaambia, "Ndugu kama mkiwa na neno la
kuwafaa watu hawa lisemeni. **16****Paulo akasimama** akawapungia mkono, akasema,
Enyi waume wa Israeli nanyi mnaomcha Mungu sikilizeni!"(mkazo umeongezewa)

### 3.5 Mabadiliko gani yanayotendeka?

Kwanza jina la Sauli lilibadilishwa kuwa Paulo. Basi hilo si jambo lisilo la kawaida, kama iliviyo hata leo kwenye tamaduni nyingine kubadilisha jina la mtu anapokuwa mkristo. Jina La Kiyahudi Sauli lamaanisha ilioulizwa "Huku" akiwa ameitwa na Mungu, Sauli aliulizwa na Barnaba. Jina lake la Kirumi Paulo yamaanisha "Mdogo" na wanahistoria wengine wapendekeza kwamba mnabii mkuu(Paulo) alitaka kujulikana kama "aliye mdogo."

Mabadiliko ya pili yalikuwa ya kicheo . Sasa Paulo na si Barnaba, ni mnenaji mkuu. Pia ni wa maana zaidi katika huduma. Fungu la 13 sasa linataja timu kama "Paulo na chama chake."

Paulo mwanafunzi anakuwa Paulo kiongozi .

**Soma Matendo ya mitume 13:43, 46, 49-52.**
43 Sinagogi ilipofumukana , Wayahudi na waongofu watauwa wengi
wakashikamana na **Paulo na Baranaba ambao**, wakisema nao wakawatia moyo
kudumu katika neema ya Mungu . 46 **Paulo na Baranaba** wakanena kwa ushujaa
wakasema, llikuwa lazima neno la Mungu linenwe kwenu kwanza, Lakini kwa
kuwa mnalisikumia mbali, na kujiona nafsi zenu kuwa hamkustahili uzima wa
milele angalieni, twawageukia mataifa. 49 Neno la Bwana likaenea katika nchi ile
yote. 50 Lakini Wayahudi wakawafitinisha wanawake watauwa wenye cheo na
wakuu wa mji wakawataharakisha watu wawaudhi **Paulo na Barnaba** wakawatoa
katika mipaka yao. 51 Nao wakawakungutia mavumbi ya miguu yao wakaenda
Ikonio. 52 Na wanafunzi walijaa furaha na Roho mtakatifu.

## Hatua za Kwanza

**3.6 Je Uhusiano gani uliopo baina ya Baranaba na Paulo sasa?**

Hali ya kuwa pamoja imebadilika tena . Sasa Paulo anajitokeza kuwa kiongozi. Na taratibu ya Luka inapoendelea, Baranaba pia anatoweka, tunafuata njia ya Paulo.

Paulo alianza kama mwanafunzi wa Baranaba. Hatimaye, na kwa vyovyote, mwanafunzi alimshinda mshauri wake. Hiyo ndiyo iliyo kuwa neema na tabia ya ukarimu wa Baranaba.Pasipokuhusika na cheo chake binafsi, Baranaba alitoa maisha yake kuupanua Ufalme wa Mungu.

**Hatua za kwanza**

**Je ungependa kuwashauri viongozi wapya walio na vipawa, pengine hata zaidi kuliko wewe?**
**Je ungependa kuwashauri sana ili wakushinde na wawe viongozi wanaofaa zaidi kuliko wewe?**
*Tazama swali la 23 la mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

**Soma Matendo 14:19-26**
19 Lakini Wayahudi wakafika toka Antiokia na Ikonio, wakawashawishi makutano
hata wakampiga kwa mawe Paulo, wakamburuta nje ya mji, wakidhania ya kuwa
amekwisha kufa. 20 Lakini wanafunzi walipokuwa wakimzunguka pande zote,
akasimama, akaingia ndani ya mji, na siku ya pili yake akatoka, akaenda zake
pamoja na Baranaba mpaka Derbe. 21 Hata walipokwisha kuihubiri Injili katika mji
ule, na kupata wanafunzi wengi wakarejea mpaka Listra na Ikonio na Antiokia.
22 Wakifanya imara roho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile imani na ya
kwamba imetupasa kuingia katika Ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi.
23 Na Walipokwisha kuwachagulia wazee katika kila kanisa na kuomba pamoja na
kufunga Wakawaweka katika mikono ya Bwana Waliyemwamini. 24 Wakapita kati
ya Pisidia wakaingia Pamfilia., 25 Na baada ya kuhubiri lile neno katika Perge,
Wakatelemka mpaka Atalia . 26 Na kutoka huko wakaabiri kwenda Antiokia, Huko
ndiko walikoombewa neema ya Mungu kwa ile kazi waliyokwisha kuitimiza.

**3.7 Je Mungu alitumiaje timu hii ya watu?**

Bwana aliwasilisha Paulo na Baranaba kama kielelezo chenye nguvu cha kuanzisha makanisa mapya ambayo yanaleta utukufu mkuu kwa Baba yetu.Timu hii ya huduma:

- Iliomba na kufunga,
- Ilifanya uinjilisti kwa kuhubiri injili,
- Ilifanya wanafunzi wengi
- Ilikusanya waumini wapya katika makanisa mapya,
- Ilichagua wazee katika kila kanisa
- Ilizidisha makanisa wakati wamishenari walitumwa kutoka kanisa katika Antiokia.

Mtu mwingine aliwahi kusema, “hakuna mpaka kwa kile Mungu anaweza kutenda kupitia yeyote asiyejali ni nani atapata sifa njema au ni nani atasifiwa.”

## Hatua za Kwanza

**Hatua za kwanza**

**Je muna timu iliyo tayari kuanzisha kanisa jipya? Mnakuza viongozi wapya kwa kuwahusisha kwenye timu ya huduma yenu?**
*Tazama swali la (23) la mkakati wa ukurusa wa utendaji kazi.*

## 4. PAULO NA TIMOTHEO: KUZIDISHA KWA KUSHAURI (MENTORING)

**Soma 2 Timotheo 2: 2-6**
2 Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.
3 Ushiriki taabu pamoja nami kama askari mwema wa Kristo Yesu.
4 Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari.
5 Hata mtu akishindana katika michezo hapewi taji asiposhindana kwa halali.
6 Yampasa mkulima mwenye taabu ya kazi kuwa wa kwanza wa kupata fungu la matunda.

### 4.1 Paulo alimfundisha Timotheo nini kuhusu kuzidisha viongozi?

Kama, tulivyoona katika sura ya Fanyeni Wanafunzi, Paulo ataja vizazi vinne katika fungu hili. Paulo alimshauri Timotheo na akamtarajia Timotheo kuwashauri wengine.


Wokovu wako na wangu ni mzuri, bali hautoshi. Utatupeleka mbinguni, lakini hauwezi kumleta mtu yeyote mwingine pamoja nawe bila wewe kuwafikia wengine.

Sisi tuna wajibu, kuwa sehemu ya mnyororo wa wanafunzi, walioungana pamoja kupitia vizazi vingi.

Ikiwa wewe ni mwanafunzi wafundishe wengine kufundisha. Kama wewe ni kiongozi mtumishi wafundishe wengine kuongoza kwa kutumika na kuwafundisha wengine wanaoweza kuwa viongozi watumishi, yote kwa utukufu wa Mungu!

Kwenye sentensi moja tu, Paulo alikabidhi Timotheo ufunguo wa huduma ya kuzidisha. Hebu tutazame mchoro muhimu wa fungu hili tena (tazama ukurasa unaofuata).

Paulo pia alimwonya Timotheo kuwa, kuwakuza viongozi wapya haikuwa kazi rahisi kungekuwa na ugumu. Kungekuwa awe, na vipaumbele sawa na asijiruhusu kuvutiwa kimawazo na vitu vya kiulimwengu. Paulo alimtia changamoto Timotheo kukimbia “shindano la mbio” ya huduma kulingana na kanuni za Kibiblia. Lakini Paulo alikuwa na habari njema, pia! Ikiwa Timotheo angalifanya kazi kwa bidii, angemwona Mungu akileta ndani mavuno ya ajabu!.




**Soma 2 Timotheo 3:10, 11**
[10] Bali wewe umeyafuata mafundisho yangu, na mwenendo wangu, na makusudi yangu, na imani na uvumilivu. [11] na upendo, na saburi, tena na adha zangu na mateso, mambo yaliyonipata katika Antiokia, katika Ikonio, na katika Listra, kila namna ya adha nilivyoistahimili, naye Bwana aliniokoa katika hayo yote.

### 4.2 Paulo alimshaurije Timotheo?

Jinsi Barnaba alivyomshauri Sauli, Paulo naye alimshauri Timotheo – kwa kuhudumu pamoja.

Kulikuwa na nyakati darasani" ambamo Paulo alifunza "mafundisho ya dini," lakini masomo ya Timotheo yalienea mbali zaidi. Alisoma "namna ya maisha" ya Paulo – akijifunza kutenda kama alivyotenda Paulo, si vile alivyosema tu. Alipatwa na mateso pamoja na Paulo, akiongeza imani yake ndani na kulikuza tunda la roho.

Uanafunzi hufanyika mara nyingi katika njia za maisha, siyo kwenye viti kanisani au madawati darasani. Tunahifadhi masomo yetu tu kwa kuyaweka katika mazoea na kuyakabidhi kwa wengine na kufanya wanafunzi.

Kama Paulo alivyofanya wanafunzi, alitumia "kanuni hiyo aliyoiona Baranaba akitumia: "Kamwe usiwahi kufanya huduma peke yako."

**Hatua za**

**Mtatumiaje kanuni ya "kamwe usifanye huduma peke yako?"** *Tazama maswali 13,14,15 and 23 kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*


- Kila mara jiulize nani unaweza kupatana naye.
- Tafuta watu unaoweza kuushiriki moyo wako na maono yako.
- Chunguza nani anayetaka kutembea nawe kwenye nira ya uongozi wa kiutumishi.
- Kumbuka ya kuwa viongozi wapya hujifunza vyema kutokana na uzoefu wa maisha, siyo madarasani.

## Hatua za Kwanza

 ©2005 e3 Partners Ministry 

### 4.3 Je, kanuni ya kukoleza ni nini?

Yesu alitumia "Kanuni ya kukoleza." Angalia kwa maanani mchoro uliopo hapa chini. Aliwekeza kiwango kikubwa zaidi cha wakati wake ndani ya wanaume wachache ili kuwawezesha kuwa viongozi na kuwafundisha wengine ili nao wawafunze wengine hadi atakaporudi. Ni dhahiri ya kwamba alitumia muda zaidi na wale wanafunzi kumi na wawili kuliko mtu mwingine yeyote. Lakini hata miongoni mwa wale kumi na wawili, alitumia muda zaidi na Petero, Yakobo na Yohana kuliko alivyofanya na wengine tisa.




**KANUNI YA KUKOLEZA**

Hatua za kwanza

**Je, una watu wa aina hii maishani mwako?**

*Tazama swali la (24) la mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

**Ikiwa sivyo, mwulize Mungu akupe wako mwenyewe.**

| | |
|---|---|
| **Barnaba** | -Mtu wa kukutia moyo, na ambaye waweza kumtia moyo. |
| **Paulo** | -Mtu wa kufundisha na kukushauri. |
| **Timotheo** | -Mtu unayeweza kumfundisha na kumshauri kwenye uongozi. |

**HATUA ZINAZOFUATA**

Vifaa vingi bora vya kuendeleza uongozi vinaweza kupatikana. Hapa chini kuna orodha ya vifaa kadha wa kadha tunavyopendekeza kwa kukusaidia kuwakuza viongozi wapya wenye maono ya kuanzisha makanisa mapya. Kumbuka: Ni muhimu kutumia vifaa vilivyo sawa kwa ajili ya watu unaowafundisha!

**Kwa kuwasaidia <u>waumini</u> kukua wawe watendakazi -**

- *Maisha mapya katika Kristo* , sehemu ya kwanza
- *Maisha mapya katika Kristo*, sehemu ya pili

Vifaa hivi vinapatikana katika lugha kadha kwenye mtandao: *http://www.nuevavidaencristo.org/*

**Kwa Kuwasaidia watendakazi kukua ili wawe wachungaji na viongozi -**

- **Tumia kitabu hiki cha maelezo cha hatua za kwanza!** unaweza kupata nakala za ziada kwenye *www.e3partners.org*.
- **Ndiyo twaweza:** Huu ni utaratibu wa mafunzo unaowasaidia watendakazi kukua ili wawe viongozi wa kuanzisha kanisa . Kifaa hiki kinapatikana kwenye mtandao kwenye *www.reachperu.com,/MinistryTools/index.htm*
- **Utaratibu wa kufunza kwenye chuo cha Biblia kwa wachungaji (BTCP)** Kifaa hiki ni cha sehemu kumi ya vifaa vinavyompa kiongozi ufahamu wa kimsingi wa Bibilia.
  - Kusudi la BTCP ni kutoa mafundisho yenye msingi wa Biblia yanayopita mipaka ya dini kwa wachungaji na viongozi, ambao watawahamasisha vilivyo na ifaavyo na maarifa ya lazima kwa ujuzi wa utendaji katika kazi ya huduma ya kanisa la pale pale.
  - Lengo la BTCP ni kuelimisha waumini katika maarifa ya misingi ya Biblia na ujuzi wa huduma, matumizi sawa ya Neno la Mungu katika huduma, kukua kwa kiroho, kuhimiza uzalishaji, na kuwatia changamoto wanafunzi kutii Neno la Mungu .
  - Filosofia ya BTCP ya elimu ya thiolojia ni mwelekeo usio wa kitaaluma usio rasmi kwa kuhamasisha maarifa ya kimsingi ya Biblia na ujuzi wa kihuduma na mazingara ya uhusiano wa mmoja kwa mwingine.
  - Unaweza kupata taarifa zaidi juu ya BTCP kwenye mtandao: *www.bibletraining.com*
- **Mfululizo wa masomo ya Omega**
  Huu ni utaratibu wa mafunzo ulioundwa na muungano wa ukoleaji wa uanzishaji makanisa. Hii seti ya vitabu vitano vya maelezo ya kufunza. Kila kimoja kikiwa na masomo ishirini na sita. Kimebuniwa kutoa mafunzo ya kithiolojia na ujuzi wa utendaji huduma, kwa ajili ya wafanya kazi kukua wawe waanzishaji wa makanisa.

## HATUA ZINAZOFUATA

Kwa habari zaidi juu ya mfululizo wa masomo ya " Omega," tazama habari chini ya hatua hizi zinazofuata.

Je bado una moyo wa kupenda kushauriwa na viongozi waliohitimu na wenye ujuzi? Jiunge na mtandao wa *www.mentorandmultiply.com*: (na upige kidoko)

- " Washauri walioorodheshwa ambao watakufunza bila malipo"

Je, ungependa habari zaidi jinsi unavyoweza kushauri viongozi katika kanisa au shirika lenu? Nenda kwenye mtandao wa *www.mentorandmultiply.com* (upige kidoko)

- **"Washauri viongozi vile Yesu na Paulo walivyofanya."**

Je, mnahitaji msaada mkikuza viongozi kuwa wachungaji wa makanisa mapya? Mikusanyiko yote ya kitamaduni na vikundi vya nyumba vinaweza kuzidisha makanisa mapya kwa haraka, wanavyoweza kufunza wachungaji wapya na kuwafanya wanafunzi wapya. Wachungaji wengine huenda wasihitimu kama wazee viongozi wa kibiblia, bali wanaweza kutoa uongozi wa uchungaji kwa mikusanyiko midogo. Vifaa hivi vinaweza kuwasaidia kufunza na kushauri wachungaji wote wapya na waliokomaa zaidi ambao wanaweza kutumia vifaa hivi kufunza wengine kwa zamu. Nenda kwenye mtandao: *www.Paul-Timothy.net/* kwenye "download" upate vifaa vya bure.

*http://www.2tim2.org* ni mtandao wenye lugha nyingi ambao unatoa vitabu vingi, nakala na maelezo yanayoendelea ya viongozi wakristo katika ulimwengu unaoendelea. Lugha zinazotumika kwa sasa ni pamoja na Kiingereza, Kihispanyora, Kifaransa na Kirusi.

Chapa zinazoruhusiwa kutolewa ni pamoja na

- "Kukua kama Kiongozi – Mtumishi"
- "Je, ni kitu gani ambacho wakristo wafaa wajue juu ya mavuno ya nyakati – za mwisho." Wakitumia ukweli wa kibiblia kwa maisha.
- "Sasa kwa vile uko wake," Rasilimali nzuri ya viongozi kutumia katika kufundisha waumini wapya.
- "Kitabu cha Maisha" – kinatumia maandiko kuhudumu ifaavyo.

Je mnataka kujiunga na masomo ya bure katika uongozi wa kikristo kwenye tarakilishi kuu ya mtandao? Mifululizo mingi inapatikana pia.

Sehemu hii ni pamoja na ungo la utafsiri wa bure. Jiunge na tarakilishi kuu kwenye mtandao wa: *http://www.freechristianleadertraining.org/prod01.htm*

## HATUA ZINAZOFUATA

**Kwamasomo Zaidi**

Mfululizo wa masomo ya "Omega" juu ya "uongozi" Yanapatikana kwenye "mtandao" wa *http://www.alliancescp.org/resources/Omegacourse.html*

Kitabu cha maelezo cha pili:

- **Somo la kwanza**. "Kanuni za Kibiblia za Uongozi".
- **Somo la pili**. "Sura ya Kiongozi"

Kitabu cha maelezo cha tatu:

- **Somo la tatu**. "Maeneo ya Uongozi"
- **Somo la nne**. "Utangulizi kwa Kazi ya Pamoja"
- **Somo la tano**. "Maendeleo ya Pamoja"

**Kitabu cha maelezo cha nne:**


- **Somo la sita**. "Uongozi wa Mtumishi"
- **Somo la saba**. "Elimu ya Uongozi"
- **Somo la nane**. "Mitindo ya Kutendeana"
- **Somo la tisa**. "Mahitaji ya Uongozi"
- **Somo la kumi**. "Kuwafundisha Viongozi Wapya"

**Kitabu cha maelezo cha tano:**

- **Somo la kumi na moja**. "Kuwaweka huru Viongozi"
- **Somo la kumi na mbili**. "Uongozi wa Mwendo au mfumo"

 ©2005 e3 Partners Ministry 

 ©2005 e3 Partners Ministry 





## Hatua za Kwanza



**KUZIDISHA**

 ©2005 e3 Partners Ministry 



# KUZIDISHA KANISA LENU

**MAWAZO MAKUU**

- Kila mwanafunzi ana wajibu katika kuzidisha Kanisa.
- Changamoto yenu ya "Hatua za Kwanza " ni kuamua jinsi mtakavyotii Matendo 1:8.

## 1. FUMBO LA MAVUNO KUZIDISHA

Kila kitu duniani kiliumbwa kiweze kuzidisha - Adamu na Hawa, wanyama wa mwitu, ndege wa angani, samaki wa baharini na kila mmea uzaao mbegu.

Kanisa liliundwa na Mungu kuzidisha pia.

Kutoka chumba kimoja huko Yerusalemu siku ya Pentekoste hadi kanisa lenu katika mji wenu leo, Mungu alitia uwezekano wa kuzidisha.

Kama Adamu, mchwa na mitofaa (apple trees) kanisa ni kiumbe chenye uhai. Silo jengo, chuo au dhehebu,ingawa mwanadamu amejaribu mara kwa mara kuiga mpango wa Mungu kwa kujaribu kuufanya hivyo. Kanisa kama kila kitu kingine ambacho Mungu aliumba "vizuri sana" linakusudiwa kuweza kuzaa sana, kuzidisha na kujaza dunia. Rasilimali za kuzidisha makanisa ziko katika mavuno.

Mwamini yeyote afaa awe mwanafunzi. Nyumba ya kila mwanafunzi, yaweza kuwa Kanisa. Na kila kanisa lafaa liwe chuo cha mafunzo!

## 2. JE MAONO YAKO YANA UKUBWA ULIONUIWA NA MUNGU?

"Funga macho yako na utazame mashamba!" Yesu akasema "yako tayari kwa mavuno" ikiwa unamwamini , utabadilisha jinsi kanisa lako linavyofanya kazi.

**Soma Matendo 1:8-11 tena**
8 "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi
mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote, na Samaria,
na hata mwisho wa nchi." 9 Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama,
akainuliwa wingu likampokea kutoka machoni pao. 10 Walipokuwa wakikaza macho
mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu
nao, wenye nguo nyeupe. 11 "Wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama
mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu
mbinguni atakuja jinsi hiyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni."

## Hatua za Kwanza

 ©2005 e3 Partners Ministry 

## 2.1 Je, hii yatuambia nini kuhusu uanzishaji wa makanisa leo?

Aya hizi hazikuwa tu zimetengwa kwa ajili ya watakatifu waliokuwa huko Yerusalemu karne ishirini zilizopita. Yerusalemu ni pale unapoishi. Yudea na Samaria ni mbali kutoka pale unapoishi. Na "mwisho wa Dunia" bado ni mwisho wa Dunia.

Muhimu zaidi kuliko matumizi ya kisasa, ni yale mambo makuu Yesu aliyoeleza.

La kwanza, atuonya vile alivyowaonya wanafunzi wake wa kwanza ya kuwa uwezo wetu kutekeleza mpango wa kupanua Ufalme wa Mungu unategemea kupokea kwetu nguvu za Roho Mtakatifu.

La pili, Tume Kuu daima itatushurutisha kwa vyovyote kijogrofia na kitamaduni kuenenda zaidi ya nyumbani kwetu.

La tatu, Yesu anarudi tena, na tunataka tuwe tukitii amri zake arudipo. Amri zake ni za lazima na papo kwa hapo. Siyo pengine au baadaye. Na ikiwa tunamtaka Yesu arudi kwa Kanisa tiifu, ni afadhali tuache kusimama na kutazama kwenye wingu kama wanafunzi wake wa kwanza (*Matendo 1:10-11*) na tushughulike.

Katika kitabu hiki cha maelezo, mmekuwa mkiomba na kujadiliana kuhusa changamoto cha Hatua za Kwanza. Kwa kutumainiwa mmekuwa mkijaza kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi, mwishoni mwa kitabu hiki cha maelezo.

Sasa twataka kukutia changamoto kumwuliza Mungu ikiwa maono uliyonayo ni makubwa na ya kutosha! Mengi ya maono yetu ni madogo sana. Mwulize Mungu adhihirishe maono yake makubwa zaidi kwako na kanisa lenu, ukitarajia kwamba yatakuwa makubwa zaidi kuliko uwezavyo kuwazia au kufikiria wala kutimiza.

## 2.2 Je kuanzisha makanisa ni kanuni ya kibiblia?

Fungu "Uanzishaji makanisa" halipo katika Biblia. Je, tunajuaje ni ya Kibiblia?

Swali zuri. Hakuna chochote katika maandiko inayotuamuru moja kwa moja "kuanzisha makanisa mapya." Lakini tunawezaje kutumaini kutii Tume Kuu ya Kristo bila kuanzisha makanisa mapya?

Jaribu kuwazia juu ya kanisa moja – tangu siku ya pentekoste- ambalo washiriki wake walinena maelfu ya ndimi (lugha) likadumu vizazi hamsini na mamia ya tamaduni, lilienea kupitia mataifa mengi katika mabara yapatayo sita.

Jinsi gani ungependa kuwa mchungaji wa Kanisa kama hilo?

Haiwezekani!

Kwa hivyo kama Yesu anatuamuru tuwe mashahidi wake na kuwafanya wanafunzi kote Duniani, bila shaka anataka tuwakusanye wanafunzi hawa kwenye makanisa – kama vile, alivyowalisha watu elfu (5,000) tano, aliwakusanya kwenye vikundi vya watu hamsini ili waweze kusimamiwa kwa urahisi zaidi.

Wanafunzi zaidi wanahitaji makanisa zaidi. Kuzidisha wanafunzi, anzisha makanisa. Na kuzidisha makanisa, fanyeni wanafunzi.

**Soma Matendo 1:8 tena**
8 "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yeursalemu, na katika Uyahudi wote na Samaria na hata mwisho wa nchi."

### 2.3 Je, Matendo ya mitume 1:8 ilipeanwa kwa nani?

Aya hii inahusu marudio kwa sababu Mungu aliipeana kwako mwenyewe. Miaka elfu mbili iliyopita, aliongea nawe moja kwa moja akasema, "Fanya wanafunzi watakaobadilisha ulimwengu! Anzia mji wako na pia uendelee mbele."

Aliongea pia kwa kanisa lako,sio tu mwili wa Kristo kote ulimwenguni, au hata dhehebu moja au mwungano. Yesu anataka kulitumia kanisa lenu – liwe kubwa au dogo – kuwaandaa viongozi na watendakazi kwenda kokote katika mji mwenu, halafu waendelee katika sehemu za mbali.

## 3. CHANGAMOTO YA MATENDO 1:8

### 3.1 Hatua ya kwanza: Mungu anakutuma wapi?

**Yerusalemu -** Mahali popote muhimu karibu na eneo la kila siku la ushawishi wa kanisa lenu. Sasa hivi chukua muda mfupi kumwomba Mungu akupe maono yake kwako na kwa kanisa lenu. Kutambua Yerusalemu yenu huwa rahisi sana. Mwulize Mungu athibitishe mipaka ya Yerusalemu yako ya kipekee, uiandike kwenye ramani ya changamoto ya Matendo 1:8.

**Uyahudi -** Ni mahali maalumu popote karibu na eneo la mamlaka la kanisa lenu na wanaoshiriki nia sawa juu ya ulimwengu. Mwulize Mungu athibitishe mahali Uyahudi wako uliko, yawezekana kuwa nje ya jiji lenu, lakini lazima liwe katika jimbo au mkoa wenu. Andika jina la Uyahudi wako katika ramani ya changamoto ya matendo 1:8

**Samaria** – Ni mahali popote maalumu nje ya eneo la mamlaka ya kanisa lenu, ambalo lina nia tofauti juu ya ulimwengu unayohitaji mawasiliano yavukayo mipaka ya tamaduni yenu, lakini linashiriki tabia zilizo sawa. Kiwango hiki chaweza kuwa karibu au mbali. Chukua muda mfupi sasa ukamwulize Mungu athibitishe mahali Samaria yako iko. Yaweza kuwa:

- Nje ya jimbo au mkoa wako, lakini ndani ya nchi yako.
- Kikundi kilicho karibu nawe kinachoongea lugha zingine au kina desturi tofauti.
- Kikundi cha kijamii cha kiuchumi ambacho ni tofauti sana kuliko chako.
- Kikundi cha watu waliokataliwa na tamaduni zenu kinachojumlisha waathiriwa wa madawa ya kulevya, makahaba, wasenge, wafungwa na watu wasio na taifa rasmi.

Liandike jina la Samaria yako kwenye ramani ya changamoto ya Matendo 1:8

**Mwisho Wanchi** ni mahali popote, maalum nje ya eneo la mamlaka ya kanisa lenu, wenye nia juu ya ulimwengu uliyo tofauti sana, uliyo na tabia chache zilizo sawa ikiwa kutakuwa na zozote. Kiwango hiki mara nyingi huwa mbali sana kijiografia. Yesu aliposema "mwisho wa nchi" alionyesha kuwa upanuzi wa Ufalme wa Mungu hauna mipaka, na kanisa lenu halina mipaka, Mungu anapoongoza. Uwe mkubwa au mdogo, tajiri au masikini, anaongoza na kukupa rasilimali, unahitaji kufuata, usiache uwoga na shaka ikunyate maono ya kanisa lenu . Andika jina la "mwisho wa nchi yako" katika ramani ya changmoto ya matendo 1:18

**Hatua za kwanza**

**Mtazidisha kanisa lenu wapi?**
*Tazama swali la 25 Kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi*

**3.2 Hatua ya Pili: Mko wapi leo?**

Upande wa kushoto chini ya ramani ya changamoto ya Matendo 1:8 kuna vikundi vinne:

**Maombi** – Ni huduma gani inayoendelea katika eneo unaloombea. Pengine unaombea huduma ambazo wewe unahusika au labda waweza kuwa unaombea huduma nyingine amabazo umesikia juu yake. Andika habari hii katika ramani ya changamoto ya, Matendo 1:8. Ikiwa huombei huduma yeyote, wakati wowote, katika eneo fulani, iache tupu.

# JEDWALI LA CHANGAMOTO YA MATENDO 1:8

| Wapi → / ↓ Nini | Yerusalemu kwetu ni: | Uyahudi kwetu ni: | Samaria kwetu ni: | Mwisho wan chi ni: |
|---|---|---|---|---|
| **Maombi** | | | | |
| **Miradi** | | | | |
| **Ushirikiano** | | | | |
| **Viongozi wa kila eneo** | | | | |

**Miradi** – Miradi ni matukio ya wakati mmoja. Safari za umisheni na matukio ya kiuinjilisti ni mifano ya miradi. Je unahusika katika miradi gani ya huduma? Andika habari hii kwenye ramani ya changamoto ya Matendo 1:8. Ikiwa hamna mradi wa huduma katika eneo maalumu iache tupu.

**Ushirikiano –** Ushirikiano ni uhusiano wa huduma unaoendelea kwa muda fulani. Kanisa lenu laweza kuanzisha kanisa jipya na kulisaidia likue, huo ni ushirikiano. Kanisa lenu laweza kutuma na kuwasaidia wamishonari katika Uyahudi wako, Samaria na mwisho wa ulimwengu hiyo ni aina nyingine ya ushirikiano. Waweza kufanya kazi na kanisa jingine, dhehebu au kituo cha makili ya umisheni kuanzisha makanisa katika sehemu nyingine ya ulimwengu-huo ni ushirikiano unaoendelea. Kama una aina zozote za ushirikiano kwa sasa, andika habari hii kwenye ramani ya changamoto ya Matendo 1:8. Ikiwa huna ushirikiano wa kihuduma katika eneo maalum, iache tupu.

**Uongozi** – Viongozi gani umekwisha kuwa nao katika maeneo haya? Maeneo yapi bado yanahitaji viongozi? Andika habari hii kwenye ramani ya changmoto ya Matendo 1:8.

### 3.3 Hatua ya tatu: Je una mpango gani wa kuzidisha?

Hili ndilo swali kuu! Bwana utatupanuaje kuingia katika huduma mpya na maeneo mapya?

Chukua dakika chache kuandika katika ramani ya changamoto ya Matendo ya mitume 1:8 unavyo mwamini Mungu katika kukuongoza kupanua huduma yako wakati ujao. Yafaa uteue tu viongozi mbalimbali miongoni mwa kanisa lako kutetea eneo lao waliokabidhiwa. Jiulize:

- Nani atakayeongoza?
- Tutalenga wapi?
- Tutafanya nini?
- Tutaifanyaje?

Kitabu cha Matendo hakina mwisho wa kialisi. Hadithi inaanza hapa bali hatujifunzi jinsi inavyojitokeza nje mpaka tunapoingia sana katika kitabu cha Ufunuo, mahali tunaposoma:

> Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila , na jamaa na lugha wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi , na mbele za mwana-kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao [10] wakilia kwa sauti kuu wakisema Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi , na mwana – kondoo." (*Ufunuo 7:9-10*)

## Hatua za Kwanza

Walitoka wapi? Kutoka makanisa yanayoonyesha kila taifa, kabila, watu na lugha!

Kitabu cha Matendo ya Mitume bado kinaandikwa. Wewe na kanisa lako ni miongoni mwa waandishi wake.

**Hatua za kwanza**

**Kusanyikeni na viongozi wengine waliopo leo kutoka kanisa lako, mkaanze kupata maono ya wajibu wa kanisa lako katika kukamilisha kitabu cha Matendo ya Mitume. Acha maswali yafuatayo yaongoze majadiliano yenu:**

- Je, jamii yenu ingeonekanaje ikiwa kila mtu angalisikia Injili?
- Viongozi wengi wanaamini ya kuwa kanisa moja linahitajika kwa kila watu elfu moja.
  Itachukua makanisa mangapi ya kiasi hiki kufikia jamii yako?
  Ni makanisa mangapi yapo sasa?
- Tukizingatia tamaduni zilizowakilishwa katika shamba lako la mavuno, kanisa lafaa lionekanaje kama linaenda kufikia shabaha ya watu munaokusudia kufikia?
- Ni vizuizi gani unavyoweza kuona mbele katika huduma ya kuanzisha makanisa yatakayoongezeka katika shamba hilo la mavuno?
- Rasilmali zinapatikana wapi katika shamba lako la mavuno? Kumbuka ya kwamba rasilmali za uzalishaji zimo katika mavuno. Ukumbuke pia ya kuwa udongo ulio bora kwa kuanzisha kanisa mara nyingi ni watu wabaya.
- Utapashaje maono ya uzalishaji yanayohimiza kila kanisa kutii Matendo 1:8?

Utakuwa aliyefaulu zaidi ukifanya kazi kwenye viwango vingi mara moja, badala ya kiwango kimoja kwa wakati. Anza kwa kutafuta watu katika kanisa lako kuongoza, timu za Yerusalemu, Yudea na Samaria vile vile na “timu ya mwisho wa nchi”

Halafu kila mojawapo ya hizo timu nne itambue njia kanisa lako limekwisha husika katika eneo lao la shabaha na kulisisimua kanisa kuelekea kuzidisha katika eneo hilo. Anzia mahali uliopo na uendelee kwenye eneo la nje. Hivi punde utakuwa na maono yaliyo dhahiri na yafaayo kuanzisha makanisa.

 ©2005 e3 Partners Ministry 

**HATUA ZINAZOFUATA**

Soma kijitabu chenye kichwa mwendo au mfumo wa kuanzisha makanisa, kinachotolewa na Halmashauri ya Tume ya Kimataifa ya Mkutano wa Baptisti ya Kusini (International Mission Board of the Southern Baptist Convention). Kijitabu hiki kinapatikana kwenye mtandao: *http://imb.org/cpm/*

Jifunze mengi kuhusu asili ya mambo ya kuanzisha makanisa kwa kusoma kitabu kinachohusu jinsi ya kuvunja ardhi ngumu kilichoandikwa na David Garisson kinapatikana kwa mtandao na chaweza kutolewa chapa bure kwenye
*http://currah.info/www./paul-timothy/docs/garrison_cp_movements.pdf*
Soma kuhusu Uhuru wa aina tisa tofauti wa mwendo wa kuanzisha makanisa kwenye *http://currah.info/www/pauil-tumity/docs/nine-freedoms.pdf*

Mwongozo wa kuzidisha makanisa wa George Patterson unapatikana kwa mtandao pamoja na uhuru wa kuitoa chapa kitabu chote kwenye *http://currah.info/www/cmg/*

Jambo la muhimu la kuzingatiwa unapofikia watu na kuanzisha makanisa yanayozalisha miongoni mwa watu tofauti ni kufahamu kupitia utafiti. Kama vile kanisa lako linavyojitokeza kufikia Uyahudi wa kwako, na meneo ya mbali sana, utumie mtandao kupata ufahamu wa mambo hayo ili uwe wa kufaa zaidi katika kupanga kwako.

Vikundi vya watu wa utafiti, Nchi na Utamaduni, muziki, sanaa, lugha, habari za jamii ya ulimwengu. Jiunge na mtandao wa tarakilishi kuu kwa kujiunga na moja wapo wa anwani zifuatazo:-

- *www.virtualresearch.org.*
- *http://www.strategyleader.org/*
- *http://www.peopleteams.org/Selection.htm.*
- *http://www.gmi.org/research/index.htm*
- *http://www.gmi.org/ow/updates/website.html*
- *http://www.worldchristiandatabase.com/wcd/default.asp*
- *www.mislinks.org/*

Soma kuhusu kanuni 19 za tume inayopatikana katika kitabu cha Matendo kwenye *http://currah.info/www/paul-timothy/docs/19principles_acts.pdf*.

Kuna rasilmali nyingi za kuanzisha makanisa kwenye
*www.churchplantingvillage.com*


**Kwa mafunzo zaidi ya kuzidisha makanisa:**
Mfululizo wa masomo ya Omega "maono" ya kuzidisha makanisa yanapatikana kwenye mtandao kwenye *http://www.alliancescp.org/resources/omegacourse.html*

**Kitabu cha maelezo cha Nne**
**Somo la 10** "Viungo vya mkakati wa mwendo au mfumo wa kuanzisha makanisa"
**Kitabu cha maelezo cha Tano**
**Somo la 14**. "Uhamasishaji"
**Somo la 15**. "Hatua zinazofuata"
**Somo la 16**. "Kufundisha kama sehemu ya mwendo au mfumo wa kuanzisha makanisa."

## Hatua za Kwanza

 ©2005 e3 Partners Ministry 

 ©2005 e3 Partners Ministry 




**Hatua za Kwanza**

 ©2005 e3 Partners Ministry 

# JITOLEE KATIKA KUANZISHA MAKANISA.

**MAWAZO MAKUU**

- Mungu ni mwenye enzi, na atatimiza makusudi yake kwa vyovyote vile ikiwa tunatii au hatutii.
- Tunapokosa kutii, aweza kutusukuma kwenye utiifu. Ama twaweza kukosa baraka Zake anapochagua wengine kuyatimiza makusudi Yake.
- Changamoto yako ya hatua za kwanza ni kuchukua hatua za kwanza za kutii amri za Mungu kwa kutekeleza kile umejifunza.

## 1. WAMISHONARI WASIOTII

**Soma Matendo ya mitume 1:8 tena**

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote na Samaria na hata mwisho wa nchi."

### 1.1 Je, Yesu hakuwa dhahiri kuhusu mahali wanafunzi walikuwa waende?

Yesu hakuacha shaka yoyote kuhusu mahali wanafunzi walikuwa waende. Alisema Walikuwa wawe mashahidi wake "katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote na Samaria, na hata mwisho wa nchi." Lakini katika sura saba za kwanza za Matendo ya Mitume, walikaa Katika Yerusalemu. Naye Mungu alisaidia kuwatia motisha.

**Soma Matendo 8: 1b, 4-8**

8.1------ Siku ile kukatukia adha kuu ya kanisa lililokuwa katika Yerusalemu; wote Wakatawanyika katika nchi ya Uyahudi na Samaria , isipokuwa hao mitume.
4 Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno. 5 Filipo Akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo.
6 Na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliosemwa na Filipo walipoyasikia na kuziona ishara alizokuwa akizifanya. 7 Kwa maana pepo wachafu wakawatoka wengi waliopagawa nao, wakilia kwa sauti kuu; na watu wengi waliopooza, na viwete, wakaponywa. 8 Ikawa furaha kubwa katika mji ule.

**Soma Matendo 8: 14 na 9:31**

**8:14** Na mitume walikuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu,Wakawapelekea Petro naYohana . . . . . . .

**9:31** Basi Kanisa likapata raha katika Uyahudi wote na Galilaya na Samaria, likajengwa, likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana, na faraja ya Roho Mtakatifu.

**1.2 Je Mungu aliwalazimishaje wanafunzi kuutimiza mpango wake?**

Wanafunzi walipokosa kutii Tume Kuu, Mungu alitumia mateso kuwatia motisha. Bila kuonywa wakawa wamishonari wasiokusudia kwa Uyahudi na Samaria Mungu aliwatumia watu wasiotii kutimiza mpango wake .Mpango wake haukukoma hata ingawa watu wake hawakutii.

**1.3 Je matokeo yalikuwa nini?**

Mara moja tu wanafunzi walipofika mahali ambapo Mungu alikuwa amewaambia waende na wakafanya kile aliwaambia wafanye, walikuwa na amani wakaimarishwa na idadi ya makanisa ikaongezeka.

**Soma Matendo 11: 19-26**
19 Basi wale waliotawanyika kwa sababu ya ile dhiki iliyotukia kwa habari ya
Stefano, Wakasafiri hata Foinike na Kipro na Antiokia, wasilihubiri lile neno ila
kwa Wayahudi peke yao. 20 Lakini baadhi ya hao walikuwa watu wa Kipro na
Kirene, nao walipofika Antiokia wakasema na Wayahudi wa Kiyunani, wakihubiri
habari njema za Bwana Yesu. 21Mkono wa Bwana ukawa pamoja nao , watu wengi
wakaamini, wakamwelekea Bwana 22 Habari hizo za watu hao zikafika masikioni
mwa kanisa lililokuwako katikaYerusalemu; wakamtuma Baranaba , aende hata
Antiokia . 23 Naye, alipokwisha kufika na kuiona neema ya Mungu akafurahi,
akawasihi wote waambatane na Bwana kwa kusudi la moyo. 24 Maana alikuwa mtu
mwema amejaa Roho Mtakatifu na imani; watu wengi wakaongezeka upande wa
Bwana . 25 Kisha akatoka akaenda Tarso kumtauta Sauli. 26 hata alipokwisha
kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika
pamoja na Kanisa na kuwafundisha watu wengi . Na wanafunzi waliitwa Wakristo
kwanza hapo Antiokia.

**1.4 Nani alianzisha kanisa la Antiokia?**

Wakati "Wamishonari wasiokusudia" walitoroka katika Yerusalemu, wengine walienda kaskazini maili mia mbili kwenda Antiokia, wakaanzisha kanisa na waumini wapya. Halafu "kanisa zazi" katika Yerusalemu likamtuma Barnaba kuliongoza. Lakini Baranaba hakufanya kazi peke yake .Kwa zamu yake, alienda Tarso kumtafuta Sauli ili amlete katika timu yake ya uongozi.

## Hatua za Kwanza

## 2. WAMISHONARI WATIIFU

**Soma Matendo 13:1-5**
1Na huko Antiokia katika kanisa lilokuwako palikuwa na manabii na waalimu,nao
ni Barnaba na Simioni aitwaye Nigeri,na Lukio Mkirene, na Manaeni na aliyekuwa
ndugu wa kunyonya, mfalme Herode, na Sauli.
2 Basi hawa walipokuwa
wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni
Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia.
3Ndipo wakiisha kufunga na kuomba,
wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao.
4Basi watu hao,wakiisha
kupelekwa na Roho Mtakatifu wakatelemkia Seleukia, na kutoka huko wakasafiri
baharini hata Kipro.
5Na walipokuwa katika salami wakalihubiri neno la Mungu
katika masinagogi ya Wayahudi, nao walikuwa naye Yohana kuwa mtumishi wao.

**2.1 Je, Barnaba na Sauli walikuwa wamishonari watiifu au wasiotii?**
Barnaba na Sauli wote walimsikiliza Mungu mara moja. Walienda mbali na Yerusalemu, Uyahudi na Samaria hata "mwisho wa nchi" kulingana nao.

## 3. ADHABU YA KUTOTI

**3.1 Nini hufanyika hasa tunapokosa kutii mwito wa Mungu?**

Wakati mwingine anatulazimisha kutii kupitia kwa vitu kama dhiki.

Nyakati zingine, anatukubalia kutotii na kuwa na "maisha ya kawaida" vile alivyofanya na Waisraeli walipokataa kwenda nchi ya ahadi. Walikuwa wamengojea kwa miaka mia nne kurudi Kanaani na wakashuhudia miujiza ya ajabu sana. Hata hivyo, wakati ulipotimia kunyakua nchi, walikataa.

**Soma Joshua 5: 4-6**
4. Na sababu yaYoshua kutahiri ni hii, watu wote waliotoka Misri waliokuwa
waume, hao watu waume wote waendao vitani walikufa katika jangwa wakiwa
njiani baada ya wao kutoka Misri.
5 Kwa kuwa watu wote waliotoka walikuwa
wamekwisha kutahiriwa; lakini watu wote waliozaliwa katika jangwa wakiwa njiani
walipokwisha kutoka Misri, hao hawakutahiriwa.
6 Kwa kuwa wana wa Israeli
walitembea muda wa miaka arubaini jangwani, hata hilo taifa zima, yaani watu
waume waendao vitani waliotoka Misri, walipokuwa wameangamia kwa sababu
hawakuisikiliza sauti ya BWANA. Nao ndio Bwana aliowaapia ya kwamba
hatawaacha waione hiyo nchi ambayo Bwana aliwaapia baba zao kwamba atatupa
sisi, nchi ijaayo maziwa na asali.

 ©2005 e3 Partners Ministry 

### 3.2 Matokeo ya kutotii kwa Waisraeli yalikuwa ni yapi?

Badala ya matembezi mafupi kutoka Misri hadi Kanaani, Waisraeli walitangatanga jangwani kwa miaka arobaini (40). Viatu vyao na nguo zao havikuchakaa. Mungu aliwalisha akawapa maji safi. Waliishi maisha ambayo mbeleni yalikwa maisha ya "kawaida" kwao Mungu aliyajibu maombi yao-bali kama adhabu, si kama baraka.

Na mwishoni mwa miaka arobaini karibu kila roho ambayo ilikuwa imetoka Misri ilikufa ikazikwa chini ya mchanga. Vile mtu mwingine alivyosema hapo awali, "wakati mwingine kitu kibaya zaidi kinachotufanyikia si kile kinachotufanyikia, bali kisichotufanyikia."

Kizazi cha "la" kilikosa kila mojawapo ya baraka za nchi ya ahadi za Mungu. Wale aliowaokoa kwa ajili ya watoto wao ni kizazi cha "Ndiyo."

Na wewe je? Unajua mapenzi ya Mungu na mpango wake wa kuupanua Ufalme Wake. Je jibu lako ni gani?

**Soma Mariko 4:24-29**
24 "Akawaambia, Angalieni msikialo" kipimo kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa, na tena mtazidishiwa. 25 Kwa maana mwenye kitu atapewa, naye asiye na kitu hata kile alicho nacho atanyang "anywa." 26 Akasema,Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi, 27 akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua,asivyojua yeye.
28 Maana nchi huzaa yenyewe, kwanza jani, tena suke kisha ngano pevu katika suke.
29 Hata matunda yakiiva mara aupeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika.

### 3.3 Yesu anaahidi nini, ikiwa utakitumia ulichojifunza? Na je utakuaje usipotumia?

Kanuni ya Ufalme wa Mungu ni: Uitumie au uikose. Kwa maneno mengine, ninavyoendelea kuitumia, ndivyo nitakavyo pokea zaidi.

Ni kitumia nilichojifunza, napata maarifa zaidi. Bali mimi nikiwa ni msikilizaji tu na siyo mtendaji, Napoteza nilichokipokea.

### 3.4 Nani anayewajibika kwa mafanikio?

Mungu yumo ndani ya kazi inayofanywa kwa pamoja. Tunafanya sehemu yetu, Naye hufanya Yake.

Tunawajibika kuchukua hatua na kuzifuata Amri Zake. Panda mbegu. Fanya kazi kwa bidii. Yalete ndani mavuno.

Bali pia, tunawajibika kupumzika ndani ya Bwana, tukihakikishwa kwamba anatunza kila kitu.

Ni Mungu tu anayewajibika katika mafanikio.

## Hatua za Kwanza

**Hatua za kwanza**

**Ungependa kujitolea kwa tukio gani leo?**
*Tazama swali la 26 kwenye mkakati wa ukurasa wa utendaji kazi.*

- **HAMASISHA -** Utatumia kifaa hiki kuhamasisha na kuwafundisha wengine?

- **FANYA UINJILISTI -** Utashiriki Injili kwa angalau watu wawili kila Juma kwa mwaka mmoja?

- **IMARISHA -** Utaanzisha angalau kazi moja mpya (kanisa, kanisa la tume, kusanyiko la tume, kundi dogo, upanuzi wa Kanisa lako, na kadhalika) kwa muda wa miezi kumi na miwili ijayo?

Fomu ya kujitolea inafuata sura hii. Tafadhali ijaze na uirudishe kwa mwalimu au mkufunzi wako.

Unapotumia kitabu cha maelezo kuwaandaa ama kuwafundisha wengine waulize wajaze nakala ya fomu ya kujitolea pia. Halafu, unaweza –

- Peana fomu iliyojazwa kwa mwalimu au mkufunzi wako mwenyewe,ama
- Kutuma taarifa hiyo kwa kipepesi kwa afisi yetu katika Plano, Texas, USA (merikani) kwenye 214.440.1190, ama
- Nenda kwenye mtandao kwenye *www.e3partners.org* na utupe majibu yako.

Tunafurahia pamoja nawe wakati Mungu anapokutumia kupanua Ufalme Wake! Hebu Bwana akubariki kwa wingi, unapoendelea kumtumikia.

**HATUA ZIFUATAZO**

Elimu yenye mwelekeo wa utiifu inasema ya kuwa mara ukijifunza kitu, lazima ukiweke kwenye matumizi kabla ya kujifunza kitu kingine. Hii inatumika kwa kuanzisha makanisa yanayozalisha katika kijitabu cha bure kinachopatikana kwenye: *http://currah.info/www/paul-timothy/docs/obedience_oriented_ed.pdf*

# KUJITOLEA KWANGU
**(JAZA NA MPE MKUFUNZI AU MWALIMU)**

Jina lako_______________________________________________

Tarehe ya leo___________________________________________

Anwani yako____________________________________________

Nambari za simu_________________________________________

Barua Pepe_____________________________________________

Jina la kanisa lako_______________________________________

Anwani ya kanisa ________________________________________

Huduma ya (e3 partners) Tunatamani kumtukuza Mungu kwa kuyafanya mafunzo yetu yawe ya msaada sana iwezekanavyo. Tafadhali tusaidie kwa kuyajibu maswali yafuatayo.

1. Ni kitu gani ulichokipenda juu ya vifaa hivi na mafunzo?

2. Tunaweza kufanya nini ili tuvinufaishe zaidi?

3. HAMASISHA: Utajikabidhi kuwafunza wengine kile ulichojifunza kutoka kwa vifaa hivi? Ni watu wangapi unaotumaini kuwafunza kwa wakati wa miezi kumi na miwili (12) ijayo? Tafadhali chagua ifaayo:

☐ (10) watu kumi ☐ (50)watu hamsini ☐ (100)watu mia moja ☐ ___(Jaza idadi)

4. FANYA UINJILISTI: Utashirikisha injili kwa watu (2) wawili kila Juma kwa mwaka ujao?

5. IMARISHA: Utaanzisha angalau kazi moja mpya (kanisa, kikundi, kituo, kikundi cha maombi, upanuzi wa Kanisa na kadhalika) kwa wakati wa miezi kumi na miwili (12) ijayo? Ngapi?_________________________________________

Asante sana kwa maoni yako. Tafadhali tuombee unaporudi nyumbani!


Mungu akubariki!

 ©2005 e3 Partners Ministry 



 ©2005 e3 Partners Ministry 

HATUA ZA KWANZA

# MKAKATI WA UTENDAJI KAZI KWENYE KARATASI

| | | |
|---|---|---|
| **MAONO** | 1. Je Bwana anatuita tuanzishe kanisa jipya? | ❑ Ndiyo<br>❑ Siyo sasa |
| <br>Ombeni<br>vunjeni ardhi | 2. Je, ni lini kanisa letu litaombea mapenzi ya Mungu kuhusu kuanzisha makanisa? | Tarehe: |
| | 3Mungu anatuita tuanzishe kanisa jipya wapi? | Mahali: |
| | 4. Ni nani anayeweza kuwa mtu wa amani katika mahali hapo? | Majina: |
| | 5. Mungu anamwita nani kuwa kwenye timu ili asaidie kuanzisha kanisa jipya? | Majina: |
| | 6. Vizuizi gani vinahitajika kushindwa katika kanisa letu? Katika eneo ambapo Mungu anatuita tuanzishe kanisa jipya?<br>❑ Utepetevu (Apathy)<br>❑ Hofu<br>❑ Ngome ya dini<br>❑ Taathira ya ulevi<br>❑ Ulevi wa madawa<br>❑ Matumizi mabaya ya maumbile<br>❑ Dhambi za usherati<br>❑ Uislamu<br>❑ Tamaa ya vitu<br>❑ Ukosefu wa imani<br>❑ Uchawi<br>❑ Ufuasi wa John Smith na kitabu chake<br>❑ Mashahidi wa Yehova<br>❑ Vikundi vingine<br>❑ Na vinginevyo? | |
| | 7. Je, tuanzishe mnara wa maombi kuhamasisha maombi kwa kanisa jipya? | Mahali maalum |
| <br>Fanyeni Uinjilisti<br>Pandeni mbegu | 8. Tutatumia njia gani ya uinjilisti? | ❑ Kisanduku cha uinjilisti<br>❑ Kijitabu cha kibinafsi cha kushuhudia (e3 tract)<br>❑ Filamu ya Yesu<br>❑ Vinginevyo? |
| | 9. Je, ni lini tutapanga mafunzo ya uinjilisti kwa kanisa lote? | Tarehe |
| <br>Fanyeni Wanafunzi<br>leeni ukuzi au ukuaji | 10. NANI: Ni wanaume na wanawake gani wanao tegemewa na kuweza kuwa wanafunzi? | Majina |
| | 11, WEKEZA MUDA.Tutawezaje kuweka muda kwa wanafunzi wetu na kujenga uhusiano nao? | ❑ Ufuasi wa mmoja kwa mmoja<br>❑ Kiongozi wa jamaa afundisha jamaa<br>❑ Vikundi vya seli<br>❑ Vikundi vidogo<br>❑ Vikundi vya kusikiliza<br>❑ Na njia nyingine? |
| | 12. TII: Ni vifaa gani vya ufuasi tutatumia kufundisha wanafunzi wetu jinsi ya kumtii Yesu? | |
| | 13. MIFANO: Ni shughuli gani za huduma tunaweza kushiriki na wanafunzi wetu kuwasaidia kujifunza kwa kututazama? | |

 ©2005 e3 Partners Ministry 

| | | |
|---|---|---|
| <br>Fanyeni Wanafunzi leeni ukuzi | 14. **KUPEANA**: Ni kazi gani za huduma tunaweza kuwapatia wanafunzi wetu ili wakue? | |
| | 15**. SIMAMIA**: Je, tunahitaji kuwasimamia wanafunzi wetu juu ya kitu chochote sasa? Tunahitaji kuwasaidia wakiwa na shida? | |
| | 16. ZIDISHA: Je, ni wakati wa mwanafunzi wangu kupata mwanafunzi wake mwenyewe? Mabadiliko gani yanahitajika ili kufanya mwanafunzi kuwa na kipau mbele katika huduma yangu? | |
| <br>Kusanyikeni Pamoja Leteni mavuno ndani | 17. Ni hatua gani tunahitaji kuchukua kuimarisha maeneo dhaifu katika kanisa letu? | ❑ Uinjilisit<br>❑ Ufuasi<br>❑ Ibada<br>❑ Ushirika<br>❑ Huduma |
| | 18. Tutawakusanyaje hao waumini wapya pamoja katika eneo la kanisa jipya? | ❑ Vikundi vya seli<br>❑ Masomo ya Biblia ya nyumbani<br>❑ Vikundi vya kusikiliza<br>❑ Na vinginevyo |
| | 19. Watakutana wapi? | Mahali |
| | 20. Je, watakutana mara ngapi? | ❑ Mara moja kwa juma?<br>❑ Mara mbili kwa juma?<br>❑ Siku gani?<br>❑ Nyakati gani? |
| <br>Kuzeni Viongozi Kusanyeni mbegu za kupanda | 21. Ni mabadiliko gani ninayohitaji kufanya ili niwe mshauri bora kwa viongozi wapya? | |
| | 22. Je, nani hao wanaoweza kuwa viongozi wapya ili tuwaalike kusaidia kuanzisha kanisa jipya? | Majina |
| | 23. Tutafanya nini kushauri viongozi zaidi? Ni kazi gani katika huduma twaweza kuwapa viongozi wapya kuwasaidia kukua? Ni mafunzo gani zaidi wanayohitaji? | ❑ Timu ya huduma?<br>❑ Chuo cha mafunzo cha Biblia?<br>❑ Mafunzo ya Omega"<br>❑ Na vinginevyo? |
| | 24. Nani ni:<br>❑ Paulo anayenishauri?<br>❑ Timotheo ninayemfundisha?<br>❑ Barnaba anayenitia moyo? | Majina |
| <br>Zidisheni, panueni shamba la mavuno | 25. Tutazidisha kanisa letu wapi?<br>❑ Yerusalemu<br>❑ Uyahudi<br>❑ Samaria<br>❑ Mwisho wa ulimwengu | Maeneo haya yako wapi kwa ajili yetu? |
| | 26. Tutazidishaje huduma yetu? | ❑ Elimisha wengine na kifaa hiki?<br>❑ Fanya uinjilisti kwa majirani wako?<br>❑ Anzisha kanisa jipya? |

## Hatua za Kwanza

 ©2005 e3 Partners Ministry 

e3 Partners Ministry
2001 W. Plano Pkwy., Suite 2600
Plano, Texas, USA  75075
214-440-1101
First.Steps@ e3partners.org
*http://www.e3partners.org*

©2005 e3 Partners Ministry